

KITABU hiki kilikubaliwa na Bwana Askofu na Mapadre mwezi wa Septemba 1917; kikaamriwa kupigwa chapa, kwa idhini ya Bwana Askofu, katika mkutano mkuu wa Mapadre waliokutanika katika Kanisa la Hego-ngo, Muheza, Januari 22, 1918. Basi tokea sasa hapana amri ya kusoma Kitabu cha Ibada kinginecho katika makanisa yetu, ila hiki tu.

Basi, kila mtu afahamu ya kuwa hiki ndicho Kitabu cha Ibada na Sala kilichoamriwa kusomwa katika makanisa yetu yote. Hakuna ruhusa ya kusoma vinginevyo, wala kuvibadilibadili vilivyoagizwa humu.

✠ FRANK ZANZIBAR :

Siku Kuu ya Ufunuo, 1919.

Kwa kuwa ni nusu tu ya kitabu hicho cha 1919 iliyopigwa chapa upya 1925, na nusu ile iliyobaki inahitajiwa na Mapadre kwa Ibada za Kanisa letu ; kitabu hiki kilichopigwa chapa sasa ndicho chenye sehemu ile ya kitabu cha 1919 iliyobaki.

Basi umeonekana wakati wa kufaa kupanga upya na kuzidi kutengeneza mambo yaliyomo katika kitabu hiki, na tena kuongeza mengine yaliyohitajiwa ili kizidi kufalia Ibada na Sala za Kanisa.

Sasa Kitabu hiki kilivyo ndicho chenye idhini yetu.

✠ THOMAS ZANZIBAR :
✠ VINCENT MASASI :

Siku Kuu ya Pentekote, 1927.

FAHIRISI

| | uk. |
|---|-----|
| 1. Kufanya Wanafunzi | 1 |
| 2. Kupaka Mafuta Wanafunzi wa Ubatizo | 3 |
| 3. Ubatizo Utakatifu | 7 |
| 4. Ubatizo wa Watoto Wachanga | 13 |
| 5. Ubatizo wa Mgonjwa Kitandani | 19 |
| 6. Kutimiza Kawaida za Ubatizo | 21 |
| 7. Kubariki Maji Matakatifu | 25 |
| 8. Kushukuru kwa Mtu ye yote | 27 |
| 9. Kushukuru kwa Mwanamke | 29 |
| 10. Litania ya Kanisa | 33 |
| 11. Maji ya Baraka | 46 |
| 12. Missa Takatifu | 49 |
| 13. Uimbo wa Kushukuru | 77 |
| 14. Ghofira ya Wafu | 81 |
| 15. Ushirika pasipo Missa | 84 |
| 16. Ibada ya Baraka | 87 |
| 17. Kipa Imara | 89 |
| 18. Kutangaza Habari za Ndoa | 92 |
| 19. Ndoa Takatifu | 93 |
| 20. Kitubio cha Kanisa | 105 |
| 21. Toba | 110 |
| 22. Ushirika wa Mgonjwa | 111 |
| 23. Kupakwa Mafuta | 115 |
| 24. Sakramenti za Mwisho | 121 |
| 25. Kumwombea aliye Kufani | 123 |
| 26. Kuwaombea Waliofariki | 131 |
| 27. Kuzikwa Mkristo | 136 |
| 28. Kuzikwa Mtoto Mchanga | 149 |
| 29. Kuzikwa Mwanafunzi | 154 |
| 30. Sala za Kanuni | 157 |

AMRI KUMI

1. Usiwe na miungu mingine ila Mimi.
2. Usijifanyizie sanamu ya kuchora ukaiabudu.
3. Usilitaje bure Jina la Bwana Mungu wako.
4. Ikumbuke Siku ya Bwana, uitakase ;
siku sita fanya kazi.
5. Waheshimu baba yako na mama yako.
6. Usiue.
7. Usizini.
8. Usiibe.
9. Usimshuhudie jirani yako uwongo.
10. Usitamani vitu vya watu.

AMRI ILIYO KUU

Mpende Bwana Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. Mpende jirani yako kama nafsi yako.

AMRI ZA KANISA

1. Kuungama dhambi zetu kwa padre na kupokea Ushirika panapo Siku Kuu ya Pasaka.
2. Kuungama dhambi zetu kwa padre kila tuangukapo katika dhambi kubwa.
3. Kuhudhuria Missa kila Siku ya Bwana na Siku Kuu iliyo ya faradhi.
4. Kutoa sadaka za kulisaidia Kanisa la Mungu gharama zake.
5. Kufunga chakula panapo siku za kufunga, isipokuwa tumepewa ruhusa ya Askofu, au Padre wa mtaa, au ya Kasisi ye yote wakati tuungamapo. Tena nyama ni mwiko kila siku ya Ijumaa.
6. Marufuku ndoa isifanyike tangu Majilio hata Kuzaliwa, wala tangu J. 5 ya Majivu hata Pasaka.
7. Kabla ya kupokea Ushirika Ut. ni marufuku : tusile cho chote, wala kunywa.

AMRI YA KUFUNGA

1. Usile cho chote, wala usivute tumbako wala kuitafuna, wala usinywe cho chote (isipo-kuwa ni kunywa maji au chai au kitu kisicho kileo mara moja tu) tangu saa 6 ya usiku wa manane hata saa 9 ya alasiri.

2. Nenda kwenye mkutano wa Wakristo, ukashirikiane nao katika kuomba na kuombea. Usipozuiwa kwa neno la haki, yafaa kuihudhuria Missa Takatifu. Yakupasa kuongeza sala zako siku hizo kumi, na kutoa sadaka ili kusaidia kazi ya Kanisa.

3. Ukipenda kufunga siku zote za Kwaresima, na siku nyinginezo, ni sadaka zako kwa Mwenezezi Mungu.

SIKU ZA KUFUNGA

¶ *Siku hizi kumi* :—

1. Kila Ijumaa ya Kwaresima.
2. Ijumaa Kuu.
3. Kila Ijumaa ya Robo Mwaka.


SIKU ZENYE MISSA YA FARADHI

KWA WAKRISTO WOTE

¶ *Siku hizi zilizotajwa chini Missa ni ya faradhi kwa wote; kila Mkristo hana budi kuihudhuria Missa Takatifu siku hizi,*

1. Kila Siku ya Bwana mwaka mzima.
2. Siku Kuu ya Kuzaliwa Bwana.
3. Ufunuo wa Bwana.
4. Kupaa kwa Bwana.
5. Mwili Mtukufu wa Kristo.
(Lakini ni halali kuiadhimisha Siku Kuu hii Siku ya Bwana ifuatayo.)
6. Kustarehe kwa Mariamu B. Mb.
7. Siku Kuu ya Watakatifu wote.

¶ *Siku hizo kila Mkristo aihudhurie Missa.*



NJIA YA NEEMA
NA
TUMAINI LA UTUKUFU

KAWAIDA YA KUFANYA WANAFUNZI

¶ Watakao kufanywa Wanafunzi na wasimame penye mpaka wa Wanafunzi, kwa taratibu; Kasisi asimame kuelekeana nao, Mhudumu wake akisimama naye, ameileta misalaba ya kuwavika.

¶ Ndipo Kasisi aseme,
Mwataka nini, wanangu ?

R. Nataka kukubaliwa kuwa mwanafunzi wa Kristo.

Basi, toeni ahadi zenu, tuziseme fungu kwa fungu.

Nitafanya bidii kuzishika amri za Mwenyezi Mungu : Baba yangu na Bwana wangu.

Nitafanya bidii kumkataa Shetani siku zote : na kuacha uchawi : hirizi : kupiga bao : sadaka za wafu : na mabaya yote ya namna hii.

Nitafanya bidii kuacha ngoma mbaya : uasherati : ulevi : uwongo : matukano : na dhambi nyinginezo zote.

Nitafanya bidii kuja Kanisani kila Siku ya Bwana : na kufundishwa na Mwalimu wangu mara mbili kila juma.

Mwenyezi Mungu akusaidieni, mzishike ahadi hizi. *Amin.*

Kufanya Wanafunzi

¶ Ndipo wapige magoti, na Kasisi amrwambie kila mmoja,

N. nakuingiza katika cheo cha Wanafunzi wa Bwana Yesu Kristo, katika Kanisa lake Katholiko. (ndipo amvike msalaba) Pokea msalaba huu, dalili ya kuwa Yesu Kristo alikufa msalabani kwa ajili yako wewe, na ya kuwa hata leo anakunyoshea mikono yake akulinde na kukubariki.

¶ Wote wakiisha kupewa misalaba, Kasisi aseme,

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, uwaangalie watu hara waombao kufundishwa wapate Ubatizo Utakatifu; urearehemu; uratia imani na toba; ili wasafike katika dhambi zao, na kutolewa gizani; hatimaye wakaonekane wamestahili kubatizwa na kuondolewa dhambi zao. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Mwenyezi Mungu akuongozeni katika njia ya kweli, akufikisheni kwa furaha kwenye Ubatizo wake Utakatifu. *Amin.*



KAWAIDA YA KUPAKA MAFUTA WANAFUNZI WA UBATIZO

JINSI YA KUPOKEA WANAFUNZI WA KA
WAIDA KATIKA CHEO CHA WANAFUNZI
WA UBATIZO

¶ Wakati wa Missa kablu hajawaruhusu Wanafunzi, au wakati mwingine unaofaa, Kasisi aende akasimame kati ya Wanafunzi wa kawaida, akiikabili madhbahu; mbele yake waliochaguliwa kupakwa mafuta, wameipa kisogo madhbahu, wamkabili Kasisi.

¶ Ndipo Kasisi aseme,
Mwataka nini, wanangu ?
Rj. Nataka kubatizwa.

¶ Kisha awaonye Wakristo, ili warwaombee waliochaguliwa.

Ndugu wapenzi, kwa kuwa watu wote wamezaliwa na dhambi, wala hawawezi kumpendeza Mungu, bila wazaliwe mara ya pili kwa maji na Roho Mtakatifu; nakusihini tumwombe Mungu Baba, kwa Jina lake Bwana wetu Yesu Kristo, awajalie watu hara wazidi kuutamani Ubatizo Utakatifu, na kupewa imani na toba, hata wakastahili kubatizwa na Roho Mtakatifu, na kufanywa viungo hayi vya Kristo.

Wanafunzi wa Ubatizo

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, umewajalia *watu hawa* wajitakie Ubatizo Utakatifu na ondoleo la dhambi zao ; Tunakuomba upende kuwakubali, kama ulivyotuahidi kwa maneno ya Mwana wako mpendwa, aliyesema, Ombeni mtapata ; tafuteni, mtaona ; bisheni, mtafunguliwa. Basi utupe sisi tunaokuomba sasa : tuone sisi tunaotafuta ; utufungulie mlango sisi tubishao ; *watu hawa* wapewe imani na toba, wakazidi kutengana na dhambi, hata wakastahili kukaribishwa katika ufalme wako wa milele na kufanywa *watotowako*. Kwa Yeye, Kristo Bwana wetu. *Amin*.

¶ *Kisha Kasisi awasaili watakao Ubatizo maswali haya, nao wamjibu mmoja mmoja,*

Wamkataa Shetani na kazi zake zote ?

R_y. Namkataa Shetani na kazi zake zote.

Wazikataa anasa za dunia na fahari yake ?

R_y. Nazikataa anasa za dunia na fahari yake.

Wazikataa tamaa mbaya za mwili ?

R_y. Nazikataa tamaa mbaya za mwili.

¶ *Kisha aseme,*

Nakuamuru, Shetani, ✝ kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, uwatoke *watu hawa*, ukaende mbali nao, kwa kuwa Bwana Yesu Kristo amewaitia Ubatizo wake Utakatifu, na kufanywa viungo vya Mwili wake. Kwa hiyo, Ee Pepo mlaaniwa, uifahamu hukumu uliyo-andikiwa, wala usithubutu kuwaonea *watu hawa*, ambao kwamba Kristo amewakomboa kwa damu yake ya thamani, akarwachagua waingie kundi lake kwa Ubatizo wake huu.

Wanafunzi wa Ubatizo

¶ *Kisha Kasisi amtie kila mmoja alama ya msalaba katika paji la uso wake kwa kidole gumba kimechooywa katika mafuta ya Wanafunzi, aseme,*

Msalaba wa Kristo uwe kati yako na Shetani siku zote. Nawe, mwanangu, upigane naye kwa ushujaa mpaka mwisho. *Amin*.

¶ *Kisha aisome Injili.*

¶. Bwana akae nanyi.

R_y. Akae na roho yako.

Sehemu ya Injili takatifu kama ilivyoandikwa na Yohana Mtakatifu.

Ndipo : Palikuwa na mtu mmoja wa Mafarisayo, jina lake Nikodemo, mkuu wa Wayahudi ; huyu alikuja kwa Yesu usiku, akamwambia, Rabbi, twajua ya kuwa U Mwalimu, umetoka kwa Mungu ; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo Wewe, ila Mungu awe pamoja naye. Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezি kuuona ufalme wa Mungu. Nikodemo amwambia, Awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee ? Aweza kuingia tumboni mwa mama yake mara ya pili akazaliwa ? Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na Roho hawezি kuuingia ufalme wa Mungu. Kilichoziwa kwa mwili ni mwili ; na kilichoziwa kwa Roho ni roho. (*Sura 3.*)

¶. Na Wewe, Bwana, uturehemu.

R_y. Tumshukuru Mungu.

Wanafunzi wa Ubatizo

¶ *Kisha Kasisi aseme,*

Wanangu, tokea leo mmepewa ruhusa ya kufundishwa Sala ya Bwana na Imani ya Mitume.

Basi, tuielekee madhbahu, na kusema fungu kwa fungu,

Baba yetu, uliye mbinguni ; Jina lako takatifu litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, Hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki zetu. Utusamehe makosa yetu, Kama sisi tunavyowasamehe waliotukosa. Usitutie majaribuni, Lakini utuokoe na maovu. Amin.

Namwamini Mungu Baba Mwenyezi, Muumba mbingu na nchi.

Na Yesu Kristo, Mwana wake pekee, Bwana wetu, Aliyechukuliwa mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu, Akazaliwa na Bikira Mariamu, Akateswa zamani za Pontio Pilato, Akasulibiwa, Akafa, Akazikwa, Akashuka mahali pa wafu ; Siku ya tatu akafufuka, Akapaa mbinguni, Ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi ; Kutoka huko atakuja kuwahukumu watu wahayi na wafu.

Namwamini Roho Mtakatifu ; Kanisa Takatifu, Katholiko ; Ushirika wa Watakatifu ; Ondoleo la dhambi ; Kiyama ya mwili, Na uzima wa milele. Amin.

¶ *Kisha wamgeukie Kasisi tena, naye aseme,*
Tuombe.

Mwenyezi Mungu uishiye milele, Baba wa mbinguni, tunakushukuru kwa unyenyekevu kwa kuwa umetuita tuijue neema yako, na

Ubatizo

kukuamini : *Uwajalie watu harwa wazidi kukuamini na kukutii, ili wastahili kuzaliwa mara ya pili, na kufanywa warithi wa wokofu wa milele. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.*

Bwana apende kuwakaribisha katika ujamaa wa Watakatifu wake, na kuwaweka salama pamoa nao, na kuwapa uzima wa milele. Amin.

¶ *Ndipo awarihusu Wanafunzi kama kawaida.*

UBATIZO UTAKATIFU

¶ *Sala hii isitumike kwa mtu ye yote asiyepakwa mafuta ya Wanafunzi kama ilivyoamriwa.*

¶ *Wakiisha kukusanyika panapo Maji ya Ubatizo, wakimwelekea Kasisi na kuipa kisogo madhbahu, Kasisi aseme,*

NDUGU wapenzi, kwa kuwa watu wote wamezaliwa na dhambi, wala hawawezi kumpendeza Mungu, bila wazaliwe mara ya pili kwa maji na Roho Mtakatifu ; nakusihini tumwombe Mungu Baba, kwa Jina lake Bwana wetu Yesu Kristo, awajalie watu harwa jambo hili wasiloweza kulipata kwa asili ya ubinadamu ; ni kubatizwa kwa maji na Roho Mtakatifu, na kukaribishwa katika Kanisa Takatifu la Mungu, na kufanywa viungo hayi vya Kristo.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, uishiye milele, kwa kubatizwa Mwana wako impendwa, Yesu Kristo, katika mto Yordani, ulitakasa maji yaoshe dhambi kwa jinsi ya siri : Tunakusihi uwatazame watu harwa kwa rehema zako ; uwaoeshe, uwatakase kwa Roho Mtakatifu ; ili wawe thabiti katika imani, wafurahi katika tumaini, wakae imara katika upendo, hata wafike kwenye nchi ya uzima wa milele, na kumiliki huko pamoja nawe. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ *Kisha Kasisi awaambie watu watakaobati-zwa maneno haya,*

Wapenzi, mmekuja hapa kujitakia Ubatizo Utakatifu. Basi, hamna budi kukiri ninyi, mbele ya hawa Mashahidi wenu, na hawa wote waliopo, kwamba mtazidi kumkataa Shetani na kazi zake zote, mtaliamini daima Neno takatifu la Mungu, na kuzishika kwa utii amri zake.

Nakulizeni,

Utazidi kumkataa Shetani na kazi zake zote, na anasa za dunia na fahari yake, na tamaa mbaya za mwili, usizifuate wala kuongozwa nazo ?

¶ *Wajibu mmoja mmoja,*
R₇. Nitazidi kuzikataa zote.

¶ *Kisha aseme,*
Wamwamini nani ?

¶ *Waigeukie madhabahu, wajibu wote pamoja.*

R₇. Namwamini Mungu Baba Mwenyezi Muumba mbingu na nchi.

Na Yesu Kristo, Mwana wake pekee, Bwana

wetu, Aliyechukuliwa mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu, Akazaliwa na Bikira Mariamu, Akateswa zamani za Pontio Pilato, Akasulibiwa, Akafa, Akazikwa, Akashuka mahali pa wafu ; Siku ya tatu akafufuka, Akapaa mbinguni, Ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi ; Kutoka huko atakuja kuwahukumu watu wahayi na wafu.

Namwamini Roho Mtakatifu ; Kanisa Taktifu, Katholiko ; Ushirika wa Watakatifu ; Ondoleo la dhambi ; Kiyama ya mwili, Na uzima wa milele. *Amin.*

¶ *Wamgeukie Kasisi,*

Wataka kubatizwa uishike imani hii ?

¶ *Wajibu mmoja mmoja,*

R₇. Ndiyo nitakayo.

Utafanya bidii kuyatimiza mapenzi ya Mungu na kuzishika amri zake ?

R₇. Nitafanya bidii kuzishika.

¶ *Kisha Kasisi aseme,*

Tuombe.

Kama vile Mwokozi wetu Kristo alivyotuagiza, akatufundisha, tunathubutu kusema,

Baba yetu.

KUYATAKASA MAJI

¶ *Ndipo Kasisi aseme,*

Mungu wa rehema, ujalie, Adamu wa kwanza aliomo katika watu harwa azikwe, mtu mpya akaonekane. *Amin.*

Uwajalie tamaa zote mbaya zife ndani yao na mambo ya roho yaishi yakakue ndani yao. *Amin.*

Ubatizo

Uwajalie wawe na uwezo na nguvu za kushinda kwa shangwe Shetani, dunia, na mwili. Amin.

Umjalie kila awekwaye wakfu kwa kazi na huduma yetu avikwe wema wako wa mbinguni, apate thawabu ya milele, kwa rehema zako, Ee Bwana Mungu Mtukufu ; Uishiye na kutawala vyote milele na milele. Amin.

¶ Ndipo Kasisi aubariki uwumba, kisha aseme au aimbe,

Y. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Y. Inueni mioyo.

R. Twaiinua kwa Bwana.

Y. Na tumshukuru Bwana Mungu wetu.

R. Ina haki, tena ni wajibu.

Ndio wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.

Kwa kuwa Mwana wako mpendwa, Yesu Kristo, alitoa katika ubavu wake mtakatifu maji na damu kwa masamaha ya dhambi zetu ; akawaagiza wanafunzi wake, waende wakafundishe Mataifa yote, na kuwabatiza kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Tunakusihii uziangalie sala za watu wako waliopo hapa ; uyatakase ✕ maji haya yaoshe dhambi kwa jinsi ya siri ; uwajalie watu hara watakaobatizwa nayo wapokee neema yako kwa wingi, wakadumu katika hesabu ya watoto wako wateule.

Kwa Yeye, Bwana wetu Yesu Kristo Mwana wako ; Aishiye na kumiliki pamoja nawe, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima milele na milele. Amin.

Ubatizo

¶ Ndipo Kasisi ayafukizie maji mara tatu, kisha aivae stola nyeupe na kappa nyeupe.

¶ Kisha, ikiwa maji ni mengi, Kasisi amtwaе atakayebatizwa kwa mkono wake wa kulia, akambatize, amtie chini ya maji mara tatu ; mara moja amtajapo BABA, mara moja amtajapo MWANA, mara moja amtajapo ROHO MTAKATIFU.

¶ Ikiwa maji ni haba, Kasisi ammiminie atakayebatizwa maji kichwani mara tatu, amepiga magoti ; mara moja amtajapo BABA, mara moja amtajapo MWANA, mara moja amtajapo ROHO MTAKATIFU.

N. Nakubatiza kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Amin.

¶ Kisha Kasisi amtie alama ya msalaba utosini, kwa kidole gumba kimechovywa katika mafuta ya Wokofu, aseme,

Nakutia alama ✕ ya msalaba kwa mafuta ya Wokofu, iwe ishara ya kuwa umekwisha kuingia katika kundi la Kristo. Amin.

¶ Ampe vazi safi.

N. pokea vazi hili, mfano wa usafi wa roho yako, ukajiweke safi hata panapo kitu cha hukumu cha Bwana wetu Yesu Kristo, ili uupate uzima wa milele. Amin.

¶ Ampe mshumaa.

N. pokea mshumaa huu, nuru yake ni mfano wa neema ya ubatizo wako ; uzishike amri zote za Mungu, ili atakapokuja Bwana ukubaliwe naye ukakaribishwe pamoja na Watakatifu wake katika ufalme wake wa milele. Amin.

Ubatizo

¶ Awaonye waliobatizwa hivi,

Wanangu, nilirwatia alama ya msalaba ili msione haya kuikiri imani yake Kristo aliyesuli-biwa, bali, mkiwa chini ya bendera yake, mpigane kwa ushujaa na dhambi, dunia, na Shetani ; mkadumu kuwa askari na watumwa amini wa Kristo hata mwisho wa maisha zenu. *Amin.*

¶ Kisha Kasisi aseme,

Ndugu wapenzi, kwa kuwa watu harwa wamezaliwa mara ya pili, na kuingizwa katika Mwili wake Kristo, ndio Kanisa lake, na tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mambo haya mema aliywapa ; na kwa moyo mmoja tumwombe, watu harwa waishi tangu sasa kwa jinsi walivyoanza leo.

Tuombe.

Tunakushukuru kwa moyo, Ee Baba wa rehema, kwa kuwa umependa watu harwa wazaliwe mara ya pili na Roho yako Mtakatifu, ukarwachagua wawe watoto wako, na kuwaingiza katika Kanisa lako Takatifu. Nasi tunakusihii kwa unyenyekevu, uwajalie wawe wafu kwa mambo ya dhambi, wawe hayi kwa mambo ya haki ; na kama walivyokwisha kushiriki kufa kwa Mwana wako, uwajalie kushiriki na kufufuka kwake ; hata kwa mwisho, waaurithi ufalme wako wa milele, pamoja na wateule wa Kanisa lako Takatifu. Kwa Yeye, Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Msaada wa Mungu ukae nasi daima. *Amin.*

UBATIZO WA WATOTO WACHANGA

¶ Wakiisha kukusanyika panapo Maji ya Ubatizo, wakimwelekea Kasisi na kuipa kisogo madhbahu, Kasisi aseme,

Ndugu wapenzi, kwa kuwa watu wote wamezaliwa na dhambi, wala hawawezi kumpendeza Mungu, bila wazaliwe mara ya pili kwa maji na Roho Mtakatifu ; nakusihini tumwombe Mungu Baba, kwa Jina lake Bwana wetu Yesu Kristo, awajalie watoto harwa jambo hili wasilowezwa kulipata kwa asili ya ubinadamu ; ni kubatizwa kwa maji na Roho Mtakatifu, na kukaribishwa katika Kanisa Takatifu la Mungu, na kufanywa viungo hayi vya Kristo.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, uishiye milele, kwa kubatizwa Mwana wako mpendwa, Yesu Kristo, katika mto Yordani, ulitakasa maji yaoshe dhambi kwa jinsi ya siri : Tunakusihii, uwatazame watoto harwa kwa rehema zako ; uwaoshe, uwatakase kwa Roho Mtakatifu ; ili wawe thabiti katika imani, wafurahi katika tumaini, wakae imara katika upendo, hata wafike kwenye nchi ya uzima wa milele, na kumiliki huko pamoja nawe. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ Kisha Kasisi awaambie watu waliorwaleta watakaobatizwa maneno haya,

Ubatizo wa Watoto

Wapenzi, mmekuja hapa kuwatachia watoto harwa Ubatizo Utakatifu. Basi hamna budi, kwa ajili yao, kuahidi mbele ya hawa wote waliopo, kwamba watamkataa Shetani na kazi zake zote, wataliamini daima Neno takatifu la Mungu, na kuzishika kwa utii amri zake.

¶ Kisha Kasisi awasaili Wadhamini maswali haya,

Wamkataa Shetani na kazi zake zote ?

R/. Namkataa Shetani na kazi zake zote.

Wazikataa anasa za dunia na fahari yake ?

R/. Nazikataa anasa za dunia na fahari yake.

Wazikataa tamaa mbaya za mwili ?

R/. Nazikataa tamaa mbaya za mwili.

¶ Kisha aseme,

Nakuamuru, Shetani, ✕ kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, uwatoke watoto harwa, ukaende mbali nao, kwa kuwa Bwana Yesu Kristo amewaitia Ubatizo wake Utakatifu na kufanywa viungo vya Mwili wake. Kwa hiyo, Ee Pepo mlaaniwa, uifahamu hukumu uliyoandikiwa, wala usithubutu kurwaonea watoto harwa, ambao kwamba Kristo amewakomboa kwa damu yake ya thamani, akawachagua waingie kundi lake kwa Ubatizo wake huu.

¶ Kisha Kasisi amtie kila mmoja alama ya msalaba katika paji la uso wake kwa kidole gumba kimechovywa katika mafuta ya Wanafunzi, aseme,

Msalaba wa Kristo uwe kati yako na Shetani siku zote. Nawe, mwanangu, upigane naye kwa ushujaa mpaka mwisho. Amin.

¶ Kisha aisome Injili.

¶ V. Bwana akae nanyi.

R/. Akae na roho yako.

Ubatizo wa Watoto

Sehemu ya Injili takatifu kama ilivyoandikwa na Marko Mtakatifu.

Ndipo : Wakamletea Yesu watoto wachanga ili awaguse ; wanafunzi wake wakawakemea wao waliowaleta. Lakini Yesu alipoona aka-chukizwa sana, akawaambia, Waacheni watoto wachanga waje kwangu, msiwazue ; kwa maana watoto kama hawo ufalme wa mbinguni ni wao. Amin, nawaambieni, Ye yote asiyeukubali ufalme wa Mungu kama mtoto mchanga hatauingia kabisa. Akawakumbatia, akaweka mikono yake juu yao, akabariki. (Sura 10)

¶ V. Na Wewe Bwana uturehemu.

R/. Tumshukuru Mungu.

¶ Kisha aseme,

Wamwamini nani ?

¶ Wadhamini waigeukie madhbahu, wajibu wote pamoja.

R/. Namwamini Mungu.

¶ Wamgeukie Kasisi.

Wataka kubatizwa uishike imani hii ?

R/. Ndiyo nitakayo.

Utafanya bidii kuyatimiza mapenzi ya Mungu na kuzishika amri zake ?

R/. Nitafanya bidii kuzishika.

¶ Kisha Kasisi aseme,

Tuombe.

Kama vile Mwokozi wetu Kristo alivyotuagiza, akatufundisha, tunathubutu kusema,

Baba yetu.

KUYATAKASA MAJI.

¶ Ndipo Kasisi aseme,

Mungu wa rehema, ujalie, Adamu wa kwanza

Ubatizo wa Watoto

aliomo katika watoto *hawa* azikwe, mtu mpya akaonekane. *Amin.*

Uwajalie tamaa zote mbaya zife ndani yao na mambo ya roho yaishi yakakue ndani yao. *Amin.*

Uwajalie *wawe* na uwezo na nguvu za kushinda kwa shangwe Shetani, dunia, na mwili. *Amin.*

Umjalie kila awekwaye wakfu kwa kazi na huduma yetu avikwe wema wako wa mbinguni, apate thawabu ya milele, kwa rehema zako, Ee Bwana Mungu Mtukufu ; Uishiye na kutawala vyote milele na milele. *Amin.*

¶ *Ndipo Kasisi aubariki uvumba, kisha aseme au aimbe,*

℣. Bwana akae nanyi.

R;. Akae na roho yako.

℣. Inueni mioyo.

R;. Twaiinua kwa Bwana.

℣. Na tumshukuru Bwana Mungu wetu.

R;. Ina haki, tena ni wajibu.

Ndio wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.

Kwa kuwa Mwana wako mpPENDWA, Yesu Kristo, alitoa katika ubavu wake mtakatifu maji na damu kwa masamaha ya dhambi zetu ; akawaagiza wanafunzi wake, waende wakafundishe Mataifa yote, na kuwabatiza kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Tunakusihi uziangalie sala za watu wako waliopo hapa ; uyatakase ✕ maji haya yaoshe dhambi kwa jinsi ya siri ; uwajalie watu *hawa* watakatizwa nayo wapokee neema yako kwa

Ubatizo wa Watoto

wingi, wakadumu katika hesabu ya watoto wako wateule.

Kwa Yeye, Bwana wetu Yesu Kristo Mwana wako ; Aishiye na kumiliki pamoja nawe, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima milele na milele. *Amin.*

¶ *Ndipo Kasisi ayafukizie maji mara tatu, kisha aivae stola nyeupe na kappa nyeupe.*

¶ *Kisha mdhamini mmoja amlete mtoto, amshike mikononi mwake, kichwa cha mtoto kimelazwa katika mkono wake wa kushoto. Kasisi ambatize mtoto, ammiminie maji kichwani mara tatu ; mara moja amtajapo BABA, mara moja amtajapo MWANA, mara moja amtajapo ROHO MTAKATIFU.*

N. Nakubatiza kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

¶ *Kisha Kasisi amtie alama ya msalaba utosini, kwa kidole gumba kimechovyywa katika mafuta ya Wokofu, aseme,*

Nakutia alama ✕ ya msalaba kwa mafuta ya Wokofu, iwe ishara ya kuwa umekwisha kuingia katika kundi la Kristo. *Amin.*

¶ *Ampe vazi safi.*

N. pokea vazi hili, mfano wa usafi wa roho yako, ukajiweke safi hata panapo kitu cha hukumu cha Bwana wetu Yesu Kristo, ili uupate uzima wa milele. *Amin.*

¶ *Ampe mshumaa.*

N. pokea mshumaa huu, nuru yake ni mfano wa neema ya ubatizo wako ; uzishike amri zote za Mungu, ili atakapokuja Bwana ukubaliwe naye ukakaribishwe pamoja na Watakatifu wake katika ufalme wake wa milele. *Amin.*

Ubatizo wa Watoto

¶ Awaonye waliobatizwa hivi,

Wanangu, niliwatia alama ya msalaba, ili msione haya kuikiri imani yake Kristo aliyesuli-biwa, bali, mkiwa chini ya bendera yake, mpigane kwa ushujaa na dhambi, dunia, na Shetani ; mkadumu kuwa askari na watumwa amini wa Kristo hata mwisho wa maisha zenu. Amin.

¶ Kisha Kasisi aseme,

Ndugu wapenzi, kwa kuwa watoto hara wamezaliwa mara ya pili, na kuingizwa katika Mwili wake Kristo, ndio Kanisa lake, na tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mambo haya mema aliyowapa ; na kwa moyo immoja tumwombe, watoto hara waishi tangu sasa kwa jinsi walivyoanza leo.

Tuombe.

Tunakushukuru kwa moyo, Ee Baba wa rehemu, kwa kuwa umependa watoto hara wazaliwe mara ya pili na Roho yako Mtakatifu, ukawachagua wawe watoto wako, na kurwaingiza katika Kanisa lako Takatifu. Nasi tunakusihi kwa unyenyekevu, uwajalie wawe wafu kwa mambo ya dhambi, wawe hayi kwa mambo ya haki ; na kama walivyokwisha kushiriki kufa kwa Mwana wako, uwajalie kushiriki na kufufuka kwake ; hata kwa mwisho, waurithi ufalme wako wa milele, pamoja na wateule wa Kanisa lako Takatifu. Kwa Yeye, Kristo Bwana wetu. Amin.

Msaada wa Mungu ukae nasi daima. Amin.

¶ Mtoto mchanga, amebatizwa hajapata akili, hana budi kufundishwa yote wafundishwayo WANAFUNZI, wa kawaida na wa Ubatizo, kabla hajaletwa kwa Askofu ili aperwe Kipa Imara.

UBATIZO WA MGONJWA KITANDANI

¶ Ikiwapo nafasi, kwanza watu wote waliopo wapige magoti, wakaseme,
Baba yetu.

¶ Kisha mgonjwa aongozwe aseme sala za imani na toba, au watu waziseme kwa ajili yake,

Mungu wangu nakuamini ; Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Uniokoe sasa kwa Ubatizo ; Unilete kwako mbinguni.

Mungu wangu nasikitika sana ; kwa kuwa nimetenda dhambi. Nataka kuziacha dhambi zangu zote ; Naomba uziondoe zote ; Kwa Ubatizo huu.

¶ Ikiwa ni mtoto mdogo anayebatizwa sala hizo zisisemwe.

¶ Ndipo Padre, au mtu mrwingine atakayembatiza yule mgonjwa, ammiminie maji kichwani hata paji la uso wake, mara tatu ; mara moja amtajapo BABA, mara moja amtajapo MWANA, mara moja amtajapo ROHO MTAKATIFU.

¶ Asikose kusema maneno haya,

N. Nakubatiza kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Amin.

¶ Ndio mwisho.

¶ Mwenye haki ya kumbatiza mgonjwa saa ya kufa ni Mkristo ye yote, asipokuwapo Padre, wala Shemasi, wala Msomaji, wala Mwalimu.

Ubatizo wa Mgonjwa

Mwanamke ana haki ya kumbatiza asipokuwapo mwanamume. Mtu wa mwisho wa kumbatiza ni yeye aliyemzaa mgonjwa, bali aweza asipokuwapo mwingine. Walakini wagonjwa wasibati-zwe ila saa ya kufa tu.

¶ Mwenye haki ya kubatizwa kitandani ni mtu adhaniwaye hatapona, anakufa.

Lakini marufuku wasibatizwe watu harwa.

(1) Asiyeanza kumjua Mungu wala Bwana Yesu Kristo.

(2) Asiyetubia dhambi zake, wala hajakiri kuziacha akijaliwa kupona, wala kuanza kute-ngeneza hali yake.

(3) Asiyetao kauli wala dalili ya kutaka Ubatizo alipokuwa mzima. Lakini iwapo wakati wa ugonjwa amejaliwa kuongoka kwa Kristo, ndipo aweza kubatizwa.

¶ Mtoto mchanga ye yote na abatizwe saa ya kufa.

¶ Mgonjwa akibatizwa kitandani, yule aliye-mbatiza ana lazima kumwarifu Padre wa mtaa bila kukawia.

¶ Mgonjwa akijaliwa kupona asikose kuletwa Kanisani, Kasisi apate kutimiza kawaida za UBATIZO zilizoachrwa pale alipobatizwa kitandani. Kisha, hana budi kufundishwa, na kuyamaliza mafundisho yake yote, kabla hajaletwa kwa Askofu ili apewe Kipa Imara.

KUTIMIZA KAWAIDA ZA UBATIZO

JINSI YA KUMKARIBISHA KATIKA KANISA TAKATIFU KATHOLIKO MTU ALIYEBATIZWA UGONJWANI, AU MTU YE YOTE ASIYEBATIZWA KWA KAWAIDA ZA KANISA KATHOLIKO.

¶ Aliyebatizwa ugonjwani akapona, na alethee Kanisani bila kukawia ili akaribishwe katika Kanisa. Akiwa ni mtu mzima, na awepo Mdhamsini wake, au akiwa ni mtoto mchanga na awepo Wadhamini warili, kama kawaida.

¶ Wakiisha kukusanyika panapo mahali pa Ubatizo wakimwelekea Kasisi na kuipa kisogo madhbahu, Kasisi aseme,

Ndugu wapenzi, nawajulisheni ya kuwa mtu (au mtoto) huyu amebatizwa ugonjwani kwa kawaida ya Kanisa iliyo kanuni. Basi msikilizeni huyu aliyembatiza akinijibu maswali yangu.

¶ Ndipo amsaili yule aliyembatiza.

Alibatizwa lini ?

Alibatizwa na nani ?

Alibatizwa mbele ya nani ?

Alibatizwa kwa kitu gani ?

Alibatizwa kwa maneno gani ?

Basi, ndugu, mmesikia ya kuwa mtu (au mtoto) huyu amebatizwa kama ilivyo kawaida ya Kanisa Katholiko.

¶ Kisha Kasisi amsaili yule aliyebatizwa ; na akiwa ni mtu mzima ajibu mwenyerewe, au Mdhamsini wake amsaidie kujibu, au Kasisi amsemeshe ; akiwa ni mtoto mchanga Wadhamini na wajibu kwa ajili yake.

Kutimiza Kawaida

¶ Aidha, ikiwa Kasisi amkaribisha mtu asiyebatizwa kwa kawaida za Kanisa Katholiko na aanze hapa.

Wamkataa Shetani na kazi zake zote ?

R/. Namkataa Shetani na kazi zake zote.

Wazikataa anasa za dunia na fahari yake ?

R/. Nazikataa anasa za dunia na fahari yake.

Wazikataa tamaa mbaya za mwili ?

R/. Nazikataa tamaa mbaya za mwili.

¶ Kisha aseme,

Nakuamuru, Shetani, ✝ kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, ukae mbali na mtu (au mtoto) huyu, kwa kuwa Bwana Yesu Kristo amemwitia Ubatizo wake Utakatifu na kufanywa kiungo cha Mwili wake. Kwa hiyo, Ee Pepo mlaaniwa, uifahamu hukumu uliyoandikiwa, wala usithubutu kumwonea mtu (au mtoto) huyu, ambaye kwamba Kristo amemkomboa kwa damu yake ya thamani, akamchagua aingie kundi lake kwa Ubatizo wake huu.

¶ Kisha Kasisi amtie alama ya msalaba katika paji la uso wake, kwa kidole gumba kimechovywa katika mafuta ya Wanafunzi, aseme,

Msalaba wa Kristo uwe kati yako na Shetani siku zote. Nawe, mwanangu, upigane naye kwa ushujaa mpaka mwisho. Amin.

¶ Kisha aseme,

Wamwamini nani ?

¶ Wakristo wote waigeukie madhabahu, wajibu pamoja naye,

R/. Namwamini Mungu.

¶ Wamgeukie Kasisi.

Imani hii utaishika ?

R/. Nitaishika.

Kutimiza Kawaida

Utafanya bidii kuyatimiza mapenzi ya Mungu na kuzishika amri zake ?

R/. Nitafanya bidii kuzishika.

¶ Kisha Kasisi aseme,

Tuombe.

Kama vile Mwokozi wetu Kristo alivyoituagiza, akatufundisha, tunathubutu kusema,

Baba yetu.

¶ Ndipo Kasisi aivae stola nyeupe na kappa nyeupe.

¶ Kisha Kasisi amtie alama ya msalaba utosini, kwa kidole gumba kimechovywa katika mafuta ya Wokofu, aseme,

Nakutia alama ✝ ya msalaba kwa mafuta ya Wokofu, iwe ishara ya kuwa umekwisha kuingia katika kundi la Kristo. Amin.

¶ Ampe vazi safi.

N. pokea vazi hili, mfano wa usafi wa roho yako, ukajiweke safi hata panapo kiti cha hukumu cha Bwana wetu Yesu Kristo, ili uupate uzima wa milele. Amin.

¶ Ampe mshumaa.

N. pokea mshumaa huu, nuru yake ni mfano wa neema ya ubatizo wako ; uzishike amri zote za Mungu, ili atakapokuja Bwana ukubaliwe naye, ukakaribishwe pamoja na Watakatifu wake katika ufalme wake wa milele. Amin.

¶ Amwonye hivi,

Mwanangu, nilikutia alama ya msalaba ili usione haya kuikiri imani yake Kristo aliyesuli-biwa, bali, ukiwa chini ya bendera yake, upigane kwa ushujaa na dhambi, dunia, na Shetani ; ukadumu kuwa askari na mtumwa amini wa Kristo hata mwisho wa maisha yako. Amin.

Kutimiza Kawaida

¶ *Kisha Kasisi aseme,*

Ndugu wapenzi, kwa kuwa mtu (*au mtoto*) huyu amezaliwa mara ya pili, na kuingizwa katika Mwili wake Kristo, ndio Kanisa lake, na tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mambo haya mema aliyompa ; na kwa moyo mmoja tumwombe, mtu (*au mtoto*) huyu aishi tangu sasa kwa jinsi alivyoanza.

Tuombe.

Tunakushukuru kwa moyo, Ee Baba wa rehema, kwa kuwa umependa mtu (*au mtoto*) huyu azaliwe mara ya pili na Roho yako Mtakatifu, ukamchagua awe mtoto wako, na kumwingiza katika Kanisa lako Takatifu. Nasi tunaku-sihi kwa unyenyekevu, umjalie awe mfu kwa mambo ya dhambi awe hayi kwa mambo ya haki ; na kama alivyokwisha kushiriki kufa kwa Mwana wako, umjalie kushiriki na kufufuka kwake ; hata kwa mwisho, aurithi ufalme wako wa milele, pamoja na wateule wa Kanisa lako Takatifu. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Msaada wa Mungu ukae nasi daima. *Amin.*

¶ *Aliyebatizwa kitandani na kukaribishwa hivi asifundishwe Kipa Imara wala Ushirika Utakatifu mpaka kwanza amalize mafundisho ya nyuma aliyokosa, na kufundishwa habari za Toba.*

¶ *Iwapo Kasisi ana shaka lenye maana ya kwamba mtu hakubatizwa ilivyo kanuni, asiweze kupata hakika yake, na ambatize kama kawaida ; bali wakati ambatizapo aseme,*

N. Kama hujabatizwa, nakubatiza kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*



KAWAIDA YA KUBARIKI MAJI MATAKATIFU

¶ *Chombo cha maji, na chumvi kidogo katika kisahani, viwekwe madhbahuni upande wa Waraka (au mahali Kasisi avaliapo Missa) : na Kasisi asimame pale, amevaa kotta na stola ya rangi ya urujuani, aseme,*

V. Msaada wetu u katika Jina la Bwana.

R. Aliyezifanya mbingu na nchi.

Enyi pepo wabaya, nakuagizeni mwitoke chumvi hii iliyo kiumbe cha Mungu. Nakua-gizeni kwa Jina la ☩ Mungu, Mungu ☩ aliye hayi, Mungu ☩ aliye Mtakatifu halisi. Chumvi hii iwafalie waaminio kwa wokofu wao ; ili waichukuao waone afya ya roho na mwili ; ubaya wa Shetani usiwepo panapo chumvi hii, bali kila kitwana chake akimbie ; kwa amri yake Yeye ajaye kuwahukumu wahayi na wafu, na ulmwengu wote kwa moto. *Amin.*

Tuombe.

Mwenyezi Mungu wa milele, tunakuomba kwa unyenyekevu, kwa rehema zako zisizo kiasi, upende kuibariki ☩ chumvi hii na ☩ kuitakasa, ambayo kwamba umeiumba kwa matumizi yetu sisi wanadamu : Iwalettee waichukuao afya ya roho na mwili ; kila kitakachoguswa nayo kitengwe na uchafu, na kulindwa na maovu ya kishetani. Kwa.

Kubariki Maji

Enyi pepo wabaya, nakuagizeni myatoke maji haya yaliyo kiumbe cha Mungu. Nakua-gizeni kwa Jina la ✕ Mungu Baba Mwenyezi, na kwa Jina la ✕ Bwana wetu Yesu Kristo Mwana wake, na kwa uweza wa ✕ Roho Mtakatifu. Maji haya yafukuzie mbali nguvu zote za adui wetu ; yakamwondoshe na kumkimbiza pamoja na wafiasi wake walioasi ; kwa uweza wake Bwana wetu Yesu Kristo ajaye kuwahukumu wahayi na wafu, na ulimwengu wote kwa moto. *Amin.*

Tuombe.

Ee Mungu, kwa ajili ya wokofu wa wanadamu umependa Sakramenti ya Ubatizo ifanyike kwa maji : Ukubali maombi yetu, ✕ ukibariki hiki kiumbe chako ; ili maji haya yatiliwe uweza wako wa Uungu ; yatufalie kufukuza pepo na kuponya maradhi ; hata kitu cho chote cha kwetu kitakachonyunyiziwa nayo kitengwe na uchafu na kulindwa na maovu. Panapo maji haya ndipo yakimbie magonjwa yote na maradhi ; wala zisiwepo hila zo zote za adui wetu ; bali maji haya yafukuzie mbali nasi kila kiwezacho kutudhuru, kisizidi kutukalia kwetu ; hata tuplicate kukaa salama na afya zetu kwa kuliitia Jina lako Takatifu. Kwa.

¶ Ndipo Kasisi atie chumvi katika maji mara tatu, kwa jinsi ya kupiga alama ya msalaba kwayo, aseme,

Chumvi hii ichanganywe na maji haya kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

Kushukuru

V. Bwana akae nanyi.
R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Ee Mungu, asili ya uweza usiozuilika, Mfalme wa ufalme usiovunjika, Mshindaji Mtukufu mwenye kuwakanyaga wakuasio, imbele za uweza wako ukali wa adui hupoa wala hila zao hazifai neno : Tunakuomba kwa unyenyekevu na kutetemeka, ukubali kukitazama kiumbe hiki, maji kwa chumvi, na kupendezwa nacho ; ukiangaze kwa utukufu wako ; ukitakase kwa upendo wako ; ili po pote patakaponyunyiziwa nacho, kwa kuliitia Jina lako Takatifu, pasafike katika nguvu za Shetani na pepo zake, pakao-ndolewe hofu yote ya hila zake. Ujalie kila panapo kiumbe hiki safi ndipo awepo Roho Mtakatifu, akitulinda sisi tumwombao. Kwa. Aishiye . . . umoja wake Yeye huyu.

KAWAIDA YA KUSHUKURU KWA MTU YE YOTE

¶ Mtu atakaye kutoa shukrani baada ya kupona katika ugonjwa (au shida nyineye yote), afike Kanisani, apige magoti katika mahali pa kawaida. Ndipo Kasisi amkabili, aseme,

Huyu ndugu yetu amekuja kumtolea Mwenyezi Mungu shukrani kwa kuwa amemponya katika

Kushukuru *

ugonjwa wake (*au shida yake*) ; basi na tunshukuru Mungu pamoja naye.

Ant. Mtukuzeni Bwana.

Zab. 34.

1. Nitamhimidi Bwana kila wakati :
Sifa zake kinywani mwangu daima.
2. Katika Bwana roho yangu itajisifu :
Wanyenyekevu wasikie wakafurahi.
3. Mtukuzeni Bwana pamoja nami :
Na tuliadhimishe Jina lake pamoja.
4. Nalimtafuta Bwana akanijibu :
Akaniponya na hofu zangu zote.
5. Wakamwelekea macho wakatiwa nuru :
Wala nyuso zao hazitaona haya.
6. Masikini huyu aliita, Bwana akasikia :
Akamwokoa na taabu zake zote.
7. Malaika wa Bwana huwalinda wamchao :
Na kuwaokoa.
8. Onjeni mwone ya kuwa Bwana yu mwema :
Yu heri mtu yule anayemtumaini.
Utukufu.

Ant. Mtukuzeni Bwana pamoja nami : na tuliadhimishe Jina lake pamoja.

¶ *Kisha Kasisi aseme,*

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Baba yetu.

Kushukuru

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, tunakushukuru kwa unyenyekevu, kwa kuwa umekubali kumponya huyu mtumishi wako katika ugonjwa wake (*au shida yake*) : Tunakusihii, Ee Baba wa rehema, umjalie akushukuru kwa moyo ; ayatimize mapenzi yako, na kufuata utakatifu na haki, hata aufikie ufalme wa upendo wako. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Baraka ya Mwenyezi Mungu, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, ikae nawe daima. *Amin.*

¶ *Ndipo Kasisi amnyunyizie magi matakatifu.*

¶ *Mtu atoaye shukrani atie sadaka yake katika mfuko uliowekwa tayari.*

¶ *Aidha, yafaa aupokee Ushirika Utakatifu siku ile ile.*

KAWAIDA YA KUSHUKURU KWA MWANAMKE

BAADA YA KUZAA MTOTO

¶ *Mwanamke aliyezaa mtoto wajibu wake ni kutoa shukrani na kuomba baraka kabla mtoto wake hajabatizwa. Basi na afike Kanisani, apige magoti katika mahali pa kawaida. Ndipo Kasisi amkabili, aseme,*

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amependa kwa wema wake kukujalia uzae salama, na kuku-hifadhi katika hatari nyingi za wakati wa kuzaa ; basi na umshukuru Mungu kwa moyo, useme,

Kushukuru

Ant. Msaada wangu.

Zab. 121.

1. Nitainua macho yangu niitazame milima :
Msaada wangu utatoka wapi ?
 2. Msaada wangu u kwa Bwana :
Aliyezifanya mbingu na nchi.
 3. Asiache mguu wako usogezwe :
Asisinzie akulindaye.
 4. Hatasinzia wala hatalala usingizi :
Yeye aliye mlinzi wa Israeli.
 5. Bwana ndiyé mlinzi wako :
Bwana ni uvuli mkono wako wa kuume.
 6. Jua halitakupiga mchana :
Wala mwezi wakati wa usiku.
 7. Bwana atakulinda na mabaya yote :
Atakulinda roho yako.
 8. Bwana atakulinda utokapo na uingiapo :
Tangu sasa na hata milele.
- Utukufu.

Ant. Msaada wangu u kwa Bwana : aliyezifanya mbingu na nchi.

¶ *Kisha Kasisi aseme,*

Bwana, uturehemu.
Bwana, uturehemu.
Kristo, uturehemu.
Kristo, uturehemu.
Bwana, uturehemu.
Bwana, uturehemu.

Baba yetu.

¶. Ee Bwana, umwokoe mwanamke huyu mtumishi wako.

R/. Anayekutumaini Wewe.

Kushukuru

¶. Ee Bwana, uwe kwake ngome yenye nguvu.

R/. Adui asimpate.

¶. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R/. Kilio changu kikufikie.

¶. Bwana akae nanyi.

R/. Akae na roho yako.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, tunakushukuru kwa unyenyekevu, kwa kuwa umekubali kumwokoa mwanamke huyu mtumishi wako katika uchungu mwingi na hatari za kuzaa : Tunakusihi, Ee Baba wa rehema, umjalie kwa msaada wako aishi kwa imani ; na kuenenda upendavyo Wewe katika maisha haya, hata aushiriki utukufu wa milele katika maisha yatakayokuja. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Baba yetu wa mbinguni akujalie amani ya roho na raha ya mwili. *Amin.*

Bwana Yesu Kristo akulinde na maovu yote, akufikishe salama kwenye utukufu wake. *Amin.*

Roho Mtakatifu akutakase hata ukautimize wito ulioitiwa naye. *Amin.*

Mariamu Mtakatifu, Mama wa Mungu, akuombee : Watakatifu wote wa Mungu wakuo-mbee : Malaika zote watakatifu wakulinde. *Amin.*

Baraka ya Mwenyezi Mungu, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, ikae nawe daima. *Amin.*

¶ *Ndipo Kasisi amnyunyizie maji matakatifu.*

¶ *Mwanamke atoaye shukrani atie sadaka yake katika mfuko uliowekwa tayari.*

Kushukuru

¶ Aidha, yafaa aupokee Ushirika Utakatifu siku ile ile.

¶ Ikiwa mtoto wake alikuwa si riziki, au amekufa kabla mama yake hajashukuru, yafaa kusema Zaburi 124 badala ya Zaburi 121.

Ant. Msaada wangu.

Zab. 124.

1. Kama isingalikuwa Bwana aliye kuwa pa-moja nasi :
 Israeli na aseme sasa.
2. Kama isingalikuwa Bwana aliye kuwa pa-moja nasi :
 Bin Adamu alipotushambulia.
3. Papo hapo wangalitumeza hayi :
 Hasira yao ilipowaka juu yetu.
4. Papo hapo maji yangalitugharikisha :
 Mto ungalipita juu ya roho zetu.
5. Papo hapo yangalipita juu ya roho zetu :
 Maji yafurikayo.
6. Na ahimidiwe Bwana:
 Asiyetutoa kuwa mawindo kwa meno yao.
7. Roho yetu imeokoka kama ndege katika mtego wa wawindaji :
 Mtego umevunjika nasi tumeokoka.
8. Msaada wetu u katika Jina la Bwana :
 Aliyezifanya mbingu na nchi.
 Utukufu.

Ant. Msaada wangu u kwa Bwana : aliyezifanya mbingu na nchi.



LITANIA YA KANISA

¶ Litania hii isemwe au iimbwe kabla ya Missa kila Ijumaa mwaka mzima, isipokuwa ni Siku Kuu ya cheo cho chote, ndipo Litania isisemwe.

¶ Aidha, Siku za Kuombea, na Siku Kuu ya Marko Mtakatifu, Litania iimbwe kabla ya Missa, kwa kuandamana ikirwezekana ; au wakati mwingine katika Makanisa yenyе ka-waida ya kuandamana.

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Kristo, utusikie.

Kristo, utusikie.

Mungu Baba, wa mbinguni,
Uturehemu masikini wenye dhambi.

Mungu Mwana, Mkombozi,
Uturehemu masikini wenye dhambi.

Mungu Roho Mtakatifu,
Uturehemu masikini wenye dhambi.

Utatu Mtakatifu, Mungu mmoja,
Uturehemu masikini wenye dhambi.

Mariamu Mtakatifu, Mama wa Mungu Mwo-kozi wetu, Utuombee.

Enyi Malaika Watakatifu na Malaika Wakuu,
na madarajayotematakatifuya Pepo Wabarikiwa,
Mtuombee.

Enyi Baba Watakatifu, Manabii, Mitume,
Mashahidi, Waungamaji, Mabikira, na jeshi
lote barikiwa la mbinguni, *Mtuombee.*

Na maovu yote, *utuokoe, Bwana.*

Na dhambi zote, *utuokoe, Bwana.*

Na hasira yako, *utuokoe, Bwana.*

Na kupotea milele, *utuokoe, Bwana.*

Na upofu wote wa moyo, *utuokoe, Bwana.*

Na kiburi, majisifu, na unafiki, *utuokoe,*
Bwana.

Na husuda, chuki, na ukorofi, *utuokoe,*
Bwana.

Na kutokupendana kwote, *utuokoe, Bwana.*

Na uasherati na ulevi, *utuokoe, Bwana.*

Na dhambi nyingine zote za kufisha, *utuokoe,*
Bwana.

Na madanganya yote ya dunia, *utuokoe,*
Bwana.

Na tamaa mbaya za mwili, *utuokoe, Bwana.*

Na hila na jeuri za Shetani, *utuokoe,*
Bwana.

Na umeme na tufani, *utuokoe, Bwana.*

Na tauni na maradhi, *utuokoe, Bwana.*

Na nzige na njaa, *utuokoe, Bwana.*

Na hatari za nyama, *utuokoe, Bwana.*

Na vita, na uaji, na mauti ya ghafla, *utuokoe,*
Bwana.

Na fitina ya siri na kuasi, *utuokoe, Bwana.*

Na elimu yote ya uwongo, *utuokoe, Bwana.*

Na uzushi na kufarakana kwa Dini, *utuokoe,*
Bwana.

Kwa Siri ya Kufanyika mwili kwako kutaka-
tifu, *utuokoe, Bwana.*

Kwa Kuzaliwa kwako, *utuokoe, Bwana.*

Kwa Kutahiriwa kwako, *utuokoe, Bwana.*

Kwa Kubatizwa kwako, *utuokoe, Bwana.*

Kwa Kufunga kwako na Kujaribiwa kwako,
utuokoe, Bwana.

Kwa Huzuni yako na Hari ya Damu, *utuokoe,*
Bwana.

Kwa Msalaba wako na Kuteswa kwako,
utuokoe, Bwana.

Kwa Kufa kwako kwa thamani na Kuzikwa
kwako, *utuokoe, Bwana.*

Kwa Kufufuka kwako kutukufu, *utuokoe,*
Bwana.

Kwa Kupaa kwako kwa ajabu, *utuokoe,*
Bwana.

Kwa Kuja kwake Roho Mtakatifu, *utuokoe,*
Bwana.

Wakati wote wa kutaabika kwetu, *utuokoe,*
Bwana.

Wakati wote wa kufanikiwa kwetu, *utuokoe,*
Bwana.

Saa ya kufa kwetu, *utuokoe, Bwana.*

Siku ile ya hukumu, *utuokoe, Bwana.*

Sisi wenye dhambi.

Utusikie, twakusihî.

Upende kulitawala Kanisa lako Takatifu
Katholiko, lishike njia njema ;

Utusikie, twakusihî.

Upende kuwaangaza Maaskofu wote, Makasisi,
na Mashemasi, walieneze kwa kweli Neno lako ;

Utusikie, twakusihî.

Upende kumhifadhi N. Askofu wetu, na kumwongoza katika kazi zake zote ;

Utusikie, twakusih.

Upende kumbariki N. Mfalme wetu, na kumjalia amani katika ufalme wake wote ;

Utusikie, twakusih.

Upende kuwavika Wakuu wa Serkali, na Wazee wote, neema, hekima, na akili ;

Utusikie, twakusih.

Upende kuwabariki watu wako wote, na kuwalinda ;

Utusikie, twakusih.

Upende kuwapa mataifa yote umoja, amani, na urafiki ;

Utusikie, twakusih.

Upende kutujalia moyo wa kukupenda na kukucha, na kufuata kwa bidii amri zako ;

Utusikie, twakusih.

Upende kuongeza hesabu ya watu wanaokufanya kazi katika nchi hii ;

Utusikie, twakusih.

Upende kuwaleta katika njia yako Waislamu, Mabanyani, na wote wasioijua kweli yako ;

Utusikie, twakusih.

Upende kuwaimarisha wasimamao ; kuwafariji walio na moyo dhaifu ; kuwainua waangukao ; na hatimaye kumwangusha Shetani chini ya miguu yetu ;

Utusikie, twakusih.

Upende kuwatanza wajane wote na yatima, na wote walio katika hatari, shida, na taabu ;

Utusikie, twakusih.

Upende kuwashifadhi wote wanaosafiri, katika nchi, hewani, na juu ya bahari ;

Utusikie, twakusih.

Upende kuwasaidia wanawake wote walio na utungu wa kuzaa ; wagonjwa wote ; na watoto wote walio wachanga ;

Utusikie, twakusih.

Upende kuwahurumia wafungwa wote, na wote waliotekwa vitani ;

Utusikie, twakusih.

Upende kuwasamehe adui zetu, nao watusingiziao na kutuudhi, uwageuze miyo ;

Utusikie, twakusih.

Upende kutuhifadha mazao ya nchi kwa jinsi yake, tupate kuyafurahia wakati wake ;

Utusikie, twakusih.

Upende kuwapa waaminifu wote walioifariki dunia faraja, nuru, na amani ;

Utusikie, twakusih.

Upende kutujalia toba la kweli ; kutusamehe dhambi zetu zote, na ulegevu wetu, na ujinga wetu ; utukirimie neema ya Roho yako Mtakatifu, ili tutengeneze maisha yetu kwa Neno lako takatifu ;

Utusikie, twakusih.

Mwana wa Mungu ;

Utusikie, twakusih.

Kristo, utusikie.

Kristo, utusikie.

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Baba yetu.

V. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R/. Kilio changu kikufikie.

V. Bwana akae nanyi.

R/. Akae na roho yako.

Tuombe.

Ee Mungu, ni sifa yako kurehemu na kusamehe siku zote : Uyakubali maombi yetu ; na kwa huruma zako utufungue sisi tuliofungwa kwa minyororo ya dhambi zetu. Kwa.

V. Bwana akae nanyi.

R/. Akae na roho yako.

V. Bwana Mwenyezi na mwenye rehema atusikie.

R/. Amin.

Roho za waaminifu kwa rehema ya Mungu wastarehe katika amani.

R/. Amin.

WAKATI WA VITA

¶ *Mwisho wa Litania, baada ya Baba yetu, iimbwe,*

Ant. Ee Bwana, uondoke, uwe msaada wetu : utukomboe kwa ajili ya fadhili zako.

Zab. Ee Mungu, tumesikia kwa masikio yetu, baba zetu wametuambia : matendo uliyoyatenda siku zao, siku za kale.

Utukufu. *Ant.* Ee Bwana.

V. Ee Kristo, utulinde na adui zetu.

R/. Uyaangalie kwa wema mateso yetu.

V. Utazame kwa huruma huzuni yetu.

R/. Utusamehe kwa rehema dhambi zetu.

V. Uzisikie kwa upole sala zetu.

R/. Ee Mwana wa Mungu aliye hayi, uturehemu.

V. Sasa na daima upende kutulinda, Ee Kristo.

R/. Ee Kristo, utusikie, utusikie, Ee Kristo.

¶ *Ndipo Kasisi aimbe,*

V. Ee Bwana, utuokoe sisi watumishi wako.

R/. Tunaokutumaini Wewe.

V. Ee Bwana, uwe kwetu ngome yenyen guvu.

R/. Adui asitupate.

V. Ee Bwana, adui asituonee.

R/. Wala mwana wa uovu asitutese.

V. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R/. Kilio changu kikufikie.

V. Bwana akae nanyi.

R/. Akae na roho yako.

Tuombe.

Ee Bwana, tunakusihii, utazame kwa huruma udhaifu wetu : uyaepushie mbali nasi mabaya yote tuliyoyastahili ; utujalie tukutumaini Wewe katika taabu zetu zote, tuokoke mikononi mwa adui zetu, tukuabudu pasipo hofu katika utakatifu na kwa haki mbele zako siku zetu zote. Kwa.

V. Bwana akae nanyi.

R/. Akae na roho yako.

V. Bwana Mwenyezi na mwenye rehema atusikie.

R/. Amin.

Roho za waaminifu kwa rehema ya Mungu wastarehe katika amani.

R/. Amin.

¶ Sala nyagine.

Ee Mungu, waweza kukomesha vita na kuwashinda adui zao wakutumainio : tunaku-sihi utusaidie, sisi watumishi wako tunaojitakia rehema ; ili tuondolewe ukali wa adui zetu, na kukuhimidi kwa shukrani isiyokoma. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

WAKATI WA NJAA

¶ Mwisho wa Litania, baada ya Baba yetu, iimbwe.

Ant. Bwana wetu mkuu na mwangi wa nguvu : akili zake hazina idadi.

Zab. 147.

1. Ni vyema kumwimbia Mungu wetu : maana kwapendeza, kusifu ni kuzuri.

2. Bwana ndiye aijengaye Yerusalem : hu-wakusanya waliotawanyika wa Israeli.

3. Huwaponya waliopondeka moyo : na kuzifunga jeraha zao.

4. Huihesabu idadi ya nyota : huzipa zote majina.

5. Bwana wetu mkuu na mwangi wa nguvu : akili zake hazina idadi.

6. Bwana huwategemeza wenye upole : hu-waangusha chini wasio haki.

7. Mwimbieni Bwana kwa kushukuru : mwimbieni Mungu wetu kwa kinubi.

8. Huzifunika mbingu kwa mawingu, huite-ngezeza nchi mvua : huyameesha majani milimani.

9. Humpa nyama chakula chake : wana kunguru wamliliao.

10. Hapendezwi na nguvu za farasi : wala hairidhii miguu ya mtu.

11. Bwana huwaridhia wamchao : wazingo-jao fadhili zake.

Utukufu.

Ant. Bwana wetu mkuu na mwangi wa nguvu : akili zake hazina idadi.

¶ Ndipo Kasisi aimbe.

¶ Ee Bwana, uzifunike mbingu kwa mawingu

R/. Na kuitengenezea nchi mvua.

¶ Uyameeshe majani kwa makundi.

R/. Na maboga kwa matumizi ya mwana-damu.

¶ Uinyweshe milima toka orofa zako.

R/. Nchi ishibe kwa mazao ya kazi zako.

¶ Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R/. Kilio changu kikufikie.

¶ Bwana akae nanyi.

R/. Akae na roho yako.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, tunakusihi : Utujalie tuzi-tumainie rehema zako katika shida zetu zote ; utulinde kwa nguvu zako wakati wote wa kutaabika kwetu. Kwa.

¶ Bwana akae nanyi.

R/. Akae na roho yako.

¶ Bwana Mwenyezi na mwenye rehema atusikie.

R/. Amin.

Roho za waaminifu kwa rehema ya Mungu wastarehe katika amani.

R/. Amin.

Litania

¶ Sala nyine.

Uzisikilize haja zetu, Ee Bwana, tunazokuumba kwa unyenyekevu : Na kwa rehema zako utuepushe na njaa ; ili sisi tuliojipatia adhabu kwa makosa yetu tuponywe kwa huruma zako. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ Kuomba mvua.

Ee Mungu, ndani yako Wewe tunaishi, tunakwenda, tuna uhayi wetu : Utujalie mvua ya kadiri utakayoona vema ; ili sisi tupokee baraka zako za maisha haya, na kuzidi kutafuta kwa bidii baraka za milele. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

WAKATI WA MARADHI

¶ Mwisho wa Litania, baada ya Baba yetu, iimbwe,

Ant. Ee Bwana, uwafurahishe wote wakutafutao : waseme daima, Atukuzwe Mungu.

Zab. 70.

1. Ee Mungu, uniokoe : Ee Bwana, unisaidie hima.

2. Waaibike, wafedheheke : wanaoitafuta roho yangu.

3. Warudishwe nyuma, watahayarishwe : wapendezwao na shari yangu.

4. Na warudi nyuma kwa sababu ya aibu yao : wanaosema, Ewe ! Ewe !

5. Washangilie, wakufurahie : wote wakutafutao.

Litania

6. Waupendao wokofu wako : waseme daima, Atukuzwe Mungu.

7. Nami ni masikini na mhitaji : Ee Mungu, unijilie kwa haraka.

8. Ndiwe msaada wangu na mwokozi wangu : Ee Bwana, usikawie.

Utukufu.

Ant. Ee Bwana, uwafurahishe wote wakutafutao : waseme daima, Atukuzwe Mungu.

¶ Ndipo Kasisi aimbe,

¶. Ee Bwana, utuokoe sisi watumishi wako.

R. Tunaokutumaini Wewe.

¶. Ee Bwana, utupelekee msaada toka patakatifu pako.

R. Na kututegemeza toka Sayuni.

¶. Ee Bwana, usitutende kwa kadiri ya hatia zetu.

R. Wala usitulipe kwa kadiri ya maovu yetu.

¶. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Kilio changu kikufikie.

¶. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu mwenye rehema, unasiliza kilio chao wenyе toba na haja zao wenyе kulemewa : Uzikubali dua zetu tunazokuumba katika taabu na misiba yetu ; utujalie mabaya yote, yatupatayo kwa hila ya Shetani au kwa werevu wa wanadamu, yaondolewe ; ili sisi watumishi wako tulindwe na madhara yote, tukushukuru daima katika Kanisa lako Takatifu. Kwa.

V. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

V. Bwana Mwenyezi na mwenye rehema atusikie.

R. Amin.

Roho za waaminifu kwa rehema ya Mungu wastarehe katika amani.

R. Amin.

¶ Sala nyininge.

Ee Mungu, hupendi mwenye dhambi afe, bali atubu akaishi : Uwatazame kwa huruma watu wako wanapokurudia ; ili tuondolewe mapigo yako, na kukutumikia kwa uaminifu. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

MAOMBEZI MENGINE

¶ Sala nyininge zitumikazo mwisho wa Litania ; yaani, baada ya Sala ya kawaida.

Ee Bwana, tunakusihi, uzikubali dua zetu : Utusamehe dhambi zetu tunazozitungama kwako ; ili tupewe ghofira na amani. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Ee Bwana, mwenye huruma isiyo kiasi, utuonyeshe rehema zako : Utusamehe dhambi zetu ; na kutuokoa katika adhabu tulizozistahili. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Ee Mungu, wachukizwa kwa kosa na kurdhishwa kwa toba : Uzikubali kwa rehema sala za watu wako wakuombao ; utuepushie mbali hasira yako tunayostahili kwa dhambi zetu. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Mwenyezi Mungu uishiye milele, umrehemu mtumishi wako N. Askofu wetu : Na kwa huruma yako uielekeze njia yake hata aupate wokofu wa milele ; ili kwa neema yako ayatake yakupendezayo, akayatimize kwa bidii yake yote. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Ee Mungu, kwako Wewe hutoka haja takatifu, mashauri mema, na matendo ya haki : Utupe sisi watumishi wako amani tusiyoweza kupewa na dunia ; ili, tukishika amri zako kwa moyo na kuondolewa hofu ya adui, tukae kwa amani chini ya hamaya yako. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Ee Bwana, utuchome moto wa Roho Mtakatifu viuno na mioyo : Ili tukutumikie wenyе miili safi ; tukupendeze wenyе mioyo safi. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Ee Mungu, umewaumba waaminifu wote na kuwaokoa : Uzijalie roho za watumishi na wajakazi wako ondoleo la dhambi zao zote ; wapewe, kwa sala za pendo, masamaha waliyayataka siku zote. Uishiye na kumiliki, Mungu, milele na milele. *Amin.*

Ee Bwana, tunakusihi, katika matendo yetu yote utuongoze kwa neema yako : Utufanikishe daima kwa msaada wako ; ili sala zetu zote na kazi zetu zianze kwako, na kwako zifulizwe na kumalizika. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Mwenyezi Mungu wa milele, Bwana wa wahayi na wafu, umewarehemu wote waliojulika kuwa wako, wakikuamini na kukutii : Tunawaombea kwako tuwakumbukao mbele zako, wengine wangali wamo katika mwili hapa

Maji ya Baraka

duniani, wengine wamekwisha kutoka katika mwili na kufika ahera ; uwakarimie baraka zako, wasamehewe dhambi zao, wakapewe furaha za milele. Kwa.

KAWAIDA YA KUNYUNYI-ZIWA MAJI YA BARAKA

¶ *Ibada hii itumike kabla ya Missa kila Siku ya Bwana mwaka mzima.*

Ant. Unisafishe, Ee Bwana, kwa husopo, nami nitakuwa safi : unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko thuluji.

Zab. Unirehemu, Ee Mungu : kwa kadiri ya fadhili zako.

Utukufu.

Ant. Unisafishe, Ee Bwana, kwa husopo, nami nitakuwa safi : unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko thuluji.

¶. Ee Bwana, utuonyeshe rehema zako.

R. Utupe wokofu wako.

¶. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Kilio changu kikufikie.

¶. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Utusikie, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele : Ukubali kumtuma Malaika wako mtakatifu kutoka mbinguni awajie wote

Maji ya Baraka

wakaao nyumbani humu ; awahifadhi, awaburudishe, awaponye na kuwalinda. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

WAKATI WA PASAKA

Ant. Nalionna maji yakitoka hekaluni upande wa kuumi, Haleluya : na wote waliofikiwa na maji hayo wakaokoka ; nao husema, Haleluya, Haleluya.

Zab. Mshukuruni Bwana kwa kuwa yu mwema : kwa maana fadhili zake ni za milele.

Utukufu.

Ant. Nalionna maji yakitoka hekaluni upande wa kuumi, Haleluya : na wote waliofikiwa na maji hayo wakaokoka ; nao husema, Haleluya, Haleluya.

¶. Ee Bwana, utuonyeshe rehema zako. Haleluya.

R. Utupe wokofu wako. Haleluya.

¶. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Kilio changu kikufikie.

¶. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Utusikie, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele : Ukubali kumtuma Malaika wako mtakatifu kutoka mbinguni awajie wote wakaao nyumbani humu ; awahifadhi, awaburudishe, awaponye na kuwalinda. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*



Jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu.



MISSA TAKATIFU

MISSA YA WANAFUNZI.

¶ Kasisi aseme, watu wote wakimwitikia,
KWA ✠ Jina la Baba na Mwana na Roho
 Mtakatifu. Amin.

¶ Nitakwenda madhbahuni kwa Mungu.
 R^y. Kwa Mungu aliye furaha yangu na
 shangwe yangu.

Zab. 43.

(*Isisemwe katika Missa ya Wafu.*)

¶ UNIHUKUMU, Bwana, unitetee kwa taifa
 lisilo haki : uniokoe na mtu wa hila, asio haki.

R^y. Kwa kuwa Wewe ndiwe Mungu wa nguvu
 zangu ; kwa nini umenifukuza : kwa nini
 ninakwenda nikihuzunika, adui wakinionea ?

¶ Niletewe nuru yako na kweli yako,
 ziniongoze : zinifikishe kwenye mlima wako
 mtakatifu na hata masikani zako.

R^y. Hivyo nitakwenda madhbahuni kwa
 Mungu, kwa Mungu aliye furaha yangu na
 shangwe yangu : nitakusifu kwa kinubi, Mungu,
 Mungu wangu.

¶ Ya nini umeinama, roho yangu : na
 kufadhaika ndani yangu ?

R^y. Umtumaini Mungu, kwa maana nitakuja
 kumsifu : aliye afya ya uso wangu na Mungu
 wangu.

¶ Utukufu una Baba, na Mwana : na Roho
 Mtakatifu,

Missa

R. Ulivyokuwa mwanzo : ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. Amin.

V. Nitakwenda madhbahuni kwa Mungu.

R. Kwa Mungu aliye furaha yangu na shangwe yangu.

V. ✠ Msaada wetu u katika Jina la Bwana.

R. Aliyezifanya mbingu na nchi.

¶ Kasisi aseme,

NAUNGAMA kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watakatifu wote, na kwenu, ndugu, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo, na maneno, na matendo ; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Kwa hiyo nawasihi Watakatifu wote waniombee, nanyi, ndugu, mniombee kwa Bwana Mungu wetu.

¶ Watu wakamjibu,

MWENYEZI Mungu akurehemu, akusamehe makosa yako, akufikishe kwenye uzima wa milele. Amin.

¶ Ndipo watu waseme,

NAUNGAMA kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watakatifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo, na maneno, na matendo ; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Kwa hiyo nawasihi Watakatifu wote waniombee, na wewe, baba, unionbee kwa Bwana Mungu wetu.

¶ Kasisi awajibu,

MWENYEZI Mungu akurehemuni, akusameheni makosa yenu, akufikisheni kwenye uzima wa milele. Amin.

BWANA Mwenyezi na mwenye rehema atujalie masamaha, ✠ ghofira, na ondoleo la dhambi zetu. Amin.

Missa

V. Urudi Ee Mungu, utuhuishe.

R. Watu wako wakufurahie.

V. Ee Bwana, utuonyeshe rehema zako.

R. Utupe wokofu wako.

V. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Kilio changu kikufikie.

V. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

MWENYEZI Mungu, kwako Wewe mioyo yote i wazi, haja zote zimejuliwa, wala hakuna la siri usilolijua : Uyasafishe mawazo ya mioyo yetu kwa kutupuzia Roho yako Mtakatifu ; ili tukupende hasa, na kuliadhimisha Jina lako takatifu kama itupasavyo. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

¶ Akiubariki uvumba aseme,
Mungu tutakayemtolea uvumba huu, apende ✠ kuubariki.
Amin.

¶ Kisha asimame penye kitabu, aisome
INTROIT.

¶ Kisha asimame kati ya madhbahu, aseme
pamoja na watu, au watu waimbe,

Bwana, uturehemu (ij.)

Kristo, uturehemu (ij.)

Bwana, uturehemu (ij.)

¶ Kisha watu waseme, au waimbe, ikiwa
imeamriwa,

UTUKUFU una Mungu juu, katika nchi amani,
kwa watu aliowaridhia. Twakusifu, twakuhimidi,
twakuabudu, twakutukuza, twakushukuru kwa
ajili ya utukufu wako mkuu, Bwana Mungu,
Mfalme wa mbinguni, Mungu Baba Mwenyezi.

Bwana, Mwana pekee, Yesu Kristo ; Bwana Mungu, Mwana Kondoo wa Mungu, Mwana wa Baba, uzichukuaye dhambi za ulimwengu, uturehemu. Uzichukuaye dhambi za ulimwengu, ukubali kuomba kwetu. Uketiye mkono wa kuumi wa Mungu Baba, uturehemu.

Kwa kuwa ndiwe uliye peke yako Mtakatifu ; ndiwe peke yako Bwana ; ndiwe peke yako uliye juu, Yesu Kristo, pamoja na † Roho Mtakatifu, katika utukufu wake Mungu Baba. Amin.

¶ Kisha Kasisi awakabili watu, aseme,

V. Bwana akae nanyi,

R \ddagger . Akae na roho yako.

[¶ Askofu asema,

V. Amani kwenu.

R \ddagger . Ikae na roho yako.]

¶ Akisimama penye kitabu, aseme,

Tuombe.

SALA.

¶ Kisha alitangaze somo,

Somo katika Waraka wa N. Mtume mbarikiwa, kwa N. au, Somo katika kitabu cha Nabii N.

SOMO.

R \ddagger . Tumshukuru Mungu (isiimbwe).

¶ Kisha aisome,

GRADUALE.

¶ Kabla ya Injili Kasisi aseme, kwa sauti ya siri, kati ya madhbahu,

Mwenyezi Mungu, unitakase moyo na midomo, kama vile ulivyonakasa midomo Nabii Isaya kwa kaa la moto. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

Bwana unibariki : Bwana awe moyoni mwangu na midomoni mwangu, ili niitangaze Injili yake inipasavyo. Amin.

¶ Akiubariki uvumba aseme,
Mungu, tutakayemtolea uvumba huu, apende † kuubariki.
Amin.

¶ Akimbariki Shemasi katika Missa Kuu.

Bwana awe moyoni mwako na midomoni mwako, ili uitangaze Injili yake ikupasavyo. † Kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Amin.

¶ Kisha aseme,

V. Bwana akae nanyi.

R \ddagger . Akae na roho yako.

† Sehemu ya Injili takatifu, kama ilivyoandonikwa na N. Mtakatifu.

R \ddagger . Atukuzwe Bwana.

INJILI.

R \ddagger . Asifiwe Kristo (isiimbwe).

¶ Siku ya Bwana, na Siku Kuu zilizo kubwa,
hapa hufuata

HOTUBA.

KUWARUHUSU WASIO AMANI

¶ Kila Siku ya Bwana Kasisi asimame kati ya Wanafunzi, akiikabili madhbahu, aseme,
Wanafunzi, mwombeni Bwana.

Sisi tuaminio tuwaombee Wanafunzi wote wa Kanisa Katholiko.

¶ Kisha aseme, wakiitikia Wakristo na Wanafunzi.

V. Ee Bwana, uwafundishe elimu ya haki.

R \ddagger . Bwana, uwarehemu.

V. Uwafunulie Injili ya kweli.

R \ddagger . Bwana, uwarehemu.

V. Uwaunganishe na Kanisa lako Takatifu,
Katholiko, Apostoliko.

R \ddagger . Bwana, uwarehemu.

¶ Ee Bwana, uwalinde na mabaya yote.
R. Bwana, uwarehemu.

Tuombe.

BWANA, Mungu wetu, uliyempeleka Mwana wako pekee, Yesu Kristo, awe wokofu wa wana-damu wote : Tunakuomba uwaangalie watumihi wako, wanafunzi wake, uwape Ubatizo Utakatifu kwa wakati wako ; ili hawa, pamoja na sisi, walitukuze Jina lako takatifu la. Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote na hata milele na milele. *Amin.*

¶ Ndipo awageukie Wanafunzi na kuvaruhusu.

Wanafunzi wa Kristo, nendeni zenu.

¶ Siku Kuu zisizo Siku za Bwana ni halali kurukiza ¶. na R/R. na kuisema Sala peke yake.

¶ Kisha asimame kati ya watu wenye kitubio cha Kanisa, akiikabili madhbahu, aseme,

Wenye kitubio cha Kanisa, ombeni.

Sisi nasi tuwaombee hawa ndugu zetu wenye kitubio.

Tuombe.

MUNGU Mwenyezi wa milele, Baba wa mbinguni : Tunakuomba uwatazame watu hawa wanaokurudia, kama yule mwana mpotevu alivyomrudia baba yake, akakubaliwa naye kwa kuwa alitubu ; uwakubali, uwarudishe katika Kanisa lako takatifu, wenye hali ya sifa na heshima. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ Ndipo awageukie na kuvaruhusu.

Wenye kitubio cha Kanisa, nendeni zenu.

MISSA YA WAAMINIFU.

¶ Kisha watu waseme, au waimbe, ikiwa imeamriwa,

NAMWAMINI Mungu mmoja, Baba Mwenyezi, Muumba mbingu na nchi, Na vitu vyote vinavyo-onekana na visivyoonekana.

Na Bwana mmoja Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu, Mwana wa azali wa Baba. Yu Mungu anatoka katika Mungu, Yu Nuru anatoka katika Nuru, Yu Mungu kweli anatoka katika Mungu kweli, Mwana wa azali asiyeumbwa, Mwenye Uungu mmoja na Baba, Kwa Yeye huyu vitu vyote vyaliumbwa. Aliyeshuka kutoka mbinguni, kwa ajili yetu wanadamu, na kwa wokofu wetu. (*Piga magoti*) Akatwaa mwili kwa uweza wa Roho Mtakatifu katika Bikira Mariamu, Akawa mwana Adamu. (*Simama*) Akasulibiwa kwa ajili yetu, zamani za Pontio Pilato, Aliteswa, akazikwa. Siku ya tatu akafufuka kama yanenavyo Maandiko matakatifu, Akapaa mbinguni, Ameketi mkono wa kuumi wa Baba. Naye atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu watu wahayi na wafu, Na milki yake haina mwisho.

Namwamini Roho Mtakatifu, Bwana, Mtoa uzima, Atokaye katika Baba na Mwana, Anayeabudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana, Aliyenena kwa vinywa vya Manabii. Naamini Kanisa Moja, Takatifu, Katholiko, na Apostoliko. Nakiri Ubatizo umoja wa kuondolea dhambi. Natazamia Kiyama ya wafu, ✕ Na uzima wa ulimwengu ujao. *Amin.*

¶ Kisha awakabili watu, aseme,

V. Bwana akae nanyi.

Rv. Akae na roho yako.

¶ Ndipo aikabili madhbahu, aisome

OFFERTORIO.

¶ Kasisi aweke tayari mkate, na divai kwa maji, kama ilivyoamriwa katika amri za Kanisa la Unguja, akisema sala hizi, kila sala kwa wakati wake, kwa sauti ya siri.

Baba Mtakatifu, Mungu Mwenyezi, wa milele, uikubali sadaka hii safi, ambayo mimi mtumishi wako, nisiyestahili, ninakutolea, Ee Mungu wangu uliye hayi, wa kweli, kwa ajili ya dhambi na makosa yetu yasiyohesabika ; na kwa ajili ya wote wanaohudhuria, na kwa ajili ya Wakristo waaminifu wote, wahayi na wafu ; itupatie wokofu na, mwisho wake, uzima wa milele. Amin.

Mungu, uliumba ¶ utu wetu mtakatifu kwa jinsi ya ajabu, ukaufanya upya kwa ajabu izidiyo ; utujalie kwa njia ya siri hii ya maji na divai, tushirikishwe Uungu wake asiyekataa kuushiriki utu wetu, Yesu Kristo Mwana wako, Bwana wetu ; Aishiye na kumiliki pamoja nawe, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima milele na milele. Amin.

Tunakutolea, Bwana, kikombe hiki cha wokofu, tukikumba, kwa rehema yako, kipandishwe mbele yako mbinguni, kiwe na kibali machoni pako, kwa ajili ya wokofu wetu sisi na wa ulimwengu pia. Amin.

Tukinyenyekea kwako, Baba, na kuleta majuto ya moyoni, tukubaliwe nawe : sadaka yetu itolewe vizuri leo mbele yako, ili ikupendeze Wewe, Bwana Mungu.

Mungu Mwenyezi, wa milele, ututakasaye, uje : uibariki ¶ sadaka hii iliyowekwa tayari kwa utukufu wa Jina lako.

¶ Akiubariki uvumba aseme,

Kwa kuombea Gabrieli Mbarikiwa, Malaika Mkuu, asimamaye kuumeni pa madhbahu ya uvumba, na kwa kuombea Watakatifu wote, upende, Bwana, kuubariki ¶ uvumba huu. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

¶ Akiifukizia sadaka.

Uvumba huu uliubariki, Bwana, upae mbele zako ; rehemaa yako ikatushukie.

¶ Akiifukizia madhbahu.

Sala yangu ipae, Ee Bwana, mbele zako kama uvumta : na kuinuka kwa mikono yangu kama dhabihu ya jioni.

Uweke mlizzi, Ee Bwana, kinywani pangu : ungojee mlangoni pa midomo yangu.

Usielekeze moyo wangu kunako jambo baya : nisizoelee matendo yasiyofaa ; pamoja na watu watendao maovu.

¶ Akimpa Shemasi chetezo.

Bwana auwashe ndani yetu moto wa upendo wake, na mwako wa upendano wa milele. Amin.

¶ Akinawa mikono.

Nitanawa mikono yangu kwa kutokuwa na kosa : nitazunguka madhbahu yako, Ee Bwana. Nipaaze sauti ya kushukuru : niieneze miujiza yako yote. Ee Bwana, nimependa makao ya nyumba yako : na mahali pa masikani ya utukufu wako. Usitie roho yangu pamoja na wenye dhambi : wala maisha yangu pamoja na watu wamwagao damu. Mikononi mwao mna madhara : na mkono wao wa kuume umejaa rushwa.. Lakini mimi kwa ukamilifu wangu nitakwenda : unikomboe, unirehemu. Mguu wangu unasimama palipo sawa : katika makusanyiko nitamkuza Bwana.

Utukufu una Baba, na Mwana : na Roho Mtakatifu.

Ulivyokuwa mwanzo : ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. Amin.

¶ Akisimama kati ya madhbahu.

Utatu Mtakatifu, uikubali sadaka hii tuitoayo kwako, tukimkumbuka Bwana wetu Yesu Kristo, alivyoteswa na kufufuka na kupaa mbinguni: nasi tunakuomba Watakatifu wako walioko mbinguni watuombee sisi tuwakumbukao hapa duniani. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

¶ Kisha awakabili watu, aseme,

OMBENI, ndugu, sadaka yangu na yenu iwe na kibali kwa Mungu, Baba Mwenyezi.

Rv. Bwana aikubali hii sadaka mikononi mwako, kwa sifa na utukufu wa Jina lake, kwa faida yetu, na kwa faida ya Kanisa lake takatifu pia.

Kasisi, kwa sauti ndogo, Amin.

¶ Aseme kwa siri,

SALA ZA SIRI.

Missa

¶ Apaaze sauti, aseme, au aimbe,
Daima milele na milele.

R^y. Amin.

¶. Bwana akae nanyi.

R^y. Akae na roho yako.

¶. Inueni mioyo.

R^y. Twaiinua kwa Bwana.

¶. Na tumshukuru Bwana Mungu wetu.

R^y. Ina haki, tena ni wajibu.

SIKU YA BWANA.

¶ Siku ya Bwana, isiyo na Dibaji yake, aseme, au aimbe,

NDIO wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.

Wewe, pamoja na Mwana wako pekee na Roho Mtakatifu, U Mungu mmoja, Bwana mmoja : umoja wako si mithili ya nafsi iliyo moja, bali ni Utatu wa Uungu mmoja. Kwa maana yote tuyaa miniyo juu ya utukufu wako tuliofunuliwa, ndiyo tuyaa onayo juu ya Mwana wako, na juu ya Roho Mtakatifu, tusitie tofauti wala kupambanua. Hata tuukiripo Uungu wa kweli, wa milele, huabudika tofauti za nafsi, na umoja wa Uungu, na utukufu sawa sawa.

Ndizo waziabudu zo Malaika na Malaika Wakuu, Makerubi nao, na Maserafi, ambao kila siku, kwa sauti moja, wanakuimbia hawaachi, wakisema,

Missa

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe, Bwana uliye juu.

Ndiye ✕ mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.

SIKU ZA KAZI

¶ Siku za kazi zisizo na Dibaji yake, aseme, au aimbe,


NDIO wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.


Kwa Kristo Bwana wetu.

Kwa Yeye sisi nasi, pamoja na Malaika na Malaika Wakuu, na jeshi la mbinguni lote pia, twakutukuza na kuliadhimisha Jina lako tukufu; tukikusifu daima, tukisema,

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe, Bwana uliye juu.

Ndiye ✕ mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.





Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu.

SALA YA KANUNI

Ndipo Kasisi aseme,
Mwenyezi Mungu wa milele, tunakusih
 i uzipokee ✕ sadaka ✕ hizi ✕ zetu,
 pamoja na sala zetu.

Tunakuomba ulipuuzie Kanisa lako Katholiko
 roho ya kweli na ya kupatana.

Umlinde mfalme wetu, N. utujalie tutawaliwe
 chini yake kama vile upendavyo Wewe.

Baba wa mbinguni, umbariki Askofu wetu, N.
 uwabariki na Maaskofu wote, na wote wachungao
 roho za watu, walihubiri neno lako kwa mafu-
 ndisho yao na kwa mwenendo wao safi.

UWAPE neema watu wako wote, wakutu-
 mikie kwa kweli siku zao zote.

Tena, uwasaidie walio na taabu, huzuni,
 ugonjwa, au haja nyingineyo yote ; hasa N.
 na N.

Tunakuomba utubariki na sisi tulipo hapa,
 tunafanya ukumbusho wa kufa kutukufu kwa
 Mwana wako, Kristo Bwana wetu. *Amin.*

NASI tunakushukuru sana kwa kuwa
 umetuonyesha uweza wa neema yako
 katika Watakatifu wako wote ; zaidi katika
 Mariamu Bikira mbarikiwa mtukufu, Mama wa
 Mwana wako Yesu Kristo, Bwana wetu na
 Mungu wetu ; na katika Babu Watakatifu,
 katika Manabii, Mitume, na Mashahidi.

Tunakuomba, Bwana, tuwaafuatise hawo,
 imani yao na utii wao, kwa Kristo Bwana wetu.
Amin.

TENA, Bwana, tunawatakia rehema watumishi wako wote waliofariki dunia katika imani ; hasa N. na N. uwajalie, tunaku-sihi, rehema yako na amani ya milele, ukawafikishe pamoja na sisi, siku ya kiyama, kunako utukufu wa Mwana wako.

Utujalie haya, Baba, kwa ajili yake Yeye, Yesu Kristo, Msuluhiha na Mwombezi wetu. *Amin.*

E E Mungu, Baba wa mbinguni, kwa wema na huruma zako ultupa Mwana wako pekee, Yesu Kristo, afe katika msalaba kwa ukombozi wetu, naye alijitoa nafsi yake kuwa sadaka isiyo mfano, awe dhabihu timilifu, sadaka kamili, na kafara ya kutosha, kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote. (*Hapa watu wote wapige magoti.*) Ameliamuru kumbukumbu la kufa kwake kwa thamani, na, katika Injili yake takatifu, ametususia tulifulize daima hata atakaporudi.

UTUSIKIE, tunakuomba, Ee Baba wa rehema, uvibariki ✠ viumbe hivi vyako, ✠ mkate na ✠ divai, na kuvitakasa kwa Roho yako Mtakatifu na kwa Neno lako, viwe kwetu Mwili ✠ wa thamani wa Mwana wako Yesu Kristo, na Damu ✠ yake.

YEYE usiku ule ule aliotolewa alitwaa mkate, akainua macho yake kwako, Mungu Baba Mwenyeze, akashukuru, akau ✠ bariki, akau-mega, akawapa wanafunzi wake, akisema, Twaeni, mle, HUU NDIO MWILI WANGU ULIOTOLEWA KWA AJILI VENU. Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.

NA vivi hivi baada ya kula, akakitwaa kikombe, akashukuru, akaki ✠ bariki, akawapa wanafunzi wake, akisema, Nyweeni

nyote hiki ; kwa maana HII NDIYO DAMU YANGU YA AGANO JIPYA, IMWAGIKAYO KWA AJILI YENU NA KWA WATU WENGI ILI IWE ONDOLEO LA DHAMBI. Fanyeni hivi, kila mtakapokunywa, kwa ukumbusho wangu. *Amin.*

KWA hiyo, Ee Bwana, Baba wa mbinguni, sisi watumishi wako tunatoa Sadaka kwako, uliye peke yako Mtukufu, ndiyo vitu vyako uliviyotupa, Sadaka hii ✠ safi, Sadaka ✠ takatifu, Sadaka ✠ isiyo mawaa, Mkate ✠ wa uzima wa milele, na Kikombe ✠ cha wokofu wa daima ; tukikukumbuka Kuteswa kutakatifu kwa huyu, Kristo, Mwana wako Bwana wetu, na Kufufuka kwake kwa uweza, na Kupaa kwake kutukufu ; na kukushukuru kwa mema yote kuliyyotupatia. *Amin.*

TUNAKUOMBA, Baba uliye mwema, uikubali Sadaka hii yetu ikutukuzayo na kukushukuru ; utujalie sisi, pamoja na Kanisa lako pia, masamaha ya dhambi zetu, na mema yote yaliyopatikana kwa mateso ya Mwana wako impendwa.

NASI, Ee Bwana, tunajitoa sadaka kwako, nafsi zetu, roho zetu, na miili yetu. Tunakuomba ye yote atakaevipokea vitakatifu hivi aushiriki vema Mwili ✠ wa thamani wa Mwana wako Yesu Kristo na Damu ✠ yake, ajazwe neema na baraka yako ya mbinguni, na kufanywa mwili mmoja naye. *Amin.*

NASI tusiostahili tunakuomba, Ee Baba, uamuru Sadaka hii yetu ichukuliwe na Malaika wako mtakatifu, pamoja na sala zetu, kunako madhbahu ya juu, mbele yako Mungu uliye Mtukufu, Kwa ✠ Kristo ✠ Bwana ✠ wetu.

KWA ✠ Yeye, pamoja na ✠ Yeye, na
ndani yake ✠ Yeye, iwe kwako Mungu
Baba ✠ Mwenyezi, katika umoja wa Roho ✠
Mtakatifu, heshima yote na utukufu,
Daima milele na milele.

R/. Amin.

Tuombe.

Kama vile Mwokozi wetu Kristo alivyotuagiza,
akatufundisha, tunathubutu kusema,

BABA yetu, uliye mbinguni ; Jina lako
takatifu litukuzwe, Ufalme wako uje,
Mapenzi yako yatimizwe, Hapa duniani kama
huko mbinguni. Utupe leo riziki zetu. Utusa-
mehe makosa yetu, Kama sisi tunavyowasamehe
waliotukosa. Usitutie majaribuni, Lakini
utuokoe na maovu. Amin.

UTUOKOE, tunakuomba, Ee Bwana, na
maovu yote. Ukubali maombezi atuombe-
ayo Mariamu Bikira wa daima, Mama wa
Mungu, pamoja na Mitume wako wabarikiwa,
na Watakatifu wako wote ; utupe amani siku
zetu ; utusaidie kwa rehema zako, tukae mbali
na dhambi siku zote, wala tusifadhaike kwa
neno lo lote. Kwa Yeye, Bwana wetu Yesu
Kristo Mwana wako ; Aishiye na kumiliki
pamoja nawe, katika umoja wa Roho Mtakatifu,
Mungu,

Daima milele na milele.

R/. Amin.

AMANI ya ✠ Bwana ikae ✠ nanyi ✠
daima.

R/. Ikae na roho yako.

¶ Kwa sauti ya siri.

KRISTO ametolewa kwa ajili yetu, Mwana
Kondoo wetu wa Pasaka, tokea alipozichu-
kua dhambi zetu mwilini mwake katika msalaba ;
kwa kuwa Yeye ndiye Mwana Kondoo wa Mungu,
azichukuaye dhambi za ulimwengu ; kwa hiyo
tuishiriki karamu ya Bwana kwa mioyo safi,
yenye furaha.

¶ Kwa sauti ya kusikika, pamoja na watu.

MWANA Kondoo wa Mungu, uzichukuaye
dhambi za ulimwengu, Uturehemu.

Mwana Kondoo wa Mungu, uzichukuaye
dhambi za ulimwengu, Uturehemu.

Mwana Kondoo wa Mungu, uzichukuaye
dhambi za ulimwengu, Utupe amani yako.

¶ Au, katika Missa ya Wafu.

MWANA Kondoo wa Mungu, uzichukuaye
dhambi za ulimwengu, Uwape raha.

Mwana Kondoo wa Mungu, uzichukuaye
dhambi za ulimwengu, Uwape raha.

Mwana Kondoo wa Mungu, uzichukuaye
dhambi za ulimwengu, Uwape raha ya milele.

¶ Kwa sauti ya siri.

(Isisemwe katika Missa ya Wafu.)

BWANA Yesu Kristo, uliwaambia Mitume
wako, amani nakuachieni, amani yangu
nakupeni : Usitazame dhambi zetu, bali uitaz-
ame imani ya Kanisa lako ; ulijalie amani na
umoja kama vile utakavyo mwenyewe ; Uishiye
na kumiliki, Mungu, milele na milele. Amin.

¶ Katika Missa Kuu, ikiwa wakipeana AMANI,
kwa sauti ndogo.

¶ V. Amani ikae nawe.

R/. Ikae na roho yako.

¶ Kwa sauti ya siri.

BWANA Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hayi, kwa nia ya Baba na kwa uweza wa Roho Mtakatifu, umetupa uzima kwa kufa kwako : Ninakuomba, kwa Mwili na Damu yako takatifu, uniokoe katika dhambi zangu, na katika maovu yote ; unitawale hata niambatane na amri zako ; wala usiniache nitengane nawe : Uishiye na kumiliki pamoja na Yeye, Baba, na Yeye, Roho Mtakatifu, Mungu, daima milele na milele. Amin.

KUUSHIRIKI Mwili wako, Bwana Yesu Kristo, ninaoupokea, nisiyestahili, kusinipatie hukumu mbaya wala adhabu ; bali, kwa pendo lako, kunihifadhi na kuniponya, mwili na roho ; Uishiye na kumiliki pamoja na Mungu Baba, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu; daima milele na milele. Amin.

NITAUPOKEA mkate wa mbinguni : nita-litangaza Jina la Bwana.

¶ Ndipo aseme mara tatu kwa siri,

BWANA, si stahili yangu Wewe uingie chini ya dari yangu ; lakini sema neno tu, na roho yangu itapona.

¶ Apokeapo Ushirika, kwa siri.

MWILI wa Bwana wetu Yesu Kristo unilinde, mwili na roho, hata uzima wa milele.

NIMRUDISHIE Bwana nini kwa ukarimu wake wote alionitendea ? Nitakipokea kikombe cha wokofu, nitalitangaza Jina la Bwana. Nitamwita Bwana astahiliye kusifiwa, nami nitaokoka na adui zangu.

DAMU ya Bwana wetu Yesu Kristo inilinde, mwili na roho, hata uzima wa milele.

¶ Kengele ipigwe mara Kasisi aanzapo kusema, Bwana, si stahili yangu. Ndipo wakiwapo watu wanaotaka kushiriki waje wajipange tayari. Mhudumu aseme, kwa sauti ya taratibu, ya kusikika vema, pamoja na watu,

BWANA, sistahili kuikaribia hii meza yako. Ninakuomba unijalie niile Nyama ya Mwana wako mpendwa Yesu Kristo, na kuinywa Damu yake, ili mwili wangu wenye dhambi usafishwe kwa Mwili wake, na roho yangu kwa Damu yake ya thamani. Kwa Yeye, Kristo Bwana wetu. Amin.

NAUNGAMA kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watakatifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo, na maneno, na matendo ; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Kwa hiyo nawasihi Watakatifu wote waniombee, na wewe, baba, unionbee kwa Bwana Mungu wetu.

¶ Kasisi aelekeane na upande wa waraka na kujibu,

MWENYEZI Mungu akurehemuni, akusameheni makosa yenu, akufikisheni kwenye uzima wa milele. Amin.

BWANA Mwenyezi na mwenye rehema, akujalieni masamaha, ✕ ghofira, na ondoleo la dhambi zenu. Amin.

¶ Kasisi akiwageukia watu tayari kurwafikia aseme,

HUYU ndiye Mwana Kondoo wa Mungu, azichukuaye dhambi za ulimwengu.

Missa

¶ Kasisi aseme kwanza, kisha watu waseme,
kisha Kasisi aseme tena,

BWANA, si stahili yangu Wewe uingie chini
ya dari yangu ; lakini sema neno tu, na roho
yangu itapona.

¶ Akiwashirikisha, aseme,

MWILI wa Bwana wetu Yesu Kristo ukulinde,
mwili na roho, hata uzima wa milele.

DAMU ya Bwana wetu Yesu Kristo ikulinde,
mwili na roho, hata uzima wa milele.

¶ Akivisafisha vyombo, kwa siri.

Utujalie, Bwana, tukipokee kwa nia safi tulichopewa
kinywani ; karama hii tupewayo duniani ituponye hata
milele na milele.

Mwili wako nilioupokea, na Damu yako niliyoinywa,
iambatane nami, Bwana : Unijalie yasisalie mawaa ya
dhambi kwangu, niliyesafika kwa siri zako takatifu, safi.
Uishiye na kumiliki milele na milele. Amin.

¶ Kisha asimame penye kitabu, aisome

AYA YA USHIRIKA

¶ Kisha awakabili watu, aseme,

V. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

¶ Akisimama penye kitabu, aseme,

Tuombe.

SALA ZA MWISHO

¶ Kisha awakabili watu, aseme.

V. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

V. Nendeni zenu kwa amani.

R. Tumshukuru Mungu.

Missa

¶ Au, ikiwa Utukufu una Mungu juu haiku-
semwa, aikabili madhbahu, aseme,

V. Tumhimidi Bwana.

R. Tumshukuru Mungu.

¶ Katika Missa ya Wafu aikabili madhbahu,
aseme,

V. Wastarehe katika amani.

R. Amin.

¶ Ndipo aseme kwa siri.

Ee Ututu Mtakatifu, upende kuikubaliibada yetu : Utujalie,
kwa rehema yako, Sadaka hii tuliyooitoa sisi tuisostahili,
mbele zako Wewe uliye Mtukufu, itufalie sisi na wote tulio-
watolea. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

¶ Kisha awakabili watu, aseme,
(Isisemwe katika Missa ya Wafu.)

BARAKA ya Mwenyezi Mungu, ✕ Baba na
Mwana na Roho Mtakatifu, ikae nanyi daima.
Amin.

¶ Askofu asema kabla ya baraka,

V. Jina la Bwana lihimidiwe.

R. Tangu leo na hata milele.

V. Msaada wetu u katika Jina la Bwana.

R. Aliyezifanya mbingu na nchi.]

¶ Akaende akaisome Injili ya mwisho.

V. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

INJILI YA KAWAIDA

✚ Mwanzo wa Injili takatifu kama ilivyoa-
ndikwa na Yohana Mtakatifu.

R. Atukuzwe Bwana.

MWANZO alikuwako Neno, naye Neno alikuwa-
ko kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.
Huyu mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote

vyalifanyika kwa huyu. Wala pasipo Yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima ; nao uzima ulikuwa nuru ya watu. Nay o nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza.

Palitokea mtu ametumwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yohana. Huyu alikuja kwa ushuhuda, ili aishuhudie nuru, wote wapate kuamini kwa yeye. Huyu hakuwa ile nuru, lakini aishuhudie ile nuru.

Kulikuwako nuru halisi, imtiayo nuru kila mtu ajaye katika ulimwengu. Alikuwako ulimwenguni, ulimwengu umepata kuwa kwa Yeye, wala ulimwengu haukumtambua. Alikuja kwake, nao walio wake hawakumpokea. Bali wote waliompokea aliwapa mamlaka ya kufanyika watoto wa Mungu, ndio waliaminio Jina lake : waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu. (*Piga goti*) Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, (*Simama*) tukautazama utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee akitoka kwa Baba, ameja neema na kweli.

R⁷. Tumshukuru Mungu.

¶ Amri za Ibada hii ya Missa Takatifu zimeandikwa katika Missale, pamoja na karwida zote zimpasazo Kasisi azishike na kuzifuliza, yeye na wahudumu wake.

DIBAJI ZA SIKU NYINGINE

¶ *Dibaji ya Missa ya Wafu.*

Ndio wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.

Kwa Kristo Bwana wetu ; ambaye ndani yake tumeona nuru ya tumaini la ufufuo mtukufu : ili wale wanaohuzunishwa kwa hakika ya kufa wafarijiwe kwa ahadi ya uzima usio mwisho. Kwa maana maisha ya waaminifu wako, Bwana, hayaondolewi bali yabadilika ; na nyumba ya masikani yetu iliyo ya dunia ikiharibiwa tunayo katika mbingu nyumba iliyo ya milele.

Kwa hiyo sisi nasi, pamoja na Malaika na Malaika Wakuu, na jeshi la mbinguni loti pia, twakutukuza na kuliadhimisha Jina lako tukufu; tukikusifu daima, tukisema,

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe, Bwana uliye juu.

Ndiye mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.

¶ *Dibaji ya Siku Kuu ya Kuzaliwa.*

Ndio wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.

Kwa kuwa umetupa Yesu Kristo Mwana wako pekee, azaliwe (kama majira haya) kwa ajili

yetu : Yeye alifanyika Mwanadamu kamili katika utu wa Bikira Mariamu mama yake, kwa uweza wa Roho Mtakatifu ; asipatikane na waa la dhambi liwalo lote, ili atusafishe na dhambi zetu.

Kwa hiyo sisi nasi, pamoja na Malaika na Malaika Wakuu, na jeshi la mbinguni lote pia, twakutukuza na kuliadhimisha Jina lako tukufu ; tukikusifu daima, tukisema,

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe, Bwana uliye juu.

Ndiye mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.

¶ Dibaji ya Siku Kuu ya Ufunuo.

Ndio wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.

Kwa kuwa alipoonekana Mwana wako pekee katika mwili wetu wenye kufa, aliturudishia uzima na nuru yake Yeye aisye kufa.

Kwa hiyo sisi nasi, pamoja na Malaika na Malaika Wakuu, na jeshi la mbinguni lote pia, twakutukuza na kuliadhimisha Jina lako tukufu ; tukikusifu daima, tukisema,

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe, Bwana uliye juu.

Ndiye mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.

¶ Dibaji ya Kwaresima.

Ndio wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.

Wewe, kwa kufunga kwetu, washinda tamaa ndani yetu, wajivutia mioyo yetu, na kutupa nguvu pamoja na ahadi za thawabu yako : kwa Kristo Bwana wetu.

Kwa Yeye sisi nasi, pamoja na Malaika na Malaika Wakuu, na jeshi la mbinguni lote pia, twakutukuza na kuliadhimisha Jina lako tukufu ; tukikusifu daima, tukisema,

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe, Bwana uliye juu.

Ndiye mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.

¶ Dibaji ya Msalaba, ya Wakati wa Mateso.

Ndio wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.

Wewe umetupa wokofu kwa njia ya mti : ili uzima utoke mle ilimotoka mauti : na yeye aliyeshinda penye mti, penye mti ashindike : kwa Kristo Bwana wetu.

Kwa Yeye sisi nasi, pamoja na Malaika na Malaika Wakuu, na jeshi la mbinguni lote pia, twakutukuza na kuliadhimisha Jina lako tukufu ; tukikusifu daima, tukisema,

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana

Missa

Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe, Bwana uliye juu.

Ndiye mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.

¶ Dibaji ya Pasaka.

Ndio wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.

Na zaidi ni wajibu wetu tukusifu kwa ufufuko utukufu wake Mwana wako, Yesu Kristo Bwana wetu : kwa kuwa ndiye Mwana Kondoo wa Pasaka, alitolewa Sadaka kwa ajili yetu, alichukua dhambi za ulimwengu ; kwa kufa kwake ameangamiza kufa, kwa kufufuka kwake ameurejezea tena uzima wa milele.

Kwa hiyo sisi nasi pamoja na Malaika na Malaika Wakuu, na jeshi la mbinguni lote pia, twakutukuza na kuliadhimisha Jina lako tukufu; tukikusifu daima, tukisema,

Mtakatifu, Mtakatifu. Mtakatifu, Bwana Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe, Bwana uliye juu.

Ndiye mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.

¶ Dibaji ya Siku Kuu ya Kupaa.

Ndio wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.

Kwa ajili ya Mwana wako mpendwa, Yesu Kristo Bwana wetu ; aliyeonekana dhahiri na

Missa

Mitume wake wote, baada ya kufufuka kwake, akapaa mbinguni machoni pao, atuandalie mahali ; ili nasi tupae huko aliko, tukamiliki naye katika utukufu.

Kwa hiyo sisi nasi, pamoja na Malaika na Malaika Wakuu, na jeshi la mbinguni lote pia, twakutukuza na kuliadhimisha Jina lako tukufu; tukikusifu daima, tukisema,

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe, Bwana uliye juu.

Ndiye mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.

¶ Dibaji ya Siku Kuu ya Pentekote.

Ndio wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.

Kwa Kristo Bwana wetu. Yeye akipaa juu ya mbingu zote, na kuketi kuumeni pako, aliwamiminia wanawe wateule, (siku ya leo), Roho Mtakatifu kama alivyoahidi.

Kwa hiyo walimwengu wote hufurahi na kushangilia. Hata nao wenye uwezo wa mbinguni, na Malaika wenye mamlaka, hukuimbia na kukutukuza, wakisema bila kukoma,

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe, Bwana uliye juu.

Ndiye mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.

Missa

¶ Dibaji ya Siku Kuu ya Mariamu Mb.

Ndio wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.

Hasa ni wajibu wetu tukusifu, katika Siku Kuu hii ya . . . Mariamu Mbarikiwa, Bikira mtukufu wa daima. Kwa kuwa yeye alimchukua mimba Mwana wako pekee, kwa uweza wa Roho Mtakatifu ; na yeye, aliye hata leo Bikira mtukufu, akatuzalia Nuru ya milele, Yesu Kristo Bwana wetu.

Kwa Yeye sisi nasi, pamoja na Malaika na Malaika Wakuu na jeshi la mbinguni lote pia, twakutukuza na kuliadhimisha Jina lako tukufu ; tukikusifu daima, tukisema,

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe, Bwana uliye juu.

Ndiye mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.

¶ Dibaji ya Siku Kuu ya Mtume au Mtunga Injili.

Ndio wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, Ee Bwana, Mchunga wa milele, tukusihu, usiliache kundi lako ; bali lilindwe na Mitume wako wabarikiwa. Likatawaliwe na mawakili wako waaminifu, uliowaweka juu ya kazi yako, wawe wachungaji wa watu wako.

Kwa hiyo sisi nasi, pamoja na Malaika na Malaika Wakuu, na jeshi la mbinguni lote pia, twakutukuza na kuliadhimisha Jina lako tukufu ; tukikusifu daima, tukisema,

Te Deum

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe, Bwana uliye juu.

Ndiye mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.

UIMBO WA KUSHUKURU

¶ Uimbwe baada ya Missa, au wakati mwininge wo wote.

Te Deum.

1. Wewe, Mungu, twakusifu :
Wewe, Bwana, twakukiri.
2. Wewe Baba wa milele :
Ulimwengu wote unakuabudu.
3. Wewe Malaika zote :
Nazo Mbingu na Nguvu zote.
4. Nao Makerubi na Maserafi :
Wakuimbia hawakomi.
5. Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu :
Bwana Mungu wa majeshi,
6. Mbingu na nchi zimejaa :
Enzi ya Utukufu wako.
7. Wakusifu Wewe :
Jamii tukufu ya Mitume.
8. Wakusifu Wewe :
Shirika lenye sifa la Manabii.
9. Wakusifu Wewe :
Jeshi la Mashahidi waliovaa mavazi meupe.

Te Deum

10. Kanisa Takatifu katika nchi zote :
Lakukiri Wewe.
11. Baba mwenye enzi :
Isiyo na kiasi.
12. Mwana wako pekee :
Wa kweli, wa kuabudiwa.
13. Na Mfariji :
Roho Mtakatifu.
14. Wewe Kristo :
Ndiwe Mfalme wa Utukufu.
15. Wewe Mwana wa milele :
Wa Baba.
16. Wewe ulipotaka kujifanya mtu, ili
umwokoe mwanadamu :
Hukuchukizwa na tumbo lake Bikira.
17. Wewe ulipoushinda uchungu wa mauti :
Uliwafungulia waaminio Ufalme wa
Mbinguni.
18. Wewe unakaa mkono wa kuume wa
Mungu :
Katika utukufu wake Baba.
19. Tunasadiki utakuja :
Kuwa Mwamuzi.
(Piga magoti).
20. Kwa hiyo twakuomba, uwasaidie watu-
mwa wako :
Uliowakomboa kwa damu yako ya
thamani.
(Simama).
21. Uwajalie pamoja na Watakatifu wako :
Utukufu wa milele.

Te Deum

22. Uwaokoe watu wako, Bwana :
Uubariki urithi wako.
23. Uwatawale :
Uwainue hata makao ya milele.
24. Sisi kila siku :
Twakutukuza.
25. Twalisifu Jina lako :
Zamani hizi na za milele.
26. Ukubali, Bwana, kutulinda :
Leo tusitende dhambi.
27. Uturehemu, Bwana :
Uturehemu sisi.
28. Utuonee huruma, Bwana :
Kwa kuwa twakutumaini Wewe.
29. Nimekutumaini Wewe, Bwana :
Nisipotee milele.
30. Umehimidiwa, Bwana, Mungu wa baba
zetu.
R_y. Wastahili kusifiwa na kutukuzwa milele.
V_y. Tumhimidi Baba na Mwana na Roho
Mtakatifu.
R_y. Tumsifu na kumwadhimisha milele.
V_y. Umehimidiwa, Bwana, katika nafasi ya
mbingu.
R_y. Wastahili kusifiwa, kutukuzwa, na kua-
dhimishwa milele.
V_y. Umhimidi Bwana, Ee roho yangu.
R_y. Wala usizisahau fadhili zake zote.
V_y. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.
R_y. Kilio changu kikufikie.
V_y. Bwana akae nanyi.
R_y. Akae na roho yako.

Te Deum

Tuombe.

Ee Mungu, huruma zako hazihesabiki, ukarimu wako hauna kiasi : Tunakushukuru sana kwa yote uliyotujalia; nasi tunakuomba, sisi tuliokarimiwa nawe baraka tulizozimba, tustahili kupewa thawabu za milele. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Mungu, ulifundisha mioyo yao wenye imani kwa nuru ya Roho Mtakatifu : Utujalie kwa Roho huyo tuyajue mambo yote kwa akili ; tuifurahie siku zote faraja yake takatifu.

Ee Mungu, huachi mtu ye yote akutumainiye ateswe kupita kiasi, bali unasikiliza sala zake : Tunakushukuru kwa ajili ya dua zetu ulizozi-kubali ; nasi tunakuomba, sisi tulipokea baraka zako tuondolewe yote yatupingayo. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*



GHOFIRA YA WAFU

¶ Baada ya Missa ya Wafu, Kasisi akipenda, aweza kusema na Sala hii. Bali ikiwapo maiti yake yeye aliyefariki, aseme kama vile ilivyo-andikwa katika Kawaida ya Kuzika.

¶ Ikiwa maiti haipo, na iwekwe jeneza tupu na mishumaa yake kama kawaida.

¶ Missa ikiisha, Kasisi avue kasula yake na manipolo, avae kappa nyeusi. Akaiendee jeneza pamoja na wahudumu wake kama kawaida.

¶ Ndipo aseme, au watu waimbe,

¶ Uniokoe, Ee Bwana, na mauti ya milele kunako siku ile ya hofu :* mbingu na nchi zitakapotikisika : utakapokuja kuuhukumu ulimwengu kwa moto.

R. Uniokoe, Ee Bwana, na mauti ya milele kunako siku ile ya hofu :* mbingu na nchi zitakapotikisika : utakapokuja kuuhukumu ulimwengu kwa moto.

¶ Nimeingia hofu, ninatetemeka :* hata hukumu iwekwe, ghadhabu ikaonekane.

R. Mbingu na nchi* zitakapotikisika :

¶ Siku ile ya ghadhabu, shida, na huzuni :* siku ya uchungu mwangi.

R. Utakapokuja* kuuhukumu ulimwengu kwa moto.

¶ Raha ya milele uwajalie, Ee Bwana :* na nuru ya daima iwaangaze.

R. Uniokoe, Ee Bwana, na mauti ya milele kunako siku ile ya hofu :* mbingu na nchi zitakapotikisika : utakapokuja kuuhukumu ulimwengu kwa moto,

Ghofira ya Wafu

¶ Ndipo Kasisi aubariki uwumba, ainyunyizie jeneza maji matakatifu na kuifukizia kama kawaida.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Baba yetu.

V. Usitutie majoribuni.

R. Lakini utuokoe na maovu.

V. Ee Bwana, uiokoe roho yake.

R. Na milango ya Jehanum.

V. Astarehe katika amani.

R. Amin.

V. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Kilio changu kikufikie.

V. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Tunakuomba, Ee Bwana, uighofiri roho ya mtumishi wako N. umfungulie minyororo ya dhambi zake zote : Ili katika utukufu wa kiyama afufuke ; na kuburudika pamoja na Watakatifu na wateule wako. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

V. Raha ya milele umjalie, Ee Bwana.

R. Na nuru ya daima imwangaze.

Astarehe katika amani.

R. Amin.

Roho yake na roho za waaminifu wote waliofariki kwa rehema ya Mungu wastarehe katika amani.

R. Amin.

Ghofira ya Wafu

¶ Badala ya sala Kasisi aweza kusema hii,

Tunakuomba, Ee Bwana, uighofiri roho ya mtumishi wako N. aliyefariki katika dunia ili akuishie Wewe : Umsamehe yote aliyokukosa kwa udhaifu wake wa ubinadamu ; ukamsafishe kwa huruma zako nyingi. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ Au hii,

Ee Mungu, umewaumba waaminifu wote na kuwaokoa : Uzijalie roho za watumishi na wajakazi wako ondoleo la dhambi zao zote ; wapewe, kwa sala za pendo, masamaha waliyyataka siku zote. Uishiye na kumiliki, Mungu, milele na milele. *Amin.*

¶ Au sala aliyoisema katika Missa, au sala yo yote inayohusu.

¶ Itumike jumla ya umoja au jumla ya wingi katika Ibada hii kama inavyohusika.

¶ Bali marufuku isitumike jumla ya umoja katika Missa ya Wafu, wala katika Sala za Wafu, isipokuwa mahali palipoamriwa.

¶ Kasisi akitumia Ibada hii kwa ajili ya waaminifu wote waliofariki, baada ya Missa ya Kawaida, aseme sala ya tatu katika zile zilizopigwe chapa juu ; bali maneno haya, Roho yake etc. yasisemrwe, aseme,

Wastarehe katika amani.

R. Amin.

Ndio mwisho.





KUSHIRIKISHA WATU PASIPO MISSA

¶ Iwapo watu wanahitaji kupewa Ushirika wakati usio wakati wa Missa, nao wana sababu yenyé maana, warweza kushirikishwa saa yo yote. Ni lazima warwe na hali ya kufunga chakula, yaani, hawajala wala kunywa wala kuvuta tumbako wala kuitafuna, tangu saa sita ya usiku wa manane.

¶ Mhudumu airwashe mishumaa mirwili madhbahuni, na Kasisi, akiisha kunawa mikono, avae kotta na stola nyeupe, achukue bursa na usfunguo wa Kijumba cha Sakramenti, akaende madhbahuni. Aipigie goti Sakramenti, akatandike korporale madhbahuni, akakifungue Kijumba, akapige goti ; kisha akitoe Chombo chenye Sakramenti na kukiweka kati ya korporale, akakiondoe kifuniko chake, akapige goti.

¶ Ndipo Mhudumu na watu waseme,
NAUNGAMA kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watakatifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo, na maneno, na matendo ; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Kwa hiyo nawasihi Watakatifu wote waniombee, na wewe, baba, unionbee kwa Bwana Mungu weṭu,

¶ Kasisi awajibu,

MWENYEZI Mungu akurehemuni, akusameheni makosa yenu, akufikisheni kwenye uzima wa milele. *Amin.*

BWANA Mwenyezi na mwenye rehema, akujali ni masamaha, ✕ ghofira, na ondoleo la dhambi zenu. *Amin.*

¶ Kisha Kasisi apige goti, akitoe *Hostia moja*, akawageukie, akaseme,

HUYU ndiye Mwana Kondoo wa Mungu, azichukua ye dhambi za ulimwengu.

¶ Kasisi aseme kwanza, kisha watu waseme, kisha Kasisi aseme tena,

BWANA, si stahili yangu Wewe uingie chini ya dari yangu ; lakini sema neno tu, na roho yangu itapona.

¶ Akirwashirikisha, aseme,

MWILI wa Bwana wetu Yesu Kristo ukulinde, mwili na roho, hata uzima wa milele.

¶ Kisha, akifika madhbahuni, akiweke Chombo chenye Sakramenti avifikiche juu yake vidole vilivyoigusa *Hostia*, akakifunge, akapige goti. Ndipo avisafishe vidole hivyo kwa maji, yarwe-kwayo tayari, akavifute kwa kileso. Kisha aseme,

Ee Karamu takatifu ! Twampokea Kristo ; twafanya ukumbusho wa mateso yake ; miyo yetu hujazwa neema ; twapewa arabuni ya utukufu ujao.

¶ Uliwapa chakula cha mbinguni.

R;. Ndicho kilicho kitamu.

¶ Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R;. Kilio changu kikufikie.

¶ Bwana akae nanyi.

R;. Akae na roho yako.

Tuombe.

Ee Mungu, umetuachia ukumbusho wa Mateso yako, katika Sakramenti iliyo ya ajabu : Utujalie, tunakusihi, tuziheshimu siri takatifu za Mwili na Damu yako ; ili tuyaone daima ndani yetu mazao ya ukombozi wako. Uishiye na kumiliki pamoja na Mungu Baba, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima milele na milele. *Amin.*

¶ *Kisha akiweke Chombo chenye Sakramenti ndani ya Kijumba, akapige goti, akakifunge Kijumba tena. Kisha awabariki.*

Baraka ya Mwenyezi Mungu, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, ikae nanyi daima. *Amin.*

¶ *Chombo cha maji kiwekwe karibu ya Kijumba siku zote, maji yake yamwagwe na Kasisi katika Pisina mara kwa mara. Bursa lakini, isiwekwe Kanisani ; bali iletre na Kasisi kila itakirapo.*



IBADA YA BARAKA YA SAKRAMENTI MBARIKIWA

¶ *Watu wakionapo Kijumba cha Sakramenti kimefungulirwa, na waimbe,*

*Dhabihu ya wokofu wetu,
Umetufungulia mbingu ;
Adui watusonga sana,
Kwa nguvu utusaidie.*

*Ee Mungu mmoja, Nafsi tatu,
Twakutukuza siku zote ;
Utupe raha ya milele
Katika nchi yetu juu. Amin.*

¶ *Uimbo huu ukimalizika, Kasisi aagize Litania au Uimbo mrwingine ulioruhusawa kwa Ibada hii, au Te Deum, au zisemwe sala zifaazo.*

¶ *Kisha watu waimbe,*
*Siri hii iliyo kubwa
Tuisujudie vema,
Ya zamani yamepita,
Mambo ya torati ile ;
Na yasiyoonekana
Tunaona kwa imani.*

*Utukufu na fahari
Ina Mungu juu ya yote,
Baba, Mwana, naye Roho,
Nafsi tatu, Mungu mmoja ;
Atukuzwe, asifiwe,
Leo, kesho, na milele. Amin.*

Ibada ya Baraka

¶ Kisha Kantor aimbe,
V. Uliwapa chakula cha mbinguni (Haleluya).
R. Ndicho kilicho kitamu (Haleluya).
(Haleluya isiimbwe ila Wakati wa Pasaka na
Siku Kuu ya Mwili Mt.)

¶ Kasisi asimame, akaimbe,
Tuombe.

Ee Mungu, umetuachia ukumbusho wa Mateso yako, katika Sakramenti iliyo ya ajabu : Utujalie, tunakusihi, tuziheshimu siri takatifu za Mwili na Damu yako ; ili tuyaone daima ndani yetu mazao ya ukombozi wako. Uishiye na kumiliki pamoja na Mungu Baba, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima milele na milele. *Amin.*

¶ Ndipo hutolerwa BARAKA.

¶ Mara Kasisi ameondolewa veli ya mabegani, watu waseme baada yake fungu kwa fungu, Mwenyezi Mungu ahimidiwe.

Jina lake takatifu lihimidiwe.

Yesu Kristo, Mungu kweli na Mwanadamu kweli, ahimidiwe.

Jina takatifu la Yesu lihimidiwe.

Moyo wake mtakatifu uhimidiwe.

Yesu Kristo, aliomo katika Sakramenti Takatifu, ahimidiwe.

Roho Mtakatifu, Mfariji, ahimidiwe.

Mama wa Mungu, Mariamu Mtakatifu, asifiwe.

Jina la Mariamu, Bikira na Mama, lisifiwe.

Ahimidiwe Mungu kwa ajili ya Malaika zake na Watakatifu wake. *Amin.*

Kipa Imara

¶ Kisha Sakramenti ifunikwe tena. Huko nyuma watu waimbe,
Ant. Tuiabudu Sakramenti Takatifu : milele na milele.

Zab. 117.

1. Msifuni Bwana, enyi mataifa yote : Mhimidini, enyi watu wote.
2. Maana fadhili zake kwetu sisi ni kuu : Na uaminifu wa Bwana ni wa milele. Utukufu.

Ant. Tuiabudu Sakramenti Takatifu : milele na milele.

¶ Ni halali kuimba Uimbo mwingine.

¶ Ni marufuku Watakatifu wasiimbiwe Litania au Uimbo katika Ibada hii, isipokuwa baada ya Zab. 117.

SAKRAMENTI YA KIPA IMARA

¶ Watakao kupewa Kipa Imara wapangwe tayari, wamepiga magoti, kila mmoja mwenye mdhamini wake amesimama nyuma yake.

¶ Ndipo Askofu awakabili, aseme, Roho Mtakatifu awashukieni, na uweza wake Aliye juu uwalindeni na dhambi. *Amin.*

V. Jina la Bwana lihimidiwe.

R. Tangu leo na hata milele.

V. Msaada wetu u katika Jina la Bwana.

R. Aliyezifanya mbingu na nchi.

V. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Kilio changu kikufikie.

V. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

¶ Ndipo Askofu awaombee, akiwanyoshea mikono yake.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu uishiye milele, ulipenda harwa watumishi wako wazaliwe mara ya pili kwa maji na Roho Mtakatifu, ukarwapa masamaha ya dhambi zao zote : Tunakusihi uwatieve nguvu za Roho Mtakatifu aliye Mfariji ; uwazidhie kila siku karama za neema yako. *Amin.* Roho ya hekima na akili. *Amin.* Roho ya shauri na nguvu za rohoni. *Amin.* Roho ya elimu na utawa. *Amin.* Uwajaze roho ya kicho chako kitakatifu ; leo na siku zote. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Ee Bwana, uwakarimie nguvu zako, ambazo zilimshinda adui wetu ulipoteswa naye na kusulibiwa : *Wakitiwa nasi alama ya msalaba, uwaweke kuwa wako daima ; wakipakwa mafuta usoni, uwajaze Roho Mtakatifu miyoni mwao ; ili waupate uzima wa milele. Uishiye na kumiliki, Mungu, milele na milele.* *Amin.*

¶ *Sasa Askofu amfikiapo kila mmoja, mdhamini wake aweke mkono wake wa kulia juu ya bega lake la kuume yule anayemdhaminia.*

Askofu amtie kila mmoja alama ya msalaba katika paji la uso wake kwa kidole gumba kimechovywa katika mafuta ya Wokofu, aka-mwekee mkono wake kichwani, aseme,

N. nakutia alama ✕ ya msalaba kwa mafuta ya Wokofu, nakuwekea mkono wangu, ufanywe imara na Roho Mtakatifu ; kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Amin.

¶ *Kisha Askofu aseme,*

V. Amani ya Bwana ikae nanyi.

R. Ikae na roho yako.

¶ *Askofu aigeukie madhbahu.*

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, uwalinde watu harwa kwa neema yako ya mbinguni, wadumu kuwa wako milele : *Wakazidi kila siku kupewa Roho yako Mtakatifu ; hata wafike kwenye ufalme wako wa mbinguni. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.*

Mwenyezi Mungu uishiye milele, umetuagiza sisi Maaskofu tuifulize kazi waliopewa Mitume na Bwana wetu Yesu Kristo : *Upende kuwatazama harwa waliopewa uwezo wa Roho Mtakatifu kwa huduma yetu ; mkono wako, Ee Baba, uwe juu yao daima, Roho yako Mtakatifu akae ndani yao siku zote, ili waupate uzima wa milele. Kwa Yeye, Bwana wetu Yesu Kristo Mwana wako : Aishiye na kumiliki pamoja nawe, katika umoja wake Yeye huyu Roho Mtakatifu, Mungu, daima milele na milele.* *Amin.*

Kama vile Mwokozi wetu Kristo alivyotuagiza, akatufundisha, tunathubutu kusema,
Baba yetu.

¶ *Kisha Askofu awakabili waliopewa Kipa Imara, awabariki.*

Akubarikini Mwenyezi Mungu, ✕ Baba na ✕ Mwana na ✕ Roho Mtakatifu. Amin.



KUTANGAZA HABARI ZA NDOA

¶ Kabla ya kuoza watu Kasisi hana budi kutangaza habari zao watakao kuoana, mara tatu, wakati wa Missa, Siku ya Bwana wanapokutanika watu wengi.

¶ Azitangaze habari hivi,

Natangaza habari za Ndoa ya N. wa Mtaa wa N. na N. wa Mtaa wa N. Mtu ye yote, akijua sababu au zuio la haki watu hawa wasiungane katika Ndoa Takatifu, lazima anijulishe. Hii ndiyo mara ya kwanza (au ya pili, au ya tatu), ya kuuliza.

¶ Watu warwili watakaoana wakikaa mitaa mbali mbali, habari zitangazwe katika mitaa yote miwili, wala Kasisi asirwaoze mpaka amekwisha kupata hakika ya kuwa habari zimetangazwa mara tatu katika mtaa mrwingine pia, wala zuio halikuonekana.

¶ Ikiwa watu warwili wameoana kishenzi, wanataka kuitengeneza hali yao, Kasisi na atangaze hivi,

Nawapasheni habari ya kuwa N. na N. waliooana kishenzi, wamelikubali shauri la Kanisa ; basi siku hizi wataozwa Kanisani kwa idhini ya Askofu, Mungu akiwajalia. Hii ndiyo mara ya . . . ya kutangaza.

SAKRAMENTI YA NDOA TAKATIFU

¶ Watu wasiperwe Sakramenti hii ila kwanza wamesailiwa vema na Kasisi maswali yaliyomriwa na Askofu, wakabainika kuwa warweza kuoana kwa halali ; tena wameperwa maonyo na malango ya kuwafaa.

¶ Wakati wa arusi Kasisi asimame Kanisani kuwakabili watakaozwa, wanasimama penye daraja la kupandia sehemu ya mapadre. (Bwana arusi kwa mkono wa kushoto wa Kasisi.)

¶ Ndipo Kasisi aseme,

Akiwapo mtu ye yote auezaye kuonyesha sababu watu hawa wasiungane kwa halali katika Ndoa, aseme sasa, au anyamaze kabisa tokeo leo.

Nawatakeni ninyi wawili, kama mtakavyojibu siku ya hukumu, siri za mioyo yetu zitakapokuwa wazi, mmojawapo wenu akijua zuio lo lote la kuwazuia msiungane kwa halali katika Ndoa, mseme sasa. Kwa maana wote walioungana kwa jinsi isivyoamriwa kwa Neno la Mungu hawaungwi na Mungu ; wala Ndoa yao si halali.

¶ Mtu akitoa sababu wasioane kwa halali, arusi iahirishrwe hata iliyo kweli itakapothubutika.

¶ Zuio lisiponenwa, Kasisi amwulize Mwanamume,

N. unahiari kumchukua mwanamke huyu kuwa mke wako wa arusi, mkae pamoja kama

ilivyoamriwa na Mungu, katika hali takatifu ya ndoa? Utampenda, utamtuliza, utamheshimu, na kumtunza katika ugonjwa na uzima; na usishughulike na wengine, utakaa na huyu peke yake, kadiri mtakavyoishi wote wawili?

¶ *Mwanamume ajibu.*

Ndivyo nitakavyofanya.

¶ *Kisha Kasisi amwulize Mwanamke,*

N. unahiari kumchukua mwanamume huyu kuwa mume wako wa arusi, mkae pamoja kama ilivyoamriwa na Mungu, katika hali takatifu ya ndoa? Utamtii, utamtumikia, utampenda, utamheshimu, na kumtunza katika ugonjwa na uzima: na usishughulike na wengine, utakaa na huyu peke yake kadiri mtakavyoishi wote wawili?

¶ *Mwanamke ajibu,*

Ndivyo nitakavyofanya.

¶ *Kisha Kasisi aseme,*

Nani aliyemleta mwanamke huyu aolewe na mwanamume huyu?

¶ *Kisha wapeane yamini hivi. Kasisi akimpokea Mwanamke katika mikono ya baba yake, au wakili wa baba yake, amshikishe Mwanamume kwa mkono wake wa kuume mkono wa kuume wa Mwanamke; na amsemeshe hivi,*

Mimi N. nahiari kukuchukua wewe N. kuwa mke wangu wa arusi, niwe nawe tangu leo hivi na baadaye, katika mema na mabaya, katika utajiri na umasikini, katika ugonjwa na uzima, nikupende, nikutunze, hata kufa, kwa amri takatifu ya Mungu; na kwa hiyo nakupa yamini yangu.

¶ *Kisha waachane mikono; na Mwanamke kwa mkono wake wa kuume amshike Mwanamume kwa mkono wake wa kuume; na Kasisi amsemeshe hivi,*

Mimi N. nahiari kukuchukua wewe N. kuwa mume wangu wa arusi, niwe nawe tangu leo hivi na baadaye, katika mema na mabaya, katika utajiri na umasikini, katika ugonjwa na uzima, nikupende, nikutunze, nikutii hata kufa, kwa amri takatifu ya Mungu; na kwa hiyo nakupa yamini yangu.

¶ *Kisha waachane mikono; na Mwanamume ampe Mwanamke Pete, akiirweka jiuu ya kitabu pamoja na sadaka yake ya Kanisa. Kasisi aibariki Pete hivi,*

¶ V. Msada wetu u katika Jina la Bwana.

R. Aliyezifanya mbingu na nchi.

V. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Kilio changu kikufikie.

V. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Bwana, tunakuomba uibariki ✕ Pete hii tuibarikiyo kwa Jina lako: umjalie huyu mtumishi wako atakayeivaa akae na mumewe kwa uaminifu, wapendane hata kufa. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ *Kisha Pete inyonyiziwe maji matakatifu. Ndipo Kasisi akiitwaa Pete, ampe Mwanamume, ili aitie katika kidole chanda cha mkono wa kushoto wa Mwanamke. Na Mwanamume akiishika Pete kidoleni, Kasisi amsemeshe hivi,*

Ndoa

Kwa Pete hii nakuoa, kwa mwili wangu nakuheshimu, mali yangu yote ya duniani nakushirikisha : Kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. Amin.

¶ Maneno hayo yote ya Mwanamume na Mwanamke yafasiriwe kwa lugha yao wenyerewe, isipokuwa wanaelerwa na Kiswahili.

¶ Kisha, Mwanamume akiiacha Pete katika kidole cha Mwanamke, wapige magoti wote warili ; na Kasisi aseme,

Tuombe.

Mungu wa milele, Muumba watu wote na kuwahifadhi, Mtoa neema yote ya rohoni, Asili ya uzima wa milele : Uwajalie hawa watumishi wako msaada wako, mwanamume huyu na mwanamke huyu, tunaowaoza kwa Jina lako ; ili wayatimize maagano waliyoagana, (kwa dalili ya pete hii,) wakae pamoja daima katika kupendana na amani kamilifu, wakizifuata sheria zako. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

¶ Kisha Kasisi awashikishe mikono yao ya kuume, aseme,

Mungu aliowaunganisha mwanadamu asi-watenganishe.

¶ Kisha awaambie watu,

Kwa sababu N. na N. wamekubaliana katika Ndoa takatifu, wakakiri haya mbele za Mungu na mbele ya makutano haya, kwa kupeana yamini na kuahidiana, wakaonyesha haya kwa kutoa Pete na kwa kuipokea, na kwa kushikana mikono : Nawanena kuwa Mume na Mkewe, kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. Amin.

Ndoa

¶ Ndipo Kasisi awabariki.

Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu, akubarikini, akuhifadhini, akulindeni : Bwana akuangalieni kwa rehema na upendeleo wake ; akujazeni na wingi wa baraka ya rohoni na neema, mkae pamoja katika maisha haya, kwa jinsi mpate, katika ulimwengu ujao, kupewa uzima wa milele. Amin.

¶ Kisha, wakiendea kunako Meza ya Bwana, isemwe au iimbre Zaburi hii ifuatayo.

Ant. Mcha Mungu.

Zab. 128.

1. Yu heri kila mtu amchaye Bwana :
Aendaye katika njia yake.
2. Taabu ya mikono yako hakika utaila :
Utakuwa heri na kwema kwako.
3. Mke wako atakuwa kama mzabibu uzaao :
Vyumbani mwa nyumba yako.
4. Wanawo kama miche ya mizeituni :
Wakizunguka meza yako.
5. Hivyo ndivyo atakavyobarikiwa :
Mtu yule amchaye Bwana.
6. Bwana akubariki toka Sayuni :
Upate kuuona uheri wa Yerusalem.
7. Siku zote za maisha yako :
Naam, ukawaone wana wa wanawo.
Utukufu.

Ant. Mcha Mungu ndiye aliye heri : Amani ikae na Israeli.

¶ Au hii, ikirewa mwanamke hana tumaini la kuzaa watoto.

Ant. Njia yako.

Zab. 67.

1. Mungu atufadhili na kutubariki :
Na kutuangazia uso wake.
2. Njia yako ijulike duniani :
Wokofu wako kati ya mataifa yote.
3. Watu na wakushukuru, Ee Mungu :
Watu wote wakushukuru.
4. Mataifa na wafurahi :
Naam waimbe kwa furaha.
5. Maana utawahukumu watu kwa haki :
Na kuwaongoza watu walioko duniani.
6. Watu na wakushukuru, Ee Mungu :
Watu wote wakushukuru.
7. Nchi imetoa mazao yake :
Mungu, Mungu wetu, atatubariki.
8. Mungu atatubariki :
Ncha zote za dunia zitamcha Yeye.
Utukufu.

Ant. Njia yako ijulike duniani : wokofu wako kati ya mataifa yote.

¶ Zaburi ikiisha, Mwanamume na Mwanamke wapige magoti mbele ya madhbahu, na Kasisi aanze mara kutoa Missa. La ! hakuna Missa, Kasisi asimame madhbahuni, akarwakabili, aseme,

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Baba yetu.

¶. Ee Bwana, uwaokoe hawa watumishi wako.

R. Wanaokutumaini Wewe.

¶. Ee Bwana, uwapelekee msaada toka patakatifu pako.

R. Na kuwategemeza toka Sayuni.

¶. Ee Bwana, uwe kwao ngome yenyen guvu.

R. Adui asiwapate.

¶. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Kilio changu kikufikie.

¶. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

(1) Mwenyezi Mungu, tunakuomba uwabariki hawa watoto wako, upande mbegu za uzima wa milele miyoni mwao : ili yote watakayo-jifunza kwa Neno lako takatifu, wayatimize kwa matendo yao. Uwaangalie kwa rehema, Ee Bwana, kutoka mbinguni, uwabariki ; ili, kwa kutii mapenzi yako, na kukaa salama chini ya hamaya yako, wapate kudumu katika pendo lako hata mwisho wa maisha yao. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

¶ (Sala hii ifuatayo isisemwe, ikirewa Mwanamke amepita wakati wa kuzaa watoto.)

(2) Bwana wa rehema, Baba wa mbinguni, kwa ukarimu wako watu waongezeka : Tunakusihi uwajalie watu hawa wawili, kwa baraka

Ndoa

yako, wapate kuzaa watoto na kukaa pamoja katika upendano na amani, hata kuwaona watoto wao wamelelewa Kikristo na kwa adili, kwa sifa na heshima yako. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

(3) Mwenyezi Mungu, umependa kuitakasa Ndoa kuwa siri bora, kwa mfano wa ndoa ya rohoni na umoja wa Kristo na Kanisa lake : Uwaangalie kwa rehema hawa watumishi wako, mume huyu ampende mke wake, akifuata Neno lako ; kama Kristo alivyolipenda Kanisa lake, akajitoa kwa ajili yake, akilitunza kama mwili wake mwenyewe ; na mke huyu ampende mume wake, ampendeze, na kuwa amini, na kumtii ; na katika upole, kiasi, na amani, awafuate wanawake walio wema, watawa. Ee Bwana, uwabariki wote wawili, uwajalie kuarithi ufalme wako wa milele. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ *Ndipo Kasisi awabariki.*

(4) Mwenyezi Mungu, aliyeaumba wazee wetu wa kwanza, Adamu na Hawa, akawatakasa na kuwaunga katika ndoa : Akumwagieni wingi wa neema yake, akutakaseni, akubarikini, mmpendeze mwili na roho ; mkakae pamoja katika upendano utakatifu hata mwisho wa maisha yenu. *Amin.*

¶ *Ndipo Kasisi awanyunyizie maji matakatifu.*

¶ *Ikiwapo Missa ya Arusi, Kasisi aseme yote kama kawaida mpaka Zab. 128.*

Wakati wanapoimba Zab. 128 ndipo Kasisi aende akavae mavazi yake ya Missa.

Ndoa

Mara wakiisha kuimba Zab. 128 Kasisi aanze Missa, akaendelee kutoa Missa kama kawaida mpaka mwisho wa Baba yetu.

Wakiisha kuimba Baba yetu Kasisi aseme sala tatu,

- (1) Mwenyezi Mungu, tunakuomba.
- (2) Bwana wa rehema.
- (3) Mwenyezi Mungu, umependa.

Ndipo hufuata Utuokoe, na masilio ya sala za Missa kama kawaida.

Kabla hajatoa Baraka ya Missa, Kasisi awabariki walioozwa, (4) Mwenyezi Mungu, aliyeaumba. Kisha awape maonyo, awanyunyizie maji matakatifu.

Ndipo hufuata sala, Ee Utatu Mtakatifu, na Kasisi akaimalize Missa kama kawaida.

¶ *Watu waliooana, wakiwa washiriki, ni wajibu wao waupokee Ushirika Utakatifu siku ile ile ya arusi, au mara wapatapo wasaa baadaye.*

ARUSI YA MKRISTO NA MWANAFUNZI

¶ *Ikiwapo arusi ya Mkristo na Mwanafunzi, sala zote na zisemwe mahali wakaapo Wanafunzi kwa kawaida.*

Aidha, Kasisi akiisha kusema maneno haya, Nawanena kuwa Mume na Mkewe, kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Amin., mara aendelee hivi.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, tunakuomba uwasaide hawa waoto wako, upande mbegu za uzima

wa milele miyoni mwao : ili yote watakayo-jifunza kwa Neno lako takatifu, wayatimize kwa matendo yao. Uwaangalie kwa rehema, Ee Bwana, kutoka mbinguni, uwasaidie ; ili, kwa kutii mapenzi yako, na kukaa salama chini ya hamaya yako, wapate kudumu katika pendo lako hata mwisho wa maisha yao. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Bwana wa rehema, Baba wa mbinguni, kwa ukarimu wako watu waongezeka : Tunakusihii uwajalie watu hawa wawili, kwa msaada wako, wapate kuzaa watoto na kukaa pamoja katika upendano na amani, hata kuwaona watoto wao wamelelewa Kikristo na kwa adili, kwa sifa na heshima yako. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Msaada wa Mungu ukae nanyi daima. *Amin.*

¶ *Aidha, katika hawa warwili waliooana, atakapobatizwa yule aliye kuruwa Mwanafunzi, ni desturi njema wafike Kanisani, ili Kasisi aibariki arusi yao.*

¶ *Wote warwili wapige magoti mbele ya madhbahu, na Kasisi asimame madhbahuni, akawakabili, aseme,*

¶. Msaada wetu u katika Jina la Bwana.

R. Aliyezifanya mbingu na nchi.

¶. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Kilio changu kikufikie.

¶. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Bwana, tunakuomba uibariki ✕ Pete hii tuibarikiyo kwa Jina lako : umjalie huyu mtumishi wako anayeivaa akae na mumewe kwa uaminifu ; wapendane hata kufa. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ *Ndipo Kasisi awabariki.*

Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu, akubarikini, akuhifadhini, akulindeni : Bwana akuangalieni kwa rehema na upendeleo wake ; akujazeni na wingi wa baraka ya rohoni na neema, mkae pamoja katika maisha haya, kwa jinsi mpate, katika ulimwengu ujao, kupewa uzima wa milele. *Amin.*

¶ *Kisha isemwe Zaburi hii ifuatayo.*

Ant. Mcha Mungu.

Zab. 128.

1. Yu heri kila mtu amchaye Bwana :
Aendaye katika njia yake.
2. Taabu ya mikono yako hakika utaila :
Utakuwa heri na kwema kwako.
3. Mke wako atakuwa kama mzabibu uzaao :
Vyumbani mwa nyumba yako.
4. Wanawo kama miche ya mizeituni :
Wakizunguka meza yako.
5. Hivyo ndivyo atakavyobarikiwa :
Mtu yule amchaye Bwana.
6. Bwana akubariki toka Sayuni :
Upate kuuona uheri wa Yerusalem.
7. Siku zote za maisha yako :
Naam, ukawaone wana wa wanawo.
Utukufu.

Ant. Mcha Mungu ndiye aliye heri : Amani ikae na Israeli.

Bwana, uturehemu.
 Bwana, uturehemu.
 Kristo, uturehemu.
 Kristo, uturehemu.
 Bwana, uturehemu.
 Bwana, uturehemu.
 Baba yetu.
 V. Ee Bwana, uwaokoe hawa watumishi wako.
 R. Wanaokutumaini Wewe.
 V. Ee Bwana, uwapelekee msaada toka patakatifu pako.
 R. Na kuwategemeza toka Sayuni.
 V. Ee Bwana, uwe kwao ngome yenye nguvu.
 R. Adui asiwapate.
 V. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.
 R. Kilio changu kikufikie.
 V. Bwana akae nanyi.
 R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, umependa kuitakasa Ndoa kuwa siri bora, kwa mfano wa ndoa ya rohoni na umoja wa Kristo na Kanisa lake : Uwaangalie kwa rehema hawa watumishi wako, mume huyu ampende mke wake, akifuata Neno lako ; kama Kristo alivyolipenda Kanisa lake, akajitoa kwa ajili yake, akilitunza kama mwili wake mwenyewe ; na mke huyu ampende mume wake, ampende, na kuwa amini, na kumtii ; na katika upole, kiasi na amani, awafuate wanawake walio wema, watawa. Ee Bwana, uwabariki wote wawili uwajalie kuu-ri thi ufalme wako wa milele. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ Ndipo Kasisi awabariki.

Mwenyezi Mungu, aliye wa umba wazee wetu wa kwanza, Adamu na Hawa, akawatakasa na kuwaunga katika ndoa : Akumwagieni wingi wa neema yake, akutakaseni, akubarikini, mmpendeze mwili na roho ; mkakae pamoja katika upendano utakatifu hata mwisho wa maisha yenu. *Amin.*

¶ Ndipo Kasisi awanyunyizie maji metakatifu.

¶ Watu warili wakiwa wameoana zamani, halafu wakabatizwa, Ndoa yao isidhaniwe kamwe kuwa si Ndoa ya halali ; walakin, wasikose kufika Kanisani ili Kasisi aibariki Ndoa yao kama vile ilivyoandikwa juu, wakiisha kubatizwa wote warili. Tena yafaa sana mume ampatie mkerwe pete, nayo ibarikiwe kama ilivyoandikwa juu.

KITUBIO CHA KANISA**KUMPA MTU KITUBIO**

¶ Mtenda dhambi ya wazi, amekwisha kuitwa na Padre wake kwa faragha, na kukubali maonyo yake na kitubio atakachopewa, Padre na amwite mbele ya Wakristo waliopo Siku ya Bwana ifuatayo ; na wakati wa Missa, kabla hajararu-husu Wanafunzi, amkaribishe na kukitangaza kitubio chake.

Nakuarifuni ya kuwa huyu ndugu yetu N. aliyetenda dhambi ya wazi, ameku ja mwenye nia ya kutubu na kujitakia kitubio.

Mwanangu, nakukaribisha katika cheo cha wenye kitubio kwa muda wa . . .

Mwenyezi Mungu akusaidie uzidi kutubu kwa kweli, upate kutimiza kitubio chako kwa utukufu wake na faida ya roho yako.

¶ Ndipo amwonyeshe mahali pake pa kukaa Kanisani ; na siku ile ile, Padre akiwaruhusu wenyewe kitubio cha Kanisa, huyu aondoke pamoja nao.

KUMRUDISHA MWENYE KITUBIO

¶ Mwenye kitubio akiwa karibu ya kutimiza kitubio chake alichopewa, Padre na atangaze kwanza ya kwamba ana kusudi la kumrudisha.

Natangaza ya kuwa ndugu yetu N. aliyepewa kitubio cha Kanisa amezitimiza siku zake. Basi nakusudia kumrudisha baada ya siku si nyangi. Akiwapo mtu ye yote ajuaye ya kwamba hana haki ya kurudishwa bado, na aje kunipasha habari.

¶ Zui o lisiponenwa na mtu, Padre na amrudishe Siku ya Bwana ifuatayo, wakati wa Missa, kabla hajawaruhusu Wanafunzi.

¶ Padre na aketi juu ya kiti, kati kati wakaapo Wanafunzi, amevaa kofla yake na kuipa kisogo madhbahu ; mbele yake mwenye kitubio apige magoti, aseme,

Naungama kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watkatifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo na maneno na matendo ; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Zaidi naungama ya kwamba nalitenda dhambi ya . . .

Kwa dhambi hii, na nyinezo zote, nasikitika sana ; nataka kuziacha ; naomba ghofira ya wazi na ruhusa ya kushiriki.

¶ Ndipo Padre aseme,

Bwana wetu Yesu Kristo kwa rehema zake nyangi akusamehe makosa yako ; na kwa amri yake niliyopewa mimi nakughofiri dhambi zako zote, kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Amin.

Baraka ya Mwenyezi Mungu, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, ikae nawe daima. Amin.

¶ Kisha amweke pamoja na Wakristo tena ; na, akiikibili madhbahu amevua kofla yake, awaongoze Wakristo wote waliope ramshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake, aseme,

¶ Utukufu una Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Ry Ulivyokuwa mwanzo, ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. Amin.

KUMTENGA ALIYEKATAA KUTUBU

¶ Padre harwezi kumtenga mtu bila kupewa idhini ya Askofu.

¶ Ni heri kila mtu aliye na haki ya kutengwa aonywe kwanza Kanisani, hivi,

Nawajulisheni ya kuwa N. ametenda dhambi ya wazi, asikubali kuitubia dhambi yake. Kwa hiyo nakusihini tumwombee sana asizidi kuendelea katika ukaidi wake, asije akaingia katika hatari kubwa ya kutengwa na Kanisa la Mungu.

¶ Wala Padre asimtenge mpaka miezi sita imekwisha kupita. Ndipo aitangaze habari hivi,

Kwa kuwa N. ametenda dhambi ya wazi akaataa kuitubia dhambi yake na kuiacha ; natangaza ya kuwa ametengwa na Kanisa la Mungu, hata aje mwenyewe kujitakia kitubio na rehema.

¶ Padre akiisha kumtenga mtu ye yote, ni wajibu wake kumwarifu Askofu habari hii na sababu yake, kabla hazijapita siku arobatashara tangu mwenye dhambi alipotengwa.

¶ Aidha, na aweke Kanisani, karibu na mlango, karatasi iliyandikwa majina ya wote waliochengwa katika Mtaa wake.

KUMRUDISHA ALIYETENGWA

¶ Padre aweza kumpa kitubio mara amwonapo analo toba la kweli.

¶ Bali aliyetengwa yu katika mamlaka na hukumu ya Askofu mwenyerwe, wala Padre asithubutu kumghofiri aliyetengwa, wala kumrudisha, kabla hajamwarifu Askofu na kupewa idhini yake.

¶ Padre na afanye hivi,

(1) Ampe kitubio kama kawaida.

(2) Atangaze ya kuwa amezitimiza siku zake kama kawaida.

(3) Akiisha kupewa idhini ya Askofu, wala zuio lisiponenwa na mtu, Padre na amrudisha Siku ya Bwana ifuatayo, wakati wa Missa, kabla hajawaruhusu Wanafunzi.

¶ Padre na aketi juu ya kiti, kati kati, bali chini karibu na mlango wa Kanisa, amevaa kofia yake na kuipa kisogo madhbahu; mbele yake yule aliyetengwa apige magoti, aseme,

Naungama kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watkatifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo na maneno na matendo; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Zaidi naungama ya kwamba nalitenda dhambi ya . . .

Kwa dhambi hii, na nyinginezo zote, nasikitika sana; nataka kuziacha; naomba ghofira ya wazi, kufunguliwa kifungo nilichofungiwa, na ruhusa ya kushiriki.

¶ Ndipo Padre aseme,

Bwana wetu Yesu Kristo kwa rehema zake nyingi akusamehe makosa yako; na kwa amri yake niliyopewa mimi nakughofiri dhambi zako zote, kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Amin.

Kwa idhini ya Bwana Askofu nakufungulia kifungo ulichofungiwa kwa amri ya Kanisa; nakurudisha katika kundi la Wakristo waaminifu; kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Amin.

Baraka ya Mwenyezi Mungu, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, ikae nawe daima. Amin.

¶ Kisha amweke pamoja na Wakristo tena; na, akiikabili madhbahu amevua kofia yake, awaongoze Wakristo wote waliopo wamshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake, aseme,

¶ Utukufu una Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Ry. Ulivyokuwa mwanzo, ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. Amin.



SAKRAMENTI YA TOBA

¶ *Kasisi aseme,*

Bwana awemo moyoni mwako na midomoni mwako, upate kuungama vema dhambi zako zote, kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

¶ *Mwenye toba aungame hivi,*

Naungama kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watakatifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo na maneno na matendo ; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Na tangu nilipoungama na kupata ghofira, . . . , dhambi zangu ninazofahamu ndizo hizi . . .

Kwa dhambi hizi, na nyinginezo nisizofahamu, nasikitika sana ; nataka kuziacha ; naomba ghofira kwa Mungu, na kwako, baba, nataka kitubio.

¶ *Ndipo Kasisi amshauri, ampe kitubio, akamghofiri.*

Bwana wetu Yesu Kristo *(aliyeacha katika Kanisa lake uwezo wa kuwaghofiri watu wote wenye dhambi wanaotubu kwa moyo na kumwamini Yeye) kwa rehema zake nyingi akusamehe makosa yako ; na kwa amri yake niliyopewa mimi nakughofiri dhambi zako zote, kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

Baraka ya Mwenyezi Mungu, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, ikae nawe daima. *Amin.*

* maneno hayo katika vifungo yawera kuachwa.

USHIRIKA WA MGONJWA

¶ *Kasisi, akiisha kunawa mikono, avae kotta na stola nyeupe, achukue bursa na ufunguo na Kibweta cha kuchukulia Sakramenti, akaende madhbahuni. Aipigie goti Sakramenti, akatandike korporale madhbahuni na kukiweka Kibweta juu yake wazi, akakifungue Kijumba, akapige goti ; kisha akitoe Chombo chenyé Sakramenti na kukiweka kati ya korporale, [akakiondoe kifuniko chake, akapige goti.*

¶ *Kisha atoe Hostia, moja kwa kila mgonjwa atakayeshirikishwa, na kutia katika Kibweta, na kukifunga. Avisafishe vidole vyake kwa maji yarwekwayo tayari, akavifute kwa kilesö ; akakifunge Chombo chenyé Sakramenti, akakirudishe Kijumbani, akakifunge Kijumba, akapige goti.*

¶ *Kisha akitie Kibweta katika mfuko wake wa hariri, kigwe cha mfuko huo akakitie shingoni, akavue kotta yake na stola, akautie mfuko chini ya kassoki yake, akaende zake nyumbani kwa mgonjwa ; akifuatana na Mhudumu (asiyevalia) wa kumchukulia kotta na stola na kitabu na vyo vyote atakavyo kwa huduma yake.*

¶ *Iwapo mgonjwa anakaa karibu na Kanisa Kasisi, akiona vema, asiutie mfuko chini ya kassoki, wala asivue kotta. Bali aushike mfuko unaoning'inia shingoni kwa mikono yake ; Mhudumu amtangulie amevaa nguo za Kanisani, achukua mshumaa mkononi na kengele ya kuonya watu. Nao rwakienda watu waionao Sakramenti wapige magoti mpaka ipite.*

Ushirika wa Mgonjwa

¶ Kasisi anapoingia chumbani aseme,
V. Amani iwe nyumbani humu.

R. Na kwa watu wote wakao ndani yake.

¶ Akipenda areza kunyunyiza maji matakatifu, kama ilivyoamrirwa. (uk. 116.)

¶ Kisha, ikiwa mgonjwa hajaungama, na aungamishwe kama kawaida.

¶ Kisha, Mhudumu na mgonjwa waseme, Naungama kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watakatifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo, na maneno na matendo ; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Kwa hiyo nawasihi Watakatifu wote waniombee, na wewe, baba, unionbee kwa Bwana Mungu wetu.

¶ Kasisi amjibu,

Mwenyezi Mungu akurehemu, akusamehe makosa yako, akufikishe kwenye uzima wa milele. *Amin.*

Bwana Mwenyezi na mwenye rehema, akujalie masamaha, ✕ ghofira na ondoleo la dhambi zako. *Amin.*

¶ Kisha Kasisi apige goti, akaitwae Hostia, akamrwonyeshe mgonjwa, akaseme,

Huyu ndiye Mwana Kondoo wa Mungu, azichukuaye dhambi za ulimwengu.

¶ Kisha aseme mara tatu,

Bwana, si stahili yangu Wewe uingie chini ya dari yangu ; lakini sema neno tu, na roho yangu itapona.

¶ Akimshirikisha, aseme,

Mwili wa Bwana wetu Yesu Kristo ukulinde, mwili na roho, hata uzima wa milele.

Ushirika wa Mgonjwa

¶ Mgonjwa akidhaniwa kuwa kufani, anaposhirikishwa Ushirika wake wa mvisho Kasisi aseme hivi,

Pokea ndugu, chakula hiki cha safari yako, Mwili wa Bwana wetu Yesu Kristo : kikulinde na adui mwovu na kukufikisha kwenye uzima wa milele.

¶ Kisha Kasisi avisafishe vidole vyake kwa maji, akavifute kwa kiles. Kisha aseme,

Tuombe.

Kama vile Mwokozi wetu Kristo alivyotu-agiza, akatufundisha, tunathubutu kusema, Baba yetu.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, Baba wa mbinguni, tunakushukuru sana kwa kuwa umetulisha chakula hiki cha rohoni, Mwili wa Mwana wako Yesu Kristo na Damu yake : Tunakuomba, utuongezee neema yako ; ili tuyatende yote uliyotumuru. Kwa Yeye. Aishiye.

¶ Au sala hii, mgonjwa akiwa karibu ya kufa.

Mwenyezi Mungu, Baba wa mbinguni, tunakushukuru sana kwa kuwa umemlisha huyu ndugu yetu chakula hiki cha rohoni, Mwili wa Mwana wako Yesu Kristo na Damu yake : Tunakuomba, umjalie aende kwa nguvu ya chakula hicho hata akuone katika utukufu wako. Kwa Yeye. Aishiye.

Baraka ya Mwenyezi Mungu, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, ikae nawe daima. *Amin.*

¶ Maji aliyonarvia vidole vyake yamwagwe motoni mle nyumbani, au katika ardhi nje.

Ushirika wa Mgonjwa

¶ Kasisi aangalie sana Hostia aichukuayo kwa mgonjwa iwe nzima, makombo yasisalie Kibretani. Yakisalia, akirudishe Kibweta Kanisani, na kukirweka Kijumbani, mpaka atoapo Missa tena.

Wakati wa Missa, akisafishapo Kikombe cha Missa, akitoe Kibweta Kijumbani, ayatie makombo katika Kikombe kwa kidole chake, akaitilie Kibweta divai kidogo akaimimine katika Kikombe, kisha akitilie Kibweta divai kidogo sana na maji mengi kidogo, akayamimine, katika Kikombe, akakifute Kibweta kwa kilesu cha Kikombe.

¶ Bali, ikiwa akihitaji Kibweta tena kabla ya Missa kutolerwa, aweza kuyatia makombo yake katika Chombo chenye Sakramenti Kijumbani kwa kidole chake, na kuzidi kukisafisha kwa kidole tu. Kisha avisafishe vidole kwa maji yarwekwayo karibu ya Kijumba. Mwisho wa maji hayo ndio kumwagwa katika pisina.

¶ Sakramenti ya Damu ya thamani ya Bwana wetu isiwewewe, sembuse kuchukulirwa nje ya Patakatifu.

¶ Kasisi akiichukua Sakramenti njiani, wajibu wake ni kusema Sala na Zaburi.

¶ Kasisi, akiisha kuweka Sakramenti Kijumbani aseme,

Ee Karamu takatifu ! Twampokea Kristo ; twafanya ukumbusho wa mateso yake ; mioyo yetu hujazwa neema ; twapewa arabuni ya utukufu ujao.

¶ Uliwapa chakula cha mbinguni.

Ry. Ndicho kilicho kitamu.

Kupakwa Mafuta

¶ Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

Ry. Kilio changu kikufikie.

¶ Bwana akae nanyi.

Ry. Akae na roho yako.

Tuombe.

Ee Mungu, umetuachia ukumbusho wa Mateso yako katika Sakramenti iliyo ya ajabu : Utujalie, tunakusihii, tuziheshimu siri takatifu za Mwili na Damu yako ; ili tuyalone daima ndani yetu mazao ya ukombozi wako. Uishiye na kumiliki pamoja na Mungu Baba, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima milele na milele. Amin.

SAKRAMENTI YA KUPAKWA MAFUTA

¶ Nafasi ikitosha, mgonjwa apewe Ghofira na Ushirika Ut. kabla ya Kupakwa mafuta. (tazama uk. 121.) Lakini si lazima.

¶ Sakramenti hii asipewe mtu asiyeanza kuzitubia dhambi zake, wala asiyebatizwa, wala aliyeharimishwa, wala mtoto asiyepeata umri wa miaka saba, wala mwenye wazimu mwenye hatari ya kufanya matata apakwapo.

¶ Mwenye haki ya kupakwaaweza kupakwa ijapokuwa amezimia au kurukiwa na akili, iwapo Kasisi anajua ya kwamba apenda kupakwa.

Kupakwa Mafuta

¶ Kasisi anapoingia chumbani aseme,
V. Amani iwe nyumbani humu.
R. Na kwa watu wote wakaaō ndani yake.

¶ Nafasi ikitosha, Kasisi ampe mgonjwa msalaba ili aibusu ; akamnyunyizie maji matakatifu ; kisha akawanyunyizie watu wanaohudhuria na chumba chote, akisema,

Ant. Unisafishe, Ee Bwana, kwa husopo, nami nitakuwa safi : unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko thuluji.

Zab. Unirehemu, Ee Mungu : kwa kadiri ya fadhili zako.

Utukufu.

Ant. Unisafishe.

V. Msaada wetu ✕ u katika Jina la Bwana.

R. Aliyezifanya mbingu na nchi.

V. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Kilio changu kikufikie.

V. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Utusikie, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele : Ukubali kumtuma Malaika wako mtakatifu kutoka mbinguni awajie wote wakaaō nyumbani humu ; awahifadhi, awaburidishe, awaponye na kuwalinda. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

¶ Ikiwa nafasi haitoshi, sala hizo zote zisise-mrwe.

¶ Kisha, ikiwa mgonjwa hajaungama, na angamishwe kama kawaida.

Kupakwa Mafuta

¶ Kisha Mhudumu na mgonjwa waseme, Naungama kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watakatifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo, na maneno na matendo ; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Kwa hiyo nawasihi Watakatifu wote waniombee, na wewe, baba, unionbee kwa Bwana Mungu wetu.

¶ Kasisi amjibu,

Mwenyezi Mungu akurehemu, akusamehe makosa yako, akufikishe kwenye uzima wa milele. Amin.

Bwana Mwenyezi na mwenye rehema, akujalie masamaha, ✕ ghofira na ondoleo la dhambi zako. Amin.

¶ Kisha, arwaagize wanaohudhuria wazidi kumwombea mgonjwa wakati anapopakwa, akiwaonya dua zifaazo kuzitoa.

¶ Kisha aseme,

Kwa Jina la ✕ Baba, na ✕ Mwana, na ✕ Roho Mtakatifu, nguvu yote ya Shetani ikomeshwe ndani yako kwa kuweka mikono yetu juu yako, na kwa maombezi ya Malaika na Malaika Wakuu, na Babu na Manabii, na Mashahidi na Waungamaji, na Mabikira, na Watakatifu wote. Amin.

¶ Kisha amtie mgonjwa alama ya msalaba kwa kidole gumba kimechovywa katika mafuta ya Wagonjwa, akisema maneno yaamriwayo chini.

Katika macho (yamefumbwa)

✕ Kwa kupakwa huku, na kwa rehema yake kuu, Bwana akusamehe yote uliyokosa kwa kutazama. Amin.

Kupakwa Mafuta

Katika masikio

¶ Kwa kupakwa huku, na kwa rehema yake kuu, Bwana akusamehe yote uliyokosa kwa kusikia. Amin.

Katika pua

¶ Kwa kupakwa huku, na kwa rehema yake kuu, Bwana akusamehe yote uliyokosa kwa kunusa. Amin.

Katika midomo (imefumbwa)

¶ Kwa kupakwa huku, na kwa rehema yake kuu, Bwana akusamehe yote uliyokosa kwa kuonja na kusema. Amin.

Katika mikono

¶ Kwa kupakwa huku, na kwa rehema yake kuu, Bwana akusamehe yote uliyokosa kwa kugusa. Amin.

Katika miguu

¶ Kwa kupakwa huku, na kwa rehema yake kuu, Bwana akusamehe yote uliyokosa kwa kutembea. Amin.

¶ *Apake macho katika kope ; masikio katika nderwe zake ; pua pande zote mbili ; midomo yote miwili kwa mara moja ; mikono kitangani ; miguu kwa juu.*

¶ *Akiisha kumpaka pote, akisafishe kidole gumba kwa makombo ya mkate, akanarwe. Kisha, mkate uchomwe motoni.*

¶ Kisha Kasisi aseme,

Bwana, uturehemu,

Kristo, uturehemu,

Bwana, uturehemu,

Baba yetu.

Kupakwa Mafuta

¶ Ee Bwana, umwokoe huyu mtumishi wako.

R. Anayekutumaini Wewe.

¶ Ee Bwana, umpelekee msaada toka patakatifu pako.

R. Na kumtegemeza toka Sayuni.

¶ Ee Bwana, uwe kwake ngome yenye nguvu.

R. Adui asimpate.

¶ Ee Bwana, uwe kwake ngome yenye nguvu.

R. Wala mwana wa uovu asimtese.

¶ Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Kilio changu kikufikie.

¶ Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Bwana Mungu, uliyenena kwa Mtume wako Yakobo : Mtu wa kwenu akiwa hawezi, na awaite wazee wa Kanisa wakamwombee, wakimpaka mafuta kwa Jina la Bwana ; na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua ; na kama ametenda dhambi atasamehewa : Tunakusihi, Mwokozi wetu, umburudishe kwa neema ya Roho Mtakatifu mgonjwa huyu : Umponye jeraha, umsammehe dhambi, umwondolee huzuni na maumivu yote ; na kwa rehema yako umrudishie afya ya roho na ya mwili ; ili, akifanywa mzima tena kwa huruma zako, azirudie kazi zake kwa utukufu wako. Uishiye na kumiliki pamoja na Mungu Baba, katika umoja wake Yeye huyu Roho Mtakatifu, Mungu, daima milele na milele. Amin.

Kupakwa Mafuta

Tuombe.

Ee Bwana, tunakusihii, umwangalie huyu mtumishi wako N. anayetaabika mwili wake kwa ugonjwa huu : Umburudishe roho yake uliyioumba ; ili, akitengenezewa mwenendo wake kwa kurudiwa kwako, ajione kwamba ameokolewa kwa huruma yako. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Tuombe.

Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele, kwa pendo lako kuu watuhifadhi sisi viumbi vyako tulipo wagonjwa, ukitumiminia neema ya baraka yako : Utusikie tukuombao kwa Jina lako, na kwa huruma ukubali ku-mwokoa huyu mtumishi wako N. katika ugonjwa huu ; umpe afya yake, umwinue kwa mkono wako, umfanye imara katika kutenda kila lililo jema, umlinde kwa uweza wako, umfikishe katika Kanisa lako Takatifu akuabudu tena mwenye hali ya heri. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ Bali mgonjwa akiwa kufani, Kasisi asikawie kumpaka mafuta pasipo sala zo zote ila sala ya ghofira. Aidha, ampake mafuta ya paji la uso tu.

Bwana wetu Yesu Kristo kwa rehema zake nyingi akusamehe makosa yako ; na kwa amri yake niliyopewa mimi nakughofiri dhambi zako zote, kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

✚ Kwa kupakwa huku, na kwa rehema yake kuu, Bwana akusamehe makosa yako yote. *Amin.*



KAWAIDA YA KUHUDUMIA SAKRAMENTI ZA MWISHO ZIKITAKIWA ZOTE PAMOJA, MGONJWA AKIWA KUFANI

¶ Kasisi anapoingia chumbani aseme,

V. Amani iwe nyumbani humu.

R. Na kwa watu wote wakaaod ndani yake.

¶ Kisha watu wote waondoke, mgonjwa aka-ungamishwe kama kawaida ikiwezekana ; la ! hairwezekani, Kasisi ampe ghofira tu.

Bwana wetu Yesu Kristo kwa rehema zake nyingi akusamehe makosa yako ; na kwa amri yake niliyopewa mimi nakughofiri dhambi zako zote, kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

¶ Ndipo watu waingie tena, na wakipiga magoti Mhudumu aseme,

Naungama kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watakatifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo na maneno na matendo ; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Kwa hiyo nawasihi Watakatifu wote waniombee, na wewe, baba, unionbee kwa Bwana Mungu wetu.

¶ Kasisi amjibu,

Mwenyezi Mungu akurehemu, akusamehe makosa yako, akufikishe kwenye uzima wa milele. *Amin.*

Bwana Mwenyezi na mwenye rehema akujalie masamaha ✚ ghofira na ondoleo la dhambi zako. *Amin.*

Sakramenti za Mwisho

¶ Kisha Kasisi apige goti, akaitwae Hostia,
akamwonyeshe mgonjwa, akaseme,

Huyu ndiye Mwana Kondoo wa Mungu,
azichukuaye dhambi za ulimwengu.

¶ Kisha aseme mara tatu,

Bwana, si stahili yangu Wewe uingie chini ya
dari yangu ; lakini sema neno tu, na roho yangu
itapona.

¶ Akimshirikisha, aseme,

Pokea, ndugu, chakula hiki cha safari yako,
Mwili wa Bwana wetu Yesu Kristo, kikulinde
na adui mwovu, na kukufikisha kwenye uzima
wa milele.

¶ Kisha Kasisi avisafishe vidole vyake kwa
maji, akavifute kwa kiles. Kisha aseme,

¶. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, Baba wa mbinguni, tunaku-
shukuru sana kwa kuwa umemlisha huyu
ndugu yetu chakula hiki cha rohoni, Mwili wa
Mwana wako Yesu Kristo na Damu yake :
Tunakuomba, umjalie aende kwa nguvu ya
chakula hicho hata akuone katika utukufu wako.
Kwa Yeye. Aishiye.

¶ Kisha aseme,

Kwa Jina la ☧ Baba na ☧ Mwana na ☧
Roho Mtakatifu, nguvu yote ya Shetani ikome-
shwe ndani yako, etc.

akamwekee mikono yake na kuendelea kumpaka
mafuta kama vile ilivyoandikwa katika
Karaida ya Sakramenti ya Kupakwa Mafuta.
(uk. 117.)



KUMWOMBEA MTU ALIYE KUFANI

¶ Kasisi anapoingia chumbani aseme,
¶. Amani iwe nyumbani humu.

R. Na kwa watu wote wakao ndani yake.

¶ Nafasi ikitosha, Kasisi ampe mgonjwa
msalaba ili aubusu ; na akipenda aweza ku-
nyunyiza maji mtakatifu, kama ilivyoamriwa.
(uk. 116.)

¶ Kasisi awaagize wote wanaohudhuria wa-
mwombee mgonjwa, naye mwenyerewe aseme sala za
kumwombea.

¶ Kisha aseme Litania hii, wote wanaohu-
dhuria wamepiga magoti.

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Mariamu Mtakatifu, umwombee.

Enyi Malaika na Malaika Wakuu, mmwombee.

Habil Baba yetu, umwombee.

Ibrahimu Baba yetu, umwombee.

Enyi jamii yote ya wenyehaki, mmwombee.

Yohana Mbatizaji Mtakatifu, umwombee.

Yusuf Mtakatifu, umwombee.

Enyi Babu Watakatifu, mmwombee.

Enyi Manabii Watakatifu, mmwombee.

Petro Mtakatifu, umwombee.

Aliye Kufani

Paolo Mtakatifu, *umwombee*.
Andrea Mtakatifu, *umwombee*.
Yohana Mtakatifu, *umwombee*.
Enyi Mitume na Watunga Injili, *mmwombee*.
Enyi Wanafunzi wote wa Bwana Yesu,
mmwombee.
Enyi Watoto msio hatia, *mmwombee*.
Stefano Mtakatifu, *umwombee*.
Lorenzo Mtakatifu, *umwombee*.
Enyi Mashahidi wote, *mmwombee*.
Gregorio Mtakatifu, *umwombee*.
Augustino Mtakatifu, *umwombee*.
Enyi Maaskofu wote, *mmwombee*.
Enyi Waungamaji wote, *mmwombee*.
Benedikto Mtakatifu, *umwombee*.
Fransis Mtakatifu, *umwombee*.
Enyi Watawa wote, *mmwombee*.
Mariamu Magdalene Mtakatifu, *umwombee*.
Luchia Mtakatifu, *umwombee*.
Enyi Mabikira wote, *mmwombee*.
Enyi Wanawake Watakatifu wote, *mmwombee*.
Enyi Watakatifu wote, *mmwombee*.
 Umwachilie, Bwana.
 Umrehemu.
 Umsamehe, Bwana.
 Umrehemu.
 Umwokoe, Bwana.
 Umrehemu.
Na ghadhabu yako *umwokoe*, Bwana.
Na hatari za kufani *umwokoe*, Bwana.
Na kufa kubaya *umwokoe*, Bwana.
Na maumivu ya jehanum *umwokoe*, Bwana.
Na maovu yote *umwokoe*, Bwana.
Na uwezo wa Shetani *umwokoe*, Bwana.

Aliye Kufani

Kwa Kuzaliwa kwako *umwokoe*, Bwana.
Kwa Msalaba wako *umwokoe*, Bwana.
Kwa Kuteswa kwako *umwokoe*, Bwana.
Kwa Kufa kwako *umwokoe*, Bwana.
Kwa Kuzikwa kwako *umwokoe*, Bwana.
Kwa Kufufuka kwako *umwokoe*, Bwana.
Kwa Kupaa kwako *umwokoe*, Bwana.
Kwa neema ya Roho Mtakatifu *umwokoe*,
Bwana.
Saa ya kufa *umwokoe*, Bwana.
Siku ile ya hukumu *umwokoe*, Bwana.
Sisi wenye dhambi, *utusikie, twakusihi*.
Upende kumwachilia, *utusikie, twakusihi*.
Upende kumsamehe, *utusikie, twakusihi*.
Upende kumwokoa, *utusikie, twakusihi*.
 Bwana, uturehemu.
 Bwana, uturehemu.
 Kristo, uturehemu.
 Kristo, uturehemu.
 Bwana, uturehemu.
 Bwana, uturehemu.
Baba yetu.
¶ *Mgonjwa akiwa sasa katika kufariki, sala zifuatazo na zisemwe.*
Ondoka, Ee roho ya Kikristo, katika ulimwengu huu, kwa Jina la Mungu Baba Mwenyezi aliyekuumba, kwa Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hayi, aliyeswa kwa ajili yako, kwa Jina la Roho Mtakatifu aliomo ndani yako. Ondoka kwa jina la Malaika na Malaika Wakuu na jeshi lote la mbinguni, kwa jina la Babu na Manabii, kwa jina la Mitume na Watunga Injili, kwa jina la Mashahidi na Waungamaji, Watawa na Mabikira, na Watakatifu wote wa Mungu.

Ukae tangu leo katika amani, uwe na makao yako katika mji mtakatifu. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Tuombe.

Ee Mungu mwenye rehema nyingi, kwa wingi wa rehema zako waziondoa dhambi zao wote watubuo kwa kweli, hata huzikumbuki tena : Umtazame kwa macho yako ya rehema huyu mtumishi wako, anayetaka sana masamaha kwako. Umtengenezee, Ee Baba mwenye upendo mwingi, kila kilichoharibika kwa hila na jeuri za Shetani, au kwa nia yake mwenyewe, au kwa udhaifu wa mwili. Umhifadhi na kumjalia adumu kuwa katika umoja wa Kanisa lako. Utazame toba lake, ukubali machozi yake, upunguze maumivu yake. Na kwa kuwa anazitumainia rehema zako tu, usimhesabie dhambi zake zilizopita, bali umtie nguvu za Roho yako Mtakatifu ; hata, utakapopenda aondoke duniani, umweke katika hali ya neema. Kwa kustahili kwake Mwana wako umpendaye, Yesu Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Ndugu yetu tukupendaye, mikononi mwake Mwenyezi Mungu tunakuweka, maana u kiumbe chake, ili, utakapookoka katika kifungo cha dunia hii, umrudie Muumba wako amini, aliyekuumba kwa mavumbi ya nchi. Majeshi ya Malaika na wailaki roho yako itakapofarakana na mwili wako, jamii tukufu ya Mitume na wakupokee, jeshi la Mashahidi wavaao mavazi meupe na wakukaribishe, kusanyiko ling'aalo la Waungamaji na wakuzunguke, Mabikira wakiimba kwa furaha na wakutangulie, ukapate raha mustarehe kifuani pa Babu.

Uso wake Yesu Kristo ukutokee mpole wenye furaha ; akakuwekee mahali mionganini mwa walioko mbele zake daima. Mungu akujalie usijue kamwe hofu ya giza ya milele. Shetani na pepo zote wabaya watoweke mbele yako ; atetemeke utakapokuja wewe pamoja na Malaika wakulindao, akakimbie mbali kwenye mashimo ya usiku wa milele.

Mungu ataondoka, adui zake watatawanyika, Nao wamchukiao wataukimbia uso wake.

Kama moshi upeperushwavyo,

Ndivyo utakavyowapeperusha ;

Kama nta iyeyukavyo mbele ya moto,

Ndivyo wabaya watakavyopotea mbele za Mungu.

Bali wenye haki watafurahi,

Watashangilia mbele za Mungu.

Makundi yote ya Jehanum waone haya, wafe-dheheke ;

Vitwana wa Shetani wasithubutu kukupingia njia.

Kristo aliyesulibiwa kwa ajili yako akuokoe na mateso.

Kristo aliyekubali kufa kwa ajili yako akuokoe na kufa kwa milele.

Kristo, Mwana wake Mungu aliye hayi, akupeleke kwenye majani yameayo ya peponi pake ; Mchunga aliye mwema akukiri kuwa kondoo wake ; akughofiri dhambi zako zote, akuveke mkono wake wa kuume katika urithi wa wateule wake.

Umwone Mkombozi wako uso kwa uso, na uwepo mbele zake daima, kwa macho ya uheri ukaitazame dhahiri Kweli isiyokoma. Na

ukiisha kuwekwa huko mionganini mwao walio heri, uufurahie utamu wa kumwona Mungu milele na milele. *Amin.*

Ee Bwana, umpokee mtumishi wako panapo wokofu, atakapotumaini kuokoka milele kwa rehema zako. *Amin.*

Mikononi mwako, Ee Bwana, tunaiweka roho ya huyu mtumishi wako N. tunakusihi, Bwana Yesu Kristo, Mwokozi wa ulimwengu, usikatae kumwekeea mahali kifuani pa Babu, kwa maana ulishuka kutoka mbinguni kwa ajili yake na kwa wokofu wake. Umkumbuke, Ee Bwana, kiumbe chako, kwa kuwa hakuumbwa na miungu mingine, bali na Wewe uliye peke yako Mungu halisi ; maana hakuna miungu mingine ila Wewe, wala kazi iliyo mfano wa kazi zako. Uifurahishe, Ee Bwana, roho yake mbele zako, wala usiyakumbuke makosa yake. Ingawa amekutenda dhambi, hakukukana Wewe, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, bali amekuamini, na jitihadi kwa Mungu amekuwa nayo moyoni, na kwa uaminifu amekuabudu Wewe, Mungu, Muumba vitu vyote.

Usizikumbuke, Ee Bwana, dhambi za ujana wake wala ujinga wake, lakini kwa kadiri ya rehema zako umkumbuke katika mwanga wa utukufu wako. Mbingu na zifunuke kwake ; Malaika na wamfurahie. Umpokee mtumishi wako, Ee Bwana, katika ufalme wako. Mikael Mtakatifu, Malaika Mkuu, na amkaribishe, Malaika watakatifu wa Mungu na waje kumlaki, na kumchukua kwenye mji ule mtakatifu, Yerusalem mpya. Petro Mtume mbarikiwa, aliyepewa na Mungu funguo za ufalme wa

mbinguni, na amkaribishe. Paolo Mtakatifu, Mtume aliystahili kuwa chombo kiteule, na amsaidie. Yohana Mtakatifu, Mtume mteule wa Mungu, aliyefunuliwa siri za mbinguni, na amwombee. Mitume wote, waliopewa na Bwana mamlaka ya kufunga na kufungua, na wa mwombee. Watakatifu wote na Wateule wa Mungu, waliostahimili mateso katika ulimwengu huu kwa ajili ya Jina la Kristo, na wamwombee. Ili, akiisha kuokoka katika kifungo cha mwili huu wa uharibifu, astahili kufika kwenye utukufu wa ufalme wa mbinguni. Kwa neema na kustahili kwake Bwana wetu Yesu Kristo ; Aishiye na kumiliki pamoja na Baba, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima milele na milele. *Amin.*

¶ *Mgonjwa akiwa hasa katika kufariki, wote waliopo na wazidi kusali kwa bidii. Mgonjwa mwenyerewe akiweza—la ! harwezi, Kasisi au mtu mwingine—aseme mara nyangi kwa sauti ya kusikika, Yesu, Yesu, Yesu, Aidha yafaa pia kusema mara kwa mara maneno haya,*

Mikononi mwako, Ee Bwana, naiweka roho yangu.

*Mimi ni wako, Ee Bwana, uniokoe.
Bwana Yesu, ipokee roho yangu.
Mariamu Mtakatifu, uniombee.*

¶ *Mgonjwa akiisha kufariki, sala zifuatazo na zisemwe.*

Njoni kumsaidia, Enyi Watakatifu wa Mungu ; njoni kumlaki, Enyi Malaika wa Bwana : ipokeeni roho yake : iletensi mbele zake Aliye juu.

Aliye Kufani

Y. Kristo aliyekuita akupokee : Malaika wakuchukue kifuani kwa Ibrahimu.

R. Ipokeeni roho yake : ileteni mbele zake Aliye juu.

Y. Raha ya milele umjalie, Ee Bwana : na nuru ya daima imwangaze.

R. Ileteni mbele zake Aliye juu.
Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Baba yetu.

Y. Usitutie majaribuni.

R. Lakini utuokoe na maovu.

Y. Raha ya milele umjalie, Ee Bwana.

R. Na nuru ya daima imwangaze.

Y. Ee Bwana, uiokoe roho yake.

R. Na milango ya Jehanum.

Y. Astarehe katika amani.

R. Amin.

Y. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R. Kilio changu kikufikie.

Y. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Tunakuomba, Ee Bwana, uighofiri roho ya huyu mtumishi wako N. aliyefariki katika dunia ili akuishie Wewe : Umsamehe yote aliyokukosa kwa udhaifu wake wa ubinadamu ; ukamsafishe kwa huruma zako nyingi. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*



KUWAOMBIA WALIOFARIKI WAKATI WO WOTE

✚ Kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.* Baba yetu. Salamu, Mariamu.

Ant. Kama ungehesabu.

Zab. 130.

1. Toka vilindini nimekulilia, Ee Bwana :
Ee Bwana, uisikilize sauti yangu.
2. Masikio yangu na yaiangalie :
Sauti ya dua zangu.
3. Kama ungehesabu maovu, Ee Bwana :
Ee Bwana, nani angesimama ?
4. Lakini kwako kuna samaha :
Ili uogopwe.
5. Nimemngoja Bwana, roho yangu imengoja :
Na neno lake nimelitumainia.
6. Roho yangu inamngoja Bwana kuliko walinzi waingojavyo asubuhi :
Naam, kuliko walinzi asubuhi.
7. Ee Israeli, umtarajie Bwana :
Maana kwa Bwana kuna fadhili.
8. Na kwake kuna ukombozi mwangi :
Naye atamkomboa Israeli na maovu yake yote.

Raha ya milele :

Uwajalie, Ee Bwana.

Na nuru ya daima :

Iwaangaze.

Ant. Kama ungehesabu maovu, Ee Bwana :
Ee Bwana, nani angesimama ?

¶. Ee Bwana, uziokoe roho zao.

R/. Na milango ya Jehanum.

¶. Wastarehe katika amani.

R/. Amin.

¶ *Kisha sala hii, au sala yo yote ya Wafu inayohusu, inaweza kusemwa.*

¶. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R/. Kilio changu kikufikie.

Tuombe.

Ee Mungu, umewaumba waaminifu wote na kuwaokoa : Uzijalie roho za watumishi na wajakazi wako ondoleo la dhambi zao zote ; wapewe, kwa sala za pendo, masamaha walioyataka siku zote. Uishiye na kumiliki, Mungu, milele na milele. *Amin.*

¶. Raha ya milele uwajalie, Ee Bwana.

R/. Na nuru ya daima iwaangaze.

Wastarehe katika amani.

R/. Amin.

¶ *Sala nyiningine.*

Uzikubali dua zetu, tunakusihi, Ee Bwana, tunazotoa mbele zako kwa ajili ya roho za watumishi wako : Uwajalie thawabu ya uzima wa milele ; kwa kuwa umewastahilisha kuishiriki imani ya Kikristo. Uishiye na kumiliki, Mungu, milele na milele. *Amin.*

Ee Bwana, tunakuomba sala yetu izifalie roho za watumishi wako : Upende kuwatenaganisha na dhambi zote ; na kuwashirikisha ukombozi wako. Uishiye na kumiliki, Mungu, milele na milele. *Amin.*

Ee Mungu, Bwana wa rehema : Uziangalie roho za watumishi wako waliofariki katika dunia ; uwajalie mahali pa kuburudika, furaha ya amani, na mwanga wa nuru yako. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Ee Bwana, tunazileta dua zetu kwa ajili ye watumishi wako waliofariki katika dunia : Uzikubali, tunakusihi ; ukawajalie wastahili kushirikiana na Watakatifu wako katika utukufu wa milele. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Mwenyezi Mungu, tunakusihi, uziangalie roho za watumishi wako waliofariki katika dunia : Uwajalie wasafishwe katika dhambi zao ; wakapewe masamaha na raha ya milele. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Ee Mungu, wapenda kuwasamehe wanadamu na kuwaokoa : Uzijalie, tunakuomba, roho za watumishi wako waliofariki katika dunia wao-mbewe na Mariamu Bikira Mbarikiwa, na Watakatifu wote ; wakaufikie ushirika wa furaha za milele. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Ee Mungu, rehema zako hazina kiasi : Uzikubali sala zetu za unyenyekevu ; ukawasamehe roho za watumishi wako waliofariki katika dunia, kwa kuwa umewapa moyo wa kulikiri Jina lako takatifu. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Mwenyezi Mungu mwenye rehema, uzikubali dua zetu : Uziangalie roho za watumishi wako waliofariki katika dunia ; na kwa ajili ya Jina lako uwasamehe dhambi zao, ukawape furaha ya nuru ya milele. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Kwa Askofu au Kasisi.

Ee Mungu, ulimkubali mtumishi wako N. kuwa Askofu (Kasisi), wa Mwana wako : Usikie kuomba kwetu ; umjalie furaha pamoja na Maaskofu (Makasisi) wako waaminifu. Kwa Yeye, Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Siku ya kufa mtu au ya kuzikwa mtu.

Tunakuomba, Ee Bwana, uighofiri roho ya mtumishi wako N. aliyefariki katika dunia ili akuishie Wewe : Umsamehe yote aliyokukosa kwa udhaifu wake wa ubinadamu ; ukamsafishe kwa huruma zako nyingi. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Siku ya ukumbusho wake.

Ee Mungu, Bwana wa rehema : Tunamwombua kwako mtumishi wako N. ambaye tunamkumbuka mbele zako leo ; umjalie mahali pa kuburudika, furaha ya amani, na mwanga wa nuru yako. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Kwa mtu mmoja aliyefariki.

Tunakuomba, Ee Bwana, uighofiri roho ya mtumishi wako N. umfungulie minyororo ya dhambi zake zote : Ili katika utukufu wa kiyama afufuke ; na kuburudika pamoja na Watakatifu na wateule wako. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Kwa watu wengi waliofariki.

Ee Mungu, ni sifa yako kurehemu na kusamehe siku zote : Uwahurumie roho za watumishi wako N. na N. na kuwasamehe makosa yao yote ; ili wafunguliwe minyororo ya mauti, wakastahili kuingia katika uzima. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Kwa baba au mama.

Ee Mungu, umetuamuru tuwaheshimu baba na mama : Kwa wema wako mwingi umrehemu baba (mama) yangu,* na kumsamehe makosa yake yote ; ili nionane naye tena katika furaha ya nuru ya milele. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

* *Au*, wazazi wangu, *ukaitumie jumla ya wingi.*

Kwa ndugu zetu.

Ee Mungu, wapenda kuwasamehe wanadamu na kuwaokoa : Uwajalie, tunakuomba, wafu wetu, ndugu zetu zote wa Mtaa huu, majirani zetu, na wote waliotutendea mema, waombewe na Mariamu Bikira Mbarikiwa, na Watakatifu wote ; wakaufikie ushirika wa furaha za milele. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Kwa wote walalao katika kiwanja cha makaburi.

Ee Mungu, kwa rehema yako roho za waaminifu wastarehe katika amani : Uwajalie watumishi wako, na wote waliolala katika Kristo hapa petu na kila mahali, ondoleo la dhambi zao ; ili wafunguliwe hatia zote, na kufurahi pamoja nawe daima. Kwa Yeye, Kristo Bwana wetu. *Amin.*



KUZIKWA MKRISTO

AMRI YA KANISA

1. Mkristo aliyecharimishwa au kutengwa, amekufa hajatubu, hana maziko kwetu.
2. Mkristo aliyejiua hana maziko kwetu.
3. Iwapo Mkristo hakuupokea Ushirika Utakatifu muda wa mwaka mzima kabla ya kufa kwake, hakuna ruhusa ya kumleta Kanisani ; bali sala zote zisomwe kaburini. Lakini ikiwa amerwahi kupokea Sakramenti za Kanisa kufani, na aletwe Kanisani kama kawaida.

SEHEMU YA KWANZA

¶ Sehemu hii isemwe, au iimbwe, Kanisani ikiwezekana ; la ! haiwezekani, isemwe penye kaburi. Ni marufuku maiti asiwekwe mahali pake Kanisani pasipo Kasisi, hata ikiwa usiku.

¶ Kasisi na wahudumu wake wamlaki maiti mlangoni pa Kanisa (au pa kirwanja cha makaburi), wamtangulie kuingia Kanisani (au kwenye kaburi).

¶ Ndipo Kasisi aseme, au watu waimbe, Mimi najua ya kuwa Mkombozi wangu yu hayi, na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi. Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, lakini katika mwili wangu nitamwona Mungu. Nami nitamwona mimi nafsi yangu, na macho yangu yatamtazama, wala si mwingine,

Hatukuja na kitu duniani, tena ni dhahiri ya kuwa hatuwezi kutoka na kitu. Bwana alitoa, na Bwana ameondoa ; Jina la Bwana lihimidiwe.

¶ Aya hizi zikiisha, iimbwe, au isomwe, Zaburi ifuatayo, watu wangali wanaingia. Wifikifa penye Patakatifu (au penye kaburi), maiti awekwe kuelekea mashariki, Kasisi na wahudumu wake wakimwelekea maiti.

¶ (Iwapo maiti ni Kasisi au Askofu, awekwe mbele ya madhbahu, kuelekea magharibi, kukabili watu wake aliorwachunga ; na Kasisi asimame kukabili madhbahu).

Ant. Kama ungehesabu.

Zab. 39.

1. Nalisema, Nitazitunza njia zangu :
Nisije nikakosa kwa ulimi wangu.
2. Nitajitia kijamanda kinywani :
Maadam asiye haki yupo mbele yangu.
3. Nalikuwa sisemi, nalinyamaa kimya :
Sina faraja, maumivu yangu yakazidi.
4. Moyo wangu ukawa moto ndani yangu :
Na katika kuwaza kwangu moto ukawaka.
5. Nalisema kwa ulimi wangu :
Ee Bwana, unijulishe mwisho wangu.
6. Na kiasi cha siku zangu ni kiasi gani :
Nijue jinsi nilivyo dhaifu.
7. Tazama, umefanya siku zangu kuwa mashubiri :
Maisha yangu kama si kitu mbele zako.
8. Ubatili tu ni kila mwanadamu ingawa amesitawi :
Bin Adamu huenda tu huko na huko kama kivuli.

9. Hufanya ghasia tu kwa ajili ya ubatili :
Huweka akiba wala hajui ni nani ataka-yeichukua.
 10. Na sasa ninangoja nini, Ee Bwana :
Matumaini yangu kwako.
 11. Uniokoe na maasi yangu yote :
Usinifanye lawama ya mpumbavu.
 12. Nimenyamaza sitafumbua kinywa changu :
Maana Wewe ndiwe uliyeyafanya.
 13. Uniondolee pigo lako :
Kwa uadui wa mkono wako nimeangamia.
 14. Ukimrudi mtu kwa kumkemea :
Kwa ajili ya uovu wake.
 15. Watowesha uzuri wake kama nondo :
Ubatili tu ni kila mwanadamu.
 16. Usikie maombi yangu, Ee Bwana, utegesikio lako niliapo :
Usiyanyamalie machozi yangu.
 17. Kwa maana mimi ni mgeni wako :
Msafiri kama baba zangu zote.
 18. Uniachilie nikunjuke uso :
Kabla sijaondoka nisiwepo tena.

Raha ya milele :
Uwajalie, Ee Bwana.

Na nuru ya daima :
Iwaangaze.
- Ant.* Kama ungehesabu maovu, Ee Bwana :
Ee Bwana, nani angesimama ?
- ¶ *Au hii,*
- Ant.* Mifupa uliyoiponda.
- Zab. 51.
1. Unirehemu, Ee Mungu :
Kwa kadiri ya fadhili zako.

2. Kwa kadiri ya wingi wa rehema zako :
Uyafute makosa yangu.
3. Unioshe kabisa na uovu wangu :
Unitakase dhambi zangu.
4. Maana nimejua mimi makosa yangu :
Na dhambi yangu i mbele yangu daima.
5. Nimekutenda dhambi Wewe peke yako :
Na maovu nimefanya mbele za macho yako.
6. Ili uhesabiwe kuwa una haki unenapo :
Na kuwa safi utoapo hukumu.
7. Mimi naliumbwu katika hali ya uovu :
Mama yangu alinichukua mimba hatiani.
8. Bali wapendezwa na kweli iliyo moyoni :
Utanijulisha hekima kwa siri.
9. Unisafshe kwa husopo nami nitakuwa safi :
Unioshe nami nitakuwa mweupe kuliko thuluji.
10. Unisikize furaha na shangwe :
Mifupa uliyoiponda ifurahi.
11. Usetiri uso wako usitazame dhambi zangu :
Uzifute hatia zangu zote.
12. Ee Mungu, uniumbie moyo safi :
Uifanye upya roho yangu ndani yangu.
13. Usinitenge na uso wako :
Wala Roho yako Mtakatifu usiniondo-lee.
14. Unirudishie furaha ya wokofu wako :
Unitegemeze kwa Roho yako bora.
15. Nitawafundisha wakosaji njia zako :
Na wenye dhambi watarejea kwako.
16. Uniponye na damu za watu, Ee Mungu,
Mungu wa wokofu wangu :
Na ulimi wangu utaiimba haki yako.

17. Ee Bwana, ufunue midomo yangu :
Na kinywa changu kitanena sifa zako.
18. Maana Wewe hupendezwi na dhabihu, kama
sivyo ningeitoa :
Walakini huridhii kafara.
19. Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika :
Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee
Mungu, hutaudharau.
20. Uitendee mema Sayuni kwa radhi yako :
Uzijenge kuta za Yerusalem.
21. Ndipo utakapopendezwa na dhabihu za
haki :
Na sadaka za kuteketezwa na kafara.
22. Ndipo watakapotoa ng'ombe :
Juu ya madhbahu yako.
Raha ya milele :
Uwajalie, Ee Bwana.
Na nuru ya daima :
Iwaangaze.

Ant. Mifupa uliyoiponda : na imfurahie
Bwana.

¶ *Baada ya Zaburi Kasisi asome sehemu ya
Msahafu, ndiyo,*

Ndugu : Kristo amefufuka, limbuko lao
waliolala. Maana kwa kuwa mauti ililetwa
na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa
na mtu. Kwa kuwa katika Adamu wote wanaku-
fa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.
Lakini kila mmoja mahali pake ; limbuko
Kristo ; baadaye walio wake Kristo, atakapo-
kuja. Ndipo palipo mwisho, atakapompa Mungu
Baba ufalme ; atakapobatilisha utawala wote,
na mamlaka yote, na nguvu. Maana sharti
amiliki Yeye, hata awaweke maadui wote chini

ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebati-
lishwa ni mauti.

¶ *Au hii,*

Ndugu : Nisemayo ni haya, ya kuwa nyama
na damu haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu ;
wala uharibifu kurithi kutokuharibika. Anga-
lieni, nawaambieni siri ; hatutalala wote, lakini
wote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba
na kufumbua, wakati wa panda la mwisho ;
maana panda litalia, na wafu watafufuka,
wasiwe na uharibifu, na sisi tutabadilika.
Maana sharti huu wenye uharibifu uvae kuto-
kuharibika, nao huu wa kufa, uvae kutokufa.
Basi, uharibifu huu utakapovaa kutokuharibika,
na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo
ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa,
Mauti imemezwa kwa kushinda. U wapi,
mauti, uchungu wako ? Ku wapi, kaburi,
kushinda kwako ? Uchungu wa mauti ni
dhambi, na nguvu za dhambi ni sheria.
Lakini tumshukuru Mungu, atupaye kushinda
kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Basi, ndugu
wapendwa, mwe imara, msiotikisika, mkizidi
sana kutenda kazi ya Bwana siku zote, kwa
kuwa taabu yenu siyo bure katika Bwana.

¶ *Au hii,*

Ndugu : Mkiwa mmefufuka pamoja na
Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko
mkono wa kuume wa Mungu, ameketi. Nieni
yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana
mlikufa, na uzima wenu umefichwa pamoja na
Kristo katika Mungu. Kristo atakapoonekana,
aliye uzima wetu, ndipo na ninyi mtaonekana
pamoja naye katika utukufu. Basi, vifisheni

viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu : kwa ajili ya hayo ghadhabu ya Mungu huwafikia wana wa kuasi. Katika hayo na ninyi mlitembea zamani, mlipoishi katika haya.

GHOFIRA YA WAFU

¶ Baada ya Somo itolerwe Missa, au, ikiwa hakuna Missa, haya yafuate mara. Walakini ikiwa msalisha yu Mvalimu asiseme ila sala tu, (uk. 145).

¶ Missa ikiisha, Kasisi avue kasula yake na manipolo, avae kappa nyeusi.

¶ Ikitolerwa Missa Kuu, Shemasi mdogo achukue msalaba, na Shemasi amsaidie Kasisi, akisimama mkono wake wa kushoto.

¶ Mchukua msalaba na wachukua mishumaa waende wakasimame penye kichwa cha maiti, mbali nacho kidogo, wameikabili madhbahu : Kasisi na wahudumu wake, wakichukua chetizo, uvumba, na maji matakatifu, wasimame penye miguu ya maiti.

¶ (Iwapo maiti ni Kasisi, Mchukua msalaba asimame upande, kwa kuwa upo msalaba madhbuni : na Kasisi asimame angali ameikabili madhbahu.)

¶ Ndipo Kasisi aseme Sala ya kumghofiri maiti.

Ee Bwana, usimhukumu mtumishi wako, maana mbele zako hakuna mtu atakayekuwa mwenye haki, isipokuwa wale uliowasafisha Wewe.

Tunakuomba hukumu yako isiwe nzito kwa huyu ndugu yetu tunayemweka kwako, kwa

kukutumaini na kukuomba, tukimkumbuka Kristo Yesu, asili ya imani yetu.

Bali umjalie aiepuke hukumu ya ukali kwa ukarimu wako, kwa maana alipokuwa hayi alitiwa muhuri yako Wewe, Utatu Mtakatifu ; Uishiye na kumiliki, Mungu, milele na milele. Amin.

¶ Marufuku Sala hii isibadiliwe neno, hata watu wengi wakirwa wanazikwa siku moja.

¶ Ndipo aseme, au watu waimbe,

¶ Uniokoe, Ee Bwana, na mauti ya milele kunako siku ile ya hofu* : mbingu na nchi zitakapotikisika : utakapokuja kuuhukumu ulimwengu kwa moto.

¶ Uniokoe, Ee Bwana, na mauti ya milele kunako siku ile ya hofu* : mbingu na nchi zitakapotikisika : utakapokuja kuuhukumu ulimwengu kwa moto.

¶ Nimeingia hofu, ninatetemeka* : hata hukumu iwekwe, ghadhabu ikaonekane.

¶ Mbingu na nchi* zitakapotikisika :

¶ Siku ile ya ghadhabu, shida, na huzuni* : siku ya uchungu mwangi.

¶ Utakapokuja* kuuhukumu ulimwengu kwa moto.

¶ Raha ya milele uwajalie, Ee Bwana* : na nuru ya daima iwaangaze.

¶ Uniokoe, Ee Bwana, na mauti ya milele kunako siku ile ya hofu* : mbingu na nchi zitakapotikisika : utakapokuja kuuhukumu ulimwengu kwa moto.

¶ Huko nyuma, watu waanzapo R. ya mwisho, Kasisi atie uvumba katika chetizo, aubariki kama karwaida.

¶ Kisha iimbrwe, au isemwe,
Bwana, uturehemu.
Kristo, uturehemu.
Bwana, uturehemu.

¶ Kisha Kasisi aanze,
Baba yetu. (kimoyomoyo.)

¶ Ndipo Kasisi amnyunyizie maiti maji na kumfukizia uvumba. Kwanza akitwae kinyunyizo, auinamie msalaba ulio kichwani pa maiti, aende na mchukua maji wakasimame upande wa kaskazini, Kasisi akamnyunyizie maiti mara tatu, yaani, miguuni, kifuani, na kichwani ; kisha apite kwenye kichwa chake, akasimame upande wa kusini, akafanye yayo hayo. Kisha arudie mahali pake, akampe mhudumu kinyunyizo, akakitwae chetezo, na kumfukizia maiti. Atamfukizia vile alivyomnyunyizia, akisimama pande zote mbili za jeneza na kumfukizia miguu, kifua, na kichwa.

¶ Iwapo hapana nafasi ya kuzunguka jeneza, Kasisi aweza kusimama mahali pake na kufanya kazi hii, akimnyunyizia maiti na kumfukizia mara tatu. Na kawaida hii ya kusimama ishikwe kila inaposemwa sala hii penye kaburi.

¶ Kisha Kasisi aseme,
V. Usitutie majoribuni.
R. Lakini utuokoe na maovu.
V. Ee Bwana, uiokoe roho yake.
R. Na milango ya Jehanum.
V. Astarehe katika amani.
R. Amin.
V. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.
R. Kilio changu kikufikie.

V. Bwana akae nanyi.
R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Ee Mungu, ni sifa yako kurehemu na kusamehe siku zote : Tunakuomba dua yetu kwa unyenyekevu, kwa ajili ya roho ya huyu mtumishi wako N. uliyemruhusu afariki katika dunia hii ; usimtie katika mikono ya adui yake, wala usimsahau milele ; bali uamuru akaribishwe na Malaika zako Watakatifu, asikose kufika kwetu Peponi ; na kwa kuwa amekutumaini na kukuamini asione adhabu za daima, bali apewe furaha za milele. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ Ndipo maiti achukulirwe kwenda kaburini.

¶ Njiani ni heri watu waimbe Litania ya Mfu na Zaburi, kama Zaburi 6, 32, 69, 102, 130, 143. Ikiwa hairwezekani kuimba, zisomwe na Kasisi.

¶ Haifai kuimba, wala kusema, maneno ya Dini penye watu wengi wasio Dini yetu. Basi katika njia zenye watu wengi yafaa maiti achukulirwe kimya, mtu asiseme na mwenziriwe.

¶ Iwapo Askofu ameruhusu Litania au Nyimbo nyiningine ziimbwe njiani, basi na ziimbwe hapo badala ya Zaburi zilizoamriwa.

SEHEMU YA PILI

¶ Ikiwa kiwanja cha makaburi hakijawekwa wakfu, Kasisi na aliweke wakfu kaburi lilochimbwa, akaseme,

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, kwa rehema zako watu wako walioifariki dunia hustarehe : Upende kulibariki kaburi hili, umweke Malaika wako alilinde ; umjalie huyu ndugu yetu, ambaye tunauzika mwili wake humu, afunguliwe minyororo ya dhambi zake zote, akapate furaha ya milele kwako, pamoja na Watakatifu wako wote. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ *Kisha, maiti angali analala katika jeneza, iimbwe BENEDICTUS.*

¶ *Huko nyuma Kasisi amnyunyizie maiti, na kaburi lake, akamfukizie, yeye na kaburi lake. Kisha maiti atiwe kaburini.*

¶ *Kazi hizi zote zimalizike kabla BENEDICTUS haijisha kuimbwa.*

*Ant. Mimi ni ufufuo na uzima.
Benedictus.*

1. Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli :
Kwa kuwa amewajia watu wake na kuwakomboa.
2. Ametuondokeshea wokofu wa nguvu :
Katika nyumba ya Daudi mtumishi wake.
3. Kama alivyosema tangu mwanzo :
Kwa vinywa vya manabii wake watakatifu.
4. Tuokolewe na adui zetu :
Na katika mikono yao wote wanaotuchukia.
5. Ili kuwatendea rehema baba zetu :
Na kukumbuka agano lake takatifu.
6. Uapo aliomwapia Ibrahimu, baba yetu :
Ya kwamba atatujalia sisi.
7. Tukiokoka mikononi mwa adui zetu :
Tumwabudu pasipo hofu.

8. Katika utakatifu na kwa haki :
Mbele zake siku zetu zote.
9. Na wewe nawe Mtoto, utakwitwa nabii wake Aliye juu :
Kwa maana utatangulia mbele ya uso wake Bwana, ufanyize njia zake.
10. Uwajulishe watu wake wokofu :
Zikiondolewa dhambi zao.
11. Kwa rehema zake Mungu wetu :
Kwazo mwangaza wa juu umetujia.
12. Kuwaangaza wakaa katika giza na uvuli wa mauti :
Na kuelekeza miguu yetu mnamo njia ya amani.
- Raha ya milele :
Uwajalie, Ee Bwana.
- Na nuru ya daima :
Iwaangaze.

Ant. Mimi ni ufufuo na uzima ; aniaminiye Mimi, ijapo afe, atakuwa ataishi : na kila mwenye uzima na kuniamini Mimi hatakufa kabisa hata milele.

¶ *Wazishi wakiisha kutoka kaburini, Kasisi aseme,*

Mtu aliyezaliwa na mwanamke siku zake si nyingi, naye amejaa taabu. Huota, hukatwa kama majani, hupita kama kivuli, wala hakai.

Kati ya uzima tu katika kufa : tutake msaada kwa nani, ila kwako Wewe, Bwana, uliye na haki kutukasirikia kwa dhambi zetu ?

Lakini, Ee Mungu uliye Mtakatifu, Bwana mwenye uweza, Mwokozi Mtakatifu mwenye rehema, usituache katika maumivu machungu ya mauti ya milele.

Wajua, Ee Bwana, siri za mioyo yetu : usizibe masikio yako ya rehema tunapokuumba : utuachilie, Ee Mungu uliye Mtakatifu, Bwana mwenye uweza, Mwokozi Mtakatifu mwenye rehema, Mhukumu mwema wa milele, usituache saa yetu ya mwisho kufarakana nawe.

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amependa, kwa rehema zake nyingi, kujitwalia roho ya huyu ndugu yetu mpendwa N. aliyefariki, sisi tunauweka mwili wake chini ya nchi : udongo kwa udongo, (*hapa wazishi watie mavumbi kidogo mara tatu*) majivu kwa majivu, mavumbi kwa mavumbi ; kwa tumaini thabiti, pasipo shaka, la Ufufuo wa uzima wa milele, kwa Bwana wetu Yesu Kristo ; atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule awezao kuvitiisha hata na vitu vyote chini yake.

Bwana, umrehemu.

Kristo, umrehemu.

Bwana, umrehemu.

Baba yetu.

¶. Usitutie majaribuni.

R;. Lakini utuokoe na maovu.

¶. Bwana akae nanyi.

R;. Akae na roho yako.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, kwako waishi roho zao waifarikio dunia katika Bwana, na kwako roho za waaminifu, wakitolewa katika mzigo wa mwili huu, wanakaa katika furaha na kustarehe: Tunamwombea huyu ndugu yetu mpendwa N. aliyetoka katika taabu za dunia hii ya dhambi,

aone furaha hiyo na kustarehe. Tunakusih iupeende, kwa wema wa neema yako, kuitimiza upesi hesabu ya wateule wako, na kuuhimiza ufalme wako ; ili sisi, pamoja nao wote waliofariki wenyewe imani ya kweli ya Jina lako takatifu, tupate mwisho mkamilifu, na raha ya mwili na ya roho, katika utukufu wako wa milele. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶. Raha ya milele umjalie, Ee Bwana.

R;. Na nuru ya daima imwangaze.

Astarehe katika amani.

R;. Amin.

Roho yake na roho za waaminifu wote waliofariki kwa rehema ya Mungu wastarehe katika amani.

R;. Amin.

¶ *Nyimbo zimekatazwa zisiimbwe ila nyimbo zilizoamririva kuimbra njiani.*

KUZIKWA MTOTO MCHANGA ALIYE MKRISTO

Yaani, asiyetimiza miaka saba umri wake.

SEHEMU YA KWANZA

¶ (1) *Itumike rangi nyeupe na mishumaa meupe ; tena ni desturi kichwa cha msalaba kichukuliwe peke yake bila fimbo yake. Zikipigwa kengele, zisipigwe kwa namna ya huzuni.*

(2) *Uvumba na maji matakatifu visitumike Kanisani, bali vitumike kaburini tu.*

(3) *Hakuna Missa wala Sala ya kumghofiri maiti.*

¶ Kasisi na wahudumu wake wamlaki maiti mlangoni pa Kanisa, wamtangulie kuingia Kanisani.

¶ Ndipo Kasisi aseme, aii watu waimbe, Mimi najua ya kuwa Mkombozi wangu yu hayi, na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi. Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, lakini katika mwili wangu nitamwona Mungu. Nami nitamwona mimi nafsi yangu, na macho yangu yatamtazama, wala si mwingine.

Hatukuja na kitu duniani, tena ni dhahiri ya kuwa hatuwezi kutoka na kitu. Bwana alitoa, na Bwana ameondoa ; Jina la Bwana lihimidiwe.

Ant. Atapokea.

Zab. 24.

1. Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana :
Dunia na wote wakaaon ndani yake.
2. Maana Yeye ndiye aliyeiweka misingi yake
juu ya bahari :
Na juu ya mito ya maji aliithubutisha.
3. Ni nani atakayepanda katika mlima wa
Bwana :
Ni nani atakayesimama katika patakatifu
pake.
4. Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe,
asiyeinua roho yake kwa ubatili :
Wala hakuapa kwa hila.
5. Atapokea baraka kwa Bwana :
Na haki kwa Mungu wa wokofu wake.
6. Hiki ndicho kizazi cha wamtafutao :
Wakutafutao uso wako, Ee Mungu wa
Yakobo.

7. Inueni vichwa vyenu, enyi malango, inukeni, enyi malango ya milele :
Mfalme wa utukufu apate kuingia.

8. Ni nani Mfalme wa utukufu :
Bwana mwenye nguvu na uhodari, Bwana
hodari wa vita.

9. Inueni vichwa vyenu, enyi malango, naam,
viinueni, enyi malango ya milele :
Mfalme wa utukufu apate kuingia.

10. Ni nani huyu Mfalme wa utukufu :
Bwana wa majeshi, ndiye Mfalme wa
utukufu.

Utukufu una Baba na Mwana :
Na Roho Mtakatifu.

Ulivyokuwa mwanzo :

Ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. Amin.

*Ant. Atapokea baraka kwa Bwana, na haki
kwa Mungu wa wokofu wake : hiki ndicho
kizazi cha wamtafutao Bwana.*

¶ Kisha Kasisi asome,

Ndugu : Wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, na Yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao. Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana Mwana Kondoo aliye kati kati ya kiti cha enzi atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhayi, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao.

¶. Bwana akae nanyi.

Ry. Akae na roho yako.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, umeahidi kuwapa uzima wa milele watoto Wakristo waliofariki katika dunia kabla hawajakukosa : Utujalie na sisi tuone furaha ya milele ; pamoja na huyu mtoto wako. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ *Ndipo maiti achukuliwe kwenda kaburini.*

SEHEMU YA PILI

¶ *Maiti na kaburi hunyunyiziwa maji matatifu, na kufukiziwa uvumba kama kawaida.*

¶ *Huko nyuma waimbe,*
Ant. Vijana.

Zab. 134.

1. Mhimidini Bwana :

Enyi watumishi wa Bwana wote pia.

2. Ninyi mnaosimama usiku :

Katika nyumba ya Bwana.

3. Painulieni patakatifu mikono yenu :

Kamhimidini Bwana.

4. Bwana akubariki toka Sayuni :

Aliyezifanya mbingu na nchi.
Utukufu.

Ant. Vijana waume na wanawali, wazee na watoto : na walisifu Jina la Bwana.

¶ *Wazishi wakiisha kutoka kaburini, Kasisi aseme,*

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amependa, kwa rehema zake nyingi, kujitwalia roho ya huyu ndugu yetu mpendwa N. aliyefariki, sisi tunauweka mwili wake chini ya nchi : udongo kwa udongo, majivu kwa majivu, mavumbi kwa mavumbi : kwa tumaini thabiti, pasipo shaka,

la Ufufuo wa uzima wa milele, kwa Bwana wetu Yesu Kristo ; atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule awezao kuvitiisha hata na vitu vyote chini yake.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Baba yetu.

¶. Usitutie majaribuni.

R. Lakini utuokoe na maovu.

¶. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, umemkubali huyu mtoto wako akae nawe Peponi : Tunakushukuru kwa rehema zako zisizo kiasi ; utujalie na sisi tuonane naye tena katika utukufu wako. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶. Bwana akae nanyi.

R. Akae na roho yako.

¶. Utukufu una Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

R. Ulivyokuwa mwanzo, ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. *Amin.*

¶. Waacheni watoto wachanga waje kwangu.

R. Kwa maana ufalme wa mbinguni ni wao.

Mwenyezi Mungu atujalie sisi, pamoja na watu wake wote waliofariki, tufurahi mbele zake milele.

R. *Amin.*

¶ *Missa ya wafu isisemwe kwa ajili ya mtoto mchanga ; lakini ikitakirwa Missa, siku yenye ruhusa isemwe Missa ya Malaika.*



KUZIKWA MWANAFUNZI

¶ Uvumba na maji matakatifu visitumike ;
wala isisemwe sala yo yote isiyandoikwa chini.

¶ Ndipo Msalisha aseme,

Mimi najua ya kuwa Mkombozi wangu yu
hayi, na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya
nchi. Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa
hivi, lakini katika mwili wangu nitamwona
Mungu. Nami nitamwona mimi nafsi yangu, na
macho yangu yatamtazama, wala si mwininge.

Hatukuja na kitu duniani, tena ni dhahiri ya
kuwa hatuwezi kutoka na kitu. Bwana alitoa,
na Bwana ameondoa ; Jina la Bwana lihimidiwe.

Ant. Kama ungehesabu.

Zab. 39.

1. Nalisema, Nitazitunza njia zangu :
Nisije nikakosa kwa ulimi wangu.
2. Nitajitia kijamanda kinywani :
Maadam asiye haki yupo mbele yangu.
3. Nalikuwa sisemi, nalinyamaa kimya :
Sina faraja, maumivu yangu yakazidi.
4. Moyo wangu ukawa moto ndani yangu :
Na katika kuwaza kwangu moto ukawaka.
5. Nalisema kwa ulimi wangu :
Ee Bwana, unijulishe mwisho wangu.
6. Na kiasi cha siku zangu ni kiasi gani :
Nijue jinsi nilivyo dhaifu.
7. Tazama, umefanya siku zangu kuwa ma-
shubiri :
Maisha yangu kama si kitu mbele zako.

8. Ubatili tu ni kila mwanadamu ingawa
amesitawi :
Bin Adamu huenda tu huko na huko
kama kivuli.
 9. Hufanya ghasia tu kwa ajili ya ubatili :
Huweka akiba wala hajui ni nani ataka-
yeichukua.
 10. Na sasa ninangoja nini, Ee Bwana :
Matumaini yangu kwako.
 11. Uniokoe na maasi yangu yote :
Usinifanye lawama ya mpumbavu.
 12. Nimenyamaza sitafumbua kinywa changu :
Maana Wewe ndiwe uliyeyafanya.
 13. Uniondolee pigo lako :
Kwa uadui wa mkono wako nimeangamia.
 14. Ukimrudi mtu kwa kumkeemea :
Kwa ajili ya uovu wake.
 15. Watoweshe uzuri wake kama nondo :
Ubatili tu ni kila mwanadamu.
 16. Usikie maombi yangu, Ee Bwana, utege
sikio lako niliapo :
Usiyanyamalie machozi yangu.
 17. Kwa maana mimi ni mgeni wako :
Msafiri kama baba zangu zote.
 18. Uniachilie nikunjuke uso :
Kabla sijaondoka nisiwepo tena.
Raha ya milele :
Uwajalie, Ee Bwana.
Na nuru ya daima :
Iwaangaze.
- Ant.* Kama ungehesabu maovu, Ee Bwana :
Ee Bwana, nani angesimama ?

¶ Kisha Msalisha asome,

Ndugu : Kristo amefufuka, limbuko lao waliolala. Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. Kwa kuwa katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa. Lakini kila immoja mahali pake ; limbuko Kristo ; baadaye walio wake Kristo, atakapokuja. Ndipo palipo mwisho, atakapompa Mungu Baba ufalme ; atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu. Maana sharti amiliki Yeye, hata awaweke maadui wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti.

¶ Maiti akiwekwa kaburini watu wasimame kimya, wakimwombea kimoyomoyo.

¶ Wazishi wakiisha kutoka kaburini, Msalisha aseme,

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amependa, kwa rehema zake nyingi, kujitwalia roho ya huyu ndugu yetu mpendwa aliyefariki, sisi tunauweka mwili wake chini ya nchi : udongo kwa udongo, majivu kwa majivu, mavumbi kwa mavumbi : hata siku ya kiyama.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, tunakuomba umwangalie kwa rehema huyu ndugu yetu mpendwa asiywahwi kubatizwa : Umjalie asifungiwe mlango wa mbinguni ; bali apate kibali machoni pak. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Mwokozi wa ulimwengu, uliyetukomboa kwa Msalaba wako, na kwa Damu yako ya thamani, utuokoe, utusaidie, tunakusihi kwa unyenyekevu, Ee Bwana,

SALA ZA KANUNI

AMBAZO YAMFAA KILA MKRISTO AZIJUE

¶ Sala hizi zisemwe kama zilivyoandikwa hapa chini. Kama zimeandikwa vinginevyo katika vitabu vingine vyaa Kanisa letu, vile vitabu na visahihishwe kwa kanuni hii.

1. BABA YETU.

Baba yetu, uliye mbinguni ; Jina lako takatifu litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, Hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki zetu. Utusamehe makosa yetu, Kama sisi tunavyowasamehe waliotukosa. Usitutie majaribuni, Lakini utuokoe na maovu. Amin.

2. SALAMU, MARIAMU.

Salamu, Mariamu, umejaa neema, Bwana yu pamoja nawe ; umebarikiwa kuliko wanawake wote ; na Yesu, uzao wa tumbo lako, amebarikiwa. Mariamu Mtakatifu, Mama wa Mungu, utuombee sisi wenye dhambi, sasa, na saa ya kufa kwetu. Amin.

3. NAMWAMINI MUNGU.

Namwamini Mungu Baba Mwenyezi, Muumba mbingu na nchi.

Na Yesu Kristo, Mwana wake pekee, Bwana wetu, Aliyechukuliwa mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu, Akazaliwa na Bikira Mariamu, Akateswa zamani za Pontio Pilato, Akasulibiwa, Akafa, Akazikwa, Akashuka mahali pa wafu ; Siku ya tatu akafufuka, Akapaa mbinguni, Ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi ; Kutoka huko atakuja kuwahukumu watu wahayi na wafu.

Sala za Kanuni

Namwamini Roho Mtakatifu ; Kanisa Taka-tifu, Katholiko ; Ushirika wa Watakatifu ; Ondoleo la dhambi ; Kiyama ya mwili, Na uzima wa milele. Amin.

4. ROHO YA KRISTO.

Roho ya Kristo, initakase.
Mwili wa Kristo, uniponye.
Damu ya Kristo, inifurahishe.
Maji ya ubavu wa Kristo, yanioshe.
Mateso ya Kristo, yanifariji.
Yesu mwema, unisikie.
Ndani ya jeraha zako unifiche.
Usiniache nitengane nawe.
Na yule adui mwovu unilinde.
Saa ya kufa kwangu uniite.
Uniambie nije kwako.
Nikusifu pamoja na Watakatifu wako.
Milele na milele. Amin.

5. MWENYEZI MUNGU AHIMIDIWE.

Mwenyezi Mungu ahimidiwe.
Jina lake takatifu lihimidiwe.
Yesu Kristo, Mungu kweli na Mwanadamu
kweli, ahimidiwe.
Jina takatifu la Yesu lihimidiwe.
Moyo wake mtakatifu uhimidiwe.
Yesu Kristo, aliomo katika Sakramenti
Takatifu, ahimidiwe.
Roho Mtakatifu, Mfariji, ahimidiwe.
Mama wa Mungu, Mariamu Mtakatifu, asifiwe.
Jina la Mariamu, Bikira na Mama, lisifiwe.
Ahimidiwe Mungu kwa ajili ya Malaika zake
na Watakatifu wake. Amin.

Sala za Kanuni

6. KUOMBEA WAFU.

Roho za waaminifu kwa rehema ya Mungu
wastarehe katika amani. Amin.

7. UTUKUFU UNA BABA.

Utukufu una Baba na Mwana na Roho
Mtakatifu. Ulivyo kuwa mwanzo, ulivyo sasa,
utakavyokuwa milele. Amin.

8. NAUNGAMA.

Naungama kwa Mwenyezi Mungu, kwa Wata-
katifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nime-
kosa sana, kwa mawazo, na maneno, na matendo;
kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya
sana. Kwa hiyo nawasihi Watakatifu wote
waniombee, na wewe, baba, unionbee kwa
Bwana Mungu wetu.

9. Bwana Yesu, unishike mkono, nisitende
dhambi.

10. Mungu Roho Mtakatifu, uniongoze, hata
nimwone Bwana Yesu uso kwa uso.

11. MALAIKA WA BWANA.

Malaika wa Bwana alimhubiri Mariamu :
naye akachukua mimba kwa uweza wa Roho
Mtakatifu. Salamu, Mariamu. etc.

Tazama, mimi mijakazi wa Bwana : na iwe
kwangu kwa neno lako. Salamu, Mariamu. etc.

Neno alifanyika mwili : akakaa kwetu. Sa-
lamu, Mariamu. etc.

V. Utuombee, Mama Mtakatifu wa Mungu.

R. Tustahili kupewa ahadi za Kristo.

Tuombe.

Bwana, tunakusihii, utupe kwa ukarimu
neema yako : Ili sisi tuliojua kwa ujumbe wa
malaika habari ya kutwaa mwili kwake Yesu

Sala za Kanuni

Kristo Mwana wako ; kwa msalaba na mateso
yake tuletwe impaka utukufu wa ufufuo wake.
Kwa Yeye, Kristo Bwana wetu. Amin.

12. MALKIA WA MBINGU.

Malkia wa mbingu, furahi. Haleluya.
Uliyemchukua tumboni. Haleluya.
Kafufuka alivyoahidi. Haleluya.
Kwa Mungu na utuombee. Haleluya.
V. Furahi, shangilia, Ee Bikira Mariamu.
Haleluya.
R. Maana hakika Bwana amefufuka. Hale-
luya.

Tuombe.

Ee Mungu, umewafurahisha wanadamu wote
kwa kufufuka kwake Bwana wetu Yesu Kristo
Mwana wako : Tunakuomba tupewe furaha
ya uzima wa milele ; tukisaidiwa kwa sala za
Bikira Mariamu aliyemzaa. Kwa Yeye, Kristo
Bwana wetu. Amin.

13. MWOKOZI WA ULIMWENGU.

Mwokozi wa ulimwengu, uliyetukomboa kwa
Msalaba wako, na kwa Damu yako ya thamani,
utuokoe, utusaidie, tunakusihi kwa unyenyekevu,
Ee Bwana.

14. AHIMIDIWE YESU.

Ahimidiwe Yesu Kristo, na kusifiwa, na
kutukuzwa milele ; ameketi katika kitit chake
cha enzi mbinguni, naye yumo katika Sakramenti
yake Takatifu madhbahuni.